.’,

# SAFARI

## YA MAUTI

**Gitonga MURIANKI**

*Riwaya*

# SAFARI YA MAUTI

**©Gitonka Murianki 2022**

Imechapishwa kwa mara ya kwanza 2022.

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku na hatia kwa wenye silika za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya waandishi kupitia kwa wakili wao.

Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume cha sheria ataweza kushtakiwa.

**ISBN : 9798371305114**

**Mhariri:**
Kaka Fred: **+254716349065**
Baruapepe: **kakafred25@gmail.com**

**Mwandishi:**
Gitonga Murianki: **+254713196298**
Baruapepe: gitongawillys@gmail.com

# Yaliyomo

Tangulizi ........ iv
Sura ya Kwanza ........ 1
Sura ya Pili ........ 9
Sura ya Tatu ........ 18
Sura ya Nne ........ 30
Sura ya Tano ........ 37
Sura ya Sita ........ 56
Sura ya Saba ........ 68
Sura ya Nane ........ 74
Sura ya Tisa ........ 83
Sura ya Kumi ........ 95
Sura ya kumi Moja ........ 102
Sura ya kumi na Mbili ........ 107
Sura ya kumi na Tatu ........ 117
Sura ya kumi na Nne ........ 128

# Tangulizi

Muungwana hanuni mashavuni ila hununa moyoni naye Malenga hununa kwa ughani wake. Riwaya hii itampa msomaji hamu ya kila aina. Kimesuka maudhui yanayokumba ukuaji wa kijamii mathalani; Ufisadi, Uhawinde, Utamadunu, Elimu, Nafasi ya mwamke katika jamii, Teknolojia, Uhasama, Mauko. Mwandishi ameikuza lugha yetu ya Kiswahili inayotumika sana katika nchi ya Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi, Afrika ya Kati, Afrika Kusini na kwingineko duniani.

Utapata funzo la kuhamasisha kutoka kwa wahusika mbalimbali mfano; Maisha ya Dharura na mwanawe Nafuu yatakupa uvumilivu wa maisha. Kalatu anakupa kila sababu ya kujituma katika gange zako za kila leo.

Mwandishi amedhihirisha visa hai vinavyofanyika katika jamii zetu. Mbona tuandikie mate ilhali kuna wino?

Kaka Fred

# Sura ya Kwanza

Kituturi chenyewe kilikuwa kimejibari na kujiinamia kiasi cha kuanguka, labda kutokana na umri au kutokana na hitilafu za kiufundi. Mlango haukufunguka vyema kwa kuwa komeo na shimo lake vilitalikiana wakati ukuta wa nyuma wa chumba hiki ulipoanza kupinda mgongo huku kuta zingine zikifuata nyayo. Kwa mwonekano, kilikaa kama gari lililobeba kupita kiasi mlimani.

Nafuu - msichana wa miaka minane hivi - alikuwa akibarizi nje ya kibanda hiki. Alivalia rinda ambalo nashuku lilikuwa jeupe siku moja. Vazi hili limekuwa bendera ya nchi huru. Halibadilishwi. Sasa limejaa matundu kama chandarua cha mbu. Wajihi wa mtoto huyu si wa mtoto. Unaonekana kama wa mtu mzima aliyeona sura zote za madhila ya maisha. Hakupata kule kuengwaengwa na kudekezwa kwa mtoto wa kawaida. Mustakabali wake ulikuwa kwenye kamba iliyotishia kukatika. Kama mtoto alikuwa katika hali hii ya kutamausha, sharti ujue yaliyo na mama yake Tija ni makubwa. Mama huyu hakuwa mtu ila mkusanyiko na mrundiko wa uchochole, mateso na visirani uliovuviwa na kupata uhai. Mrundiko huu ndio ulioharibu kabisa sura yake nzuri isipendeze. Mwanamke huyu alijawa na hawafu ya kuishi. Kesho yake ilikuwa fumbo gumu alilohofia kulifumbua. Pale alipofikia mama huyu, maneno kama mapenzi, udugu na imani hayakubeba maana yoyote kwake. Yalijaa unasibu uliokejeli nafsi na hisia.

Nafuu aliyatunga macho yake mwembeni, kwa mwonekano akaingiwa na magezo fulani akilini. Aliangalia upande uelekeao barabarani, tena akakaza macho mtini. Mara hii kwa makini zaidi kama aliyeona kitu fulani kule juu. ‘Mwembe mzima huu una tunda moja tu? Una faida gani? Heri ukatwe! Nitamwambia mama akirudi aukate, labda tupande mboga’alijiambia nafsini. Alipoliangalia lile embe moja ndogo tena, mawazo yake yakachukua mkondo mwingine. ‘Lakini, huu mti umezaa tunda moja tu makusudi? La, mpaka kuwe na shida. Shida kubwa. Si bure kumpata kijana kibogoyo. Hili embe nalo mpaka lina upweke. Maskini ona lilivyo na umbo nzuri kama moyo wa binadamu. Mimi na hili tunda tu wamoja! Mti mmoja mkubwa tunda moja, mama mmoja mkubwa mtoto mmoja! Labda pia lina njaa. Hakujanyesha karibuni. Mbolea pia ni ndogo’. Alizidi kuwaza. Kitambo kidogo Nafuu alimwona mdudu aina ya

mboza akipita juu karibu na tunda lile. Akachukua kijiti kumrushia huku akijiambia ‘Mpaka awe ni huyu mdudu mshenzi ameyaangusha maua yote yasifike kutoa matunda. Mpaka ni yeye anayeyafanya maembe madogo mapooza na kuyapukutisha’. Kwa kufikiria hivi akakumbuka kitu na kuanza kulia.

Tija mamaye Nafuu alitokea mandharinyuma ya kibanda chao. Hapakuwa na uzio maalum. Angepitia upande wowote na kujipata kwa majirani kuomba hiki au kile. ‘‘Nisamehe mwanangu, nimekuweka sana hujafungua kinywa. Acha kulia. Njoo na majani makavu tukoke moto. Mbalu alikataa kunipa ujira wangu wa jana niliouendea tupate kifunguakinywa. Nilisahau kumwita mheshimiwa katika salamu. Amenikata shilingi ishirini kwa hilo” Tija alijibu huku akiinjika sufuria mekoni.

Nafuu alinyamaza kwa muda, akapinduka na kuangalia kule mwembeni. Machozi yalianza kumpofusha. “Yule nzi anazidi kulizunguka lile embe” Nafuu alimwarifu mama yake kwa sauti ya kuvunjikiwa. “Eti nini Nafuu, embe gani?” Mama alimkagua mwanawe kwa macho akishangaa kilichomsumbua. Alijishughulisha na mapishi maadamu alichelewa sana. “Mama utaukata ule mwembe nikikuambia uukate? Mwembe mkubwa hivyo una embe moja dogo tu! Halafu mama, kuna nzi anayetaka kula hilo embe.” Wakati huu Tija alikuwa akiepua chai yake ya mkandaa. “Hahaha! Eti Nzi kala embe. Atakuwa wa ajabu huyu.” Tija alimtania bintiye. “Utaukata?” Aliuliza Nafuu kwa mkazo zaidi. Tija sasa alitilia maanani swala hili. “Mbona niukate? Kwa sababu una tunda moja? La, kumbuka vile ulivyozaa mwaka jana. Tulikula mengi na mengine tukayauza. Hilo vazi ulilovaa lilinunuliwa kwa mauzo ya maembe hayo. Mabati ya nyumba hii ni ushuhuda kwamba mwembe huu bado ni muhimu kwetu. Kabla ya kuijenga hii nyumba tulikuwa tukiishi katikati ya migomba ile pale, tulipofukuzwa kwa mjomba wako Chui kwa tetesi za kula sana na choo chake kujaa haraka, sikuwa na pa kupaita nyumbani. Nilizunguka kijijini nikiokota matambara ya kila aina kama kichaa, nikaifanya migomba mifumbati na kwa mabati makuukuu ya chumba kilichokuwa chetu na marehemu bibi aliyezikwa pale, nikajiundia kiota tulimoishi. Mwanangu kama ulitoboa katika uyabisi na mvua wakati huo ukiwa na miaka miwili tu, hakuna baya litakalokupata maishani. Lakini baba yako namwachia mungu...” Tija alisema. “Baba ni mzuri. Tukipatana naye dukani huninunulia pipi.” Nafuu alidakia. “Huyo ni…” Tija alikumbuka Nafuu bado alikuwa mdogo wa mambo kama yale,

akabadilisha mkondo wa mazungumzo. ‘‘Shika hapa. Kaimati za Kalatu huwa tamu sana, najua utazipenda”

***

Ni miaka sita tangu mzee Mbaara amfukuze mkewe Tija. Tija alikumbuka kama jana siku aliyotembezewa mkono baada ya kuchelewa kanisani kulikokuwa na mchango wa kujenga kanisa jipya. Kwa sababu ya shughuli za harambee, waumini walifumukana mwendo wa saa tisa unusu. Kwa kawaida ibada huisha saa sita na Tija kukimbilia nyumbani kumtengenezea mumewe chamcha. Aliyajua majukumu yake ya boma alivyojua jina lake. Daima hungemwona akisimama na kina mama wanzake kujuliana hali. Walipomwuliza angewaambia *‘Nina dharura’* Mazoea ya kusema hivi yalimzalia jina. Akaitwa *Mama Dharura*. Jina hili likasambaa kama moto nyikani hata kulimeza jina lake halisi. Akawa Dharura tangu kipindi kile.

Siku hii alimpata Mbaara amemeza swila, macho yamemtoka pima kwa hamaki au labda kwa ulevi wa chingamu iliyokuwa mdomoni. Alipomtia machoni kwa mbali alisimama kutoka alikokuwa ameketi kijiweni nje ya chumba chao na karibu na alipomfungia ng’ombe wao, Zebu. “Umefika eeh? Inaonekana ibada ilipamba moto leo. Funzo kuu?” Aliuliza kwa kejeli. *Dharura* hakuwa tayari kwa jambo ambalo lingemharibia siku yake. ‘‘Kupendana,’’alijibu kwa upole bila kujua kilichokuwa kikimkodolea macho. “Kupendana! Ndio maana hasa … sasa huo muda wote mmekuwa mkifanya mapenzi?” Aliuliza Mbaara. “Ah! Yapi hayo nawe mume wangu. Tulikuwa tunafanya pia…” “Mazoezi ya mapenzi!” Mbaara alidakiza kwa hamaki.’’ “Mbaara, mbona hauchunji maneno yako leo, hata hausubiri kusikia?” Tija alilalamika. “Nisikie nini mjinga wewe! Nimechoka na unavyojipodoapodoa siku hizi ukienda huko, migorogo imekutawala sana. Una nia ya kumfurahisha huyo mhubiri wenu daktari wa mahaba? Nilikuambia sitaki uende huko, bado unayeyukia huko kwa mahaba. Kweli mapenzi ni ulimbo. Mimi mumeo hunioni tena, nimekuwa kombamwiko, kinyonga mgonjwa asiyeweza masafa hasa! Mimi kwako ni Nguchiro mwendawazimu. Ni mume wa nani hajapata chamcha saa hii? Ni nyumba ya nani haijaona ufagio? Nilijua tu baada ya muda utakuwa kinusapesa kama wanawake wengine. Ulidhani nimeficha pesa za marehemu baba yangu katika hizo benki zako za ndotoni.” Mbaara sasa alikuwa anahema kama mkufunzi wa mazoezi ya viungo mbele ya wanafunzi wake. Mwanamke ni mwanamke tu. Ni kimelea mtegemea jasho la mwanamume. Daima hujiona aliye na haki ya juhudi za mwanamume. Mapenzi, kwake

hutumia pesa na cheo kama kawi kudumu. Anavyong'ara na kutononoka utadhani ndiye mwenye chumo!" Mbaara aliendelea kumdhalilisha mkewe kwa maneno makali. Hasira nayo ilineemeka moyoni na kumdhibiti mzimamzima.

Muda huu wote, Dharura alimkazia macho makavu. Mgongoni alikuwa amemfunga mwanawe. "Hata huongei tena bata mgonjwa wewe!" Mbaara alifoka. "Acha kufanya hasira bwana. Tulia tuelewane tusonge mbele. ''Dharura hangezificha tena hasira zake. "Tulia tuelewane tusonge mbele… Naona mmefundishwa ushairi pia!" Mbaara alisema kwa kebehi. "Tulichelewa katika mchango wa kujenga kanisa letu la kisasa." Tija akisema. "Mmh! Huyu zuzu pia anachangiwa ajenge duka eeh…" Mbaara alisema huku akiwasha msokoto fulani. "Sijasema duka. Nimesema kanisa ah! Dharura alizidi kupandwa na ghadhabu" Na tulisema usiwe ukivutia hiki kitu karibu yangu?" Dharura alilalamika huku akisonga mbali. ''Umesemaje? Mmeambiwa pia mtudharau sisi waume zenu eh...!''Mbaara alisema haya huku akimpiga mkewe makofi mawili. Dharura alisepetuka kama aliyetaka kuanguka lakini kwa bahati akafanikiwa kuketi. Alilia kwikwikwi. Mtoto aliyekuwa kalala mgongoni muda huu wote aligutuka na kuchangia kilio kwa mamaye. ''Siwezi kukaliwa na kinyangarika mimi. Nimechunwa jogoo sawasawa!" Baba mtu alisikika akifoka akifuata ujia utokao barabarani.

Hii haikuwa mara ya kwanza kwa Mbaara kumpiga mkewe. Alimpiga, akaenda kwao na baada ya siku chache hasira ikapungua na kurudi kwake, kwa matumaini ya kujenga boma lake. Nikisema kwao si nyumbani, ni mahali ilipokuwa aila yake na walipoishi na bibi kabla ya mauko yake. Ni kibanda alimopigana na majipanya kila alipokwenda huko kwa siku chache kabla ya kumwachia uhuru wa muda. Marehemu bibi yake alimwambia siku moja kwamba familia ni mke. Mke naye ni mhanga. Hujitolea siku zote kudumisha ndoa yake. Kila alipokumbuka hili hasira zilimwambaa na joto la huduma kumparamia, akachukua virago vyake na huyoo kwa mumewe. Mara nyingi aliapa kutorudi na bado akajipata kwake na huyo tu Mbaara wake mwingi wa vituko na vitushi.

Muda huu alihisi kuchoka. Ndio, mwili na roho. Alihisi kudhalilishwa na mtu aliyempenda na kumdhamini. Akaishiwa na nguvu. Akahofia mustakabali wake na wa mwanawe; Nafuu! Nakuwe huko kuwa mhanga, lakini pia mhanga anapovamiwa na adui aliyempiku nguvu hutorosha nafsi yake. Kuishi na mtu kama huyu afadhali kuishi na

mwendawazimu. Mtu ambaye angeraukia kileo na usiku wa manane arudipo nyumbani ni fujo na kutaka chakula asichojua kilikotoka.

Gharama ya uraibu huu bado ameitundika barabara mabegani mwangu. Singeweka senti moja hivi kwa nyumba. Ni kana kwamba anahisi harufu ya pesa. Shamba nalo humuuma, haingii mle ila mazao yanapoiva akiyauzia shambani na kutuacha katika utashi wa ubao. Mhanga amechoka! ‘Heri kumbeba nungunungu mgongoni kuliko kuishi na baradhuli.’ Alijisemea bado tu pale alipoketi baada yale makofi ya mumewe. Dharura alihisi uzito wa ulimwengu mzima begani mwake. Alijitolea kuilinda familia yake kwa adha zote ila si kwa mauti yake au ya mwanawe.

Aliporudisha fikira nyuma aliona giza nene, akitazama leo yake akaona heri jana. Kesho ilikuwa moto usiozimika. Heri moto, moto usiojua aliyeuwasha! Dharura kwa mara ya kwanza akaingiwa na chuki kwa mumewe aliyemuenzi tangu walipooana yapata miaka kadhaa iliyopita. Akamwona kiumbe dhalimu asiyestahili mapenzi; mnyama aliyawapiku wanyama halisi.

Alikumbuka ndoto aliyoota siku ya kwanza alipohamia kwa Mbaara. Alivyoparamiwa na simba jike aliyekuwa na ari ya kumla. Kwanza alimwona kama paka mdogo wakupendeza. Akaazimia kumhifadhi na kumtunza kwake. Alipokuwa akimkaribia kumchukua alibadilikia mikononi. Akawa Simba! Yule hayawani akasimamana naye, miguu ya nyuma imejikita chini na ile ya mbele inamparura uso. Naye kwa ujasiri usioeleweka alimshika kichwa na kukigotesha ukutani aliposimama. Meno yake yote yakang’oka. Yule simba alimtishia kwa makucha yake makali. Dharura akaishika ile miguu na kuigotesha ule ukuta kucha zikang’oka. Simba akawa hana nguvu tena bali hakufa. Ndoto hii sasa ilimtia uyabisi fulani mwilini.

“Mie nimechoka! Punda ameutua mzigo! Habebi tena! Sitaki kuua wala kuuawa! Hili guu la mwisho hapa kwako mwanamume.” Mbaara aliyekuwa ashafika barabarani alisikia hilo. Akashtuka kidogo. Hakuwahi kusikia udhabiti wa aina hio katika sauti ya mkewe. Potelea mbali. ‘Mwanamke ni mwanamke tu. Mara ngapi alisema vile na akarudi’. Alijisemea moyoni akiendelea na safari yake iliyokomea ulevini kwa mama pima. Dharura akaingia nyumbani na kutoka na alichoamini kilikuwa chake na kwenda kwa ami yake Chui.Wakati huu Nafuu alikuwa amelala. Alipolia kuonyesha umoja wake na mama alipopokea pigo lile, alinyonya na kurudi usinginzini. Maskini malaika huyu, hakujua yeye ni abiria katika mashua baharini kwenye dhoruba kali kama si abiria wa

ndege iliyomea itilafu za kimitambo juu ya bahari Hindi. Alitulia tu mgongoni.

Kule kwa Chui matumbo yakawa mengi. Chui akamtolea Dharura makucha. Hivyo ndivyo Dharura alivyojipata wakilala shambani mwake mwa uridhi katikati ya migomba na mwanawe Nafuu. Kibanda walichoishi na bibi kilikuwa kimebomoka kitambo. Aliokota matambara ya kila aina, akatumia ufundi wote kujiundia makao. Akaweka chumba chake paa, dirisha hata mlango, migomba nayo ilikuwa mifumbati. Huku ni kule kuliama la mbwa ukikosa la mama.

Mbaraa alibaki mpweke kama aliyefiwa. Mchwa nao walikitafuna chumba chake kwa shangwe. Hivi sasa kila mahali kulikuwa madirisha. Aliye ndani hakuwa na faragha. Mgeni hangehitaji kubisha kujua kama mwenyeji wake alikuwa ndani au la. Aliyekuwa ng'ombe wao sasa ni fremu zenye uhai. Akiinama kula alionekana ngozi iliyoanikwa kwenye vigingi vinne. Ungemwona Mbaara kwa jagi isiyojulika rangi yake kwa uchafu amemwinamia yule ng'ombe ati anamkama. Kuvuta tu chuchu ng'ombe mzima angeporomoka!

Wanakijiji walisikika wakisema mwanaume huyu alirogwa, wengine wakasema ni laana ya mama yake mzazi. Wale wa dini kama akina Dharura walisema ni laana ya kumtusi nabihi wa Mungu.Walikumbuka kwa masikitiko shamba la Dharura. Halikuhisi mabadiliko ya majira. Daima lilikuwa na mboga za kila aina. Migomba ya shamba hili haikuisha mikungu ya ndizi bila kutaja mitunda mingine kama mifenesi, miparachichi na mipapai.
Ng'ombe wake mmoja alitoa lita ishirini kwa siku. Wanakijiji wengi walifaidi maziwa yake. Muone sasa, yeye na Mbaara walikuwa katika ligi moja. Tabia ya mzee huyu imekuwa kuni zilizopika chakula jioni na mbalamwezi iliyowaweka wazee barazani.

Wale waliosema kwamba alilaaniwa na mama yake walikuwa na sababu nyingi za kusema hivyo. Hata wewe jiulize, ni mzazi yupi angefungiwa kwa nyumba ateseke hadi kufa kwa njaa, kiu na jeraha la mguuni asilaani?

***

Mbaara alikuwa kitindamimba wa Bwana na Bi Mutua. Mutua alikuwa mwanasiasa wa kitambo aliyeng'atuliwa kitini na mbalu. Kando na hilo, alikuwa mwanabiashara mashuhuri. Aliposhindwa na Mbalu aliamua kustaafu siasani na kushughulika na biashara yake ya kuuza dhahabu iliyolanguliwa kutoka Afrika ya Kusini. Wanaoendesha biashara

kama hii ni kina Mamba na Papa. Nyonyo zao huwa zinapiga kwa mapigo ya madini na fedha. Hawa na walanguzi wa mihadarati ni kama pacha kwani msabaha wao ni mkubwa. Ni biashara inayohusisha kuua na kuuana, kulaghai na kulaghaiwa. Aghalabu mwuzaji na mnunuzi hawapatani macho kwa macho kwa sababu za kiusalama. Kaka yake Mbaara aliuawa katika biashara hii aliyofunzwa na baba yake mzazi. Alikuwa ametumwa na baba kuwasilisha mali hii kwa mteja wao mmoja Mnaijeria. Jamaa huyu alipopokea dhahabu na kumpa pesa alimvizia tena akamwuua na kuzichukua tena zile ngwenje. Mutua alifariki katika ajali ya ndege kule Duale Kameruni katika harakati za kumtafuta jamaa huyu alipize kisasi. Inasemekana kuwa Mnaijeria huyu alikuwa na macho yake humu nchini katika uwanja wa ndege na hivyo Mutua alipopanda ile ndege ya mauti, Ijeke alipata ujumbe na pale akaamua kumwangamiza huyu hasidi wake pamoja na abiria wengine. Mbaara akaachwa na Mama-mhandisi wa mitambo-aliyekuwa amepofuka kutokana na ajali katika kiwanda fulani cha kutengeneza sabuni. Mbaara alikuwa mpenda anasa kweli kweli. Aliondokea kuwa limbukeni. Angemwacha mama yake na kijakazi na kwenda tafrija zilizochukua siku nyingi. Hakuna tamasha ya muziki ingempita humu nchini labda ziwe mbili wakati moja. Katika safari zake hizi mara nyingi angekodi ndege na kuwatumbuiza marafiki zake wengi kwa gharama yake. Alivaa mavazi ya maelfu ya pesa bila kutaja mikufu, bangili na pete za dhahabu zilizokuwa za marehemu baba yake. Hangekula katika magenge tunayoyaita hoteli. Sifai nikueleze alivyowanasa vidosho kwa sumaku pesa. Gharama ya matumizi yake kwa siku ingeulisha ule mtaa wetu kwa mwezi baada ya kumlipa kila mtu, mpaka mwendawazimu wa pale mshahara wa haja. Kijana huyu, katika maisha haya yake ya peponi, alitangamana na kutagusana watoto wa watu waliostahili kuitwa watu si wa viroboto akina mimi na wewe.

Shida yake kubwa ni kuwa alizifanya pesa zake kuwa tasa. Kwa wakati fulani hela zilizokuwa kibindoni zilikwisha, akaanza kuuza ploti na mali nyingine kukidhi mahitaji yake ya kiwango cha juu.

Mama mtu aliumia; kwanza, kwa kufiwa na mume na mwanawe katika chini ya muda wa mwaka mmoja, pili, kuwa kipofu jambo lililomfanya kukosa huduma za msingi hali alikuwa mwenyenacho. Mara tu, Mbaara alipotoka zake naye mjakazi alijitawala, akawa kiguu na njia. Aidha, kijakazi huyu aliwaleta marafiki zake wa kiume na kike na kuwaburudisha kwa mazuri jumba lile. Wakala wakanywa, mwenye nyumba naye akashiba harufu tu ya maposhoposho. Wakati mmoja mama huyu akitoka hamamuni aliteleza na kuvunjika mguu. Kwa kukosa wa

kumsaidia alijikokota kwa kupapasapasa hadi kochini. Mjakazi aliporudi keshoye alicholalamikia tu ni kwa nini mtu mzima alijiendia haja kubwa na ndogo kama mtoto. Mbaara alipokuja alipata mama yake yu dhaifu kwa njaa na maumivu yasiyosemeka. Hakuwa na nguvu za kumgombeza mjakazi ambaye hakuwa amelipwa kwa miezi mitatu sasa. Pale alipokuwa Mbaara hakuwa na senti mfukoni. Alikuwa ameuza kila kitu isipokuwa pale walipopaita nyumbani. Bima ya afya nayo ilikuwa haijalipwa kwa muda sasa.

Kiwango cha sukari cha mama kilifanya kupona kwake muhali. Gharama za matibabu ya mama yake zilimfanya akauze nyumba na chochote kilichokuwemo. Mama naye akafia sadarukini. Lakini kabla ya hajafariki alimwita mwanawe na kumwambia, "Mwanangu, umekula raha zote sasa ngoja karaha, kila chozi nililolia juu yako utalilipa, tone kwa tone. Kwa hundi nono ya yasiyoandikika. Buriani mwanangu"

Masahibu wa Mbaara waligeuka umande jua lichomozapo pale mifuko yake ilipotoboka. Sarafu zilizosalia kutokana na mauzo ya nyumba ile alijinunulia kikataa alichoishi. Pale, kumbukukumbu za maisha yake ya awali zikamtwaanga bila huruma. Hizi ndizo zilizomkitisha ulevini, daima aliogopa kuwa yeye. Akaishi muradi alikuwa akipumua. Kupata mlo mmoja kwa siku ilikuwa neema nadra.

Dharura alikuwa chini ya mwembe pale nyumbani kwake akichambua mchele wa chamcha. Siku hii hakuenda kazini katika genge la Kalatu alipokuwa amepata ajira kama mpishi. Hii ni kwa sababu mwenyewe alikuwa ameshikwa na polisi kwa kutokuwa na stakabadhi za afya zilizohitajika kuendesha kibarua hicho. Afisa wa afya ya umma alitaka elfu mbili za kunyooshea mambo japo ziliadimika. Kalatu alikuwa radhi kutoa chauchau ila Dharura akamzuia. Alibebwa na kupelekwa korokoroni kwa kuhatarisha afya ya umma. Afisa huyu alimsingizia kuwa mmoja wa waliowapikia watu nyama ya mbwa na fisi. Ni juzi tu ngozi na kichwa cha fisi vimepatikana si mbali sana na ilipokuwa biashara ya Kalatu. Msako mkuu ulianzishwa kuchunguza na kutadhmini hali ya magenge, hoteli na buchari kote Tunu.

Kushikwa huku kwa Kalatu kulichangia Dharura kuchemkwa na hasira. Kukamkumbusha dhuluma nyingi alizopitia mikononi mwa watu. Akakumbuka aliyopitia mikononi mwa mumewe pamoja na yale ya Chui na Mbalu. Hasira na chuki zikamsakama kooni. Wazazi wake waliuawa na umma. Baba yake Dharura alikuwa mrina asali katika msitu wa Hidaya. Hii ndiyo iliyokuwa kazi iliyoilisha familia yake. Si kula kushiba ila kuhakikisha tu nyoyo zilipiga damu milini. Siku hii ya mauti, alikuwa katika shughuli zake msituni. Akafika kijijini saa za alfajiri. Kumbe kutokana na magwada yake duni aliyotumia kurina, nyuki wengine walipenyezapenyeza hadi ndani katika nguo zake. Nyuki mmoja msi adabu alipofika sehemu fulani mwilini mwa baba mtu akamwuma. Mzee akarusha asali chini pamoja na vifaa vyake vya kazi.

Kitendo hiki kiliwakasirisha nyuki wengine waliokuwa mwilini na katika safari za kusikojulikana mavazini mwa mrina asali huyu. Wakaanza mashambulizi kwa hatamu jambo lililomfanya baba Dharura kuyavua mavazi yake yote na kuanza kurukaruka na kukimbia hapa na pale. Kurukaruka huku na ile miguno ya “*Ah*!” na “*Oh*” iliamsha jirani mmoja ambaye ndio alikuwa anawahi lepe la usingizi kutokana mtoto wake aliyelia karibu usiku wote. Mtoto huyu ameugua kwa siku mbili sasa. Naye mama yake angemkazakaza hirizi iliyokuwa kiunoni na kusema maneno fulanifulani. Muda ulivyosonga ndivyo mwana huyu alivyozidiwa. Sasa alikuwa amelala na kumpa mama nafasi ya kufunga jicho, Kitambo kidogo alisikia vishindo vya yule mrina asali. Akatoka nje polepole kuangalia kilichokuwa kikijiri. Alipomwona baba mtu uchi wa mnyama, alipiga kamsa iliyokileta kijiji kizima pale. Maskini mzee huyu

hakuwahi kujieleza kabla ya kuvamiwa na umati uliokuwa na ghadhabu na kipigwa kipopo hadi kufa. Kisha na maana ni kuwa alikuwa mchawi asiyestahili msamaha. Umati ule ulifululiza hadi kwake na kumvamia mkewe pia na kumuua. Nafuu na Kanini waliponea kwa kuwa walikuwa kwa bibi yao yapata maili tano kutoka pale.

Kulipokucha nguo na asali yake baba mtu vilipatikana mita chache kutoka mahali walipompokea uhai. Kijiji kizima kilijawa na aibu isiyomithilika kugundua jinsi hukumu yao ilivyowapotosha. Dharura akakumbuka haya kama alivyohadithiwa na bibi.

Hasira ya maonevu na chuki vikamtia katika ulimwengu mwingine. Wingu kubwa nzito la mawazo likamgubika mzimamzima. Nafuu alikuwa akichezea vijiwe pale mbele yake lakini mamaye hakumwona kabisa. Kama mtu aliyepandwa na jazba alianza kusema akilini mwake:

'Nachukia, ndio nachukia dhuluma. Dhuluma dhidi ya wanyonge. Wenye nguvu kuning'ing'iniza haki za wayonge mkononi kama kicha cha funguo na kuzichezea kama mtoto achezeavyo gololi. Kujifanya wamiliki na wagamvi wa haki zote. Mpaka ya kuishi! Wakajitweza mamlaka ya kuua na kuongezea idadi ya mayatima na wajane wa kudharauliwa na haohao wauaji…Nao mahakimu bandia, wanaotoa hukumu hizi nawachukia kuliko mauti. Nachukia dhuluma ya tajiri kumnyima ujira mfanyikazi wake hata wa pesa kidogo. Nachukia matajiri maskini wasioshiba kula vya wachochole waliowanyong'onyesha na kuwafyonza damu. Wasiotosheka na mamilioni kwenye benki hata wanyakue shilingi ya mjane. Naam, hao wanaosifu njaa kudharau shibe... Mapenzi nayo ni upuzi mtupu, ni ujinga wa kuzaliwa nao. Ni ugonjwa wa hisia mseto; kumpenda anayekuchukia na kuchukia anayekupenda. Kama huu si ugonjwa basi ni uchawi wa mchawi hatari aliyekiroga kizazi cha binadamu na akafa. Au tuseme ni laana ya mazimwi fulani. Kupenda leo kesho huhisi penzi la jana. Mapenzi ya misimu na majira afadhali chuki. Ukipenda penda kwa dhati uliyempenda na uache kumtosa ushuru kwa mapenzi. Lakini pia penda kwa macho wazi, masikio nayo fungua, moyo nao ujaze tahadhari usije kubaki skrebu ya dunia yakikufika. Dunia haina mageni; matukio yake na mifumo hujirudiarudia. Penzi ni kama elimu isiyo na mwalimu wala mtaala, hivyo, ukipenda kuwa tayari kujiwajibikia penzi.

Nachukia, chuki ya mtu kukosa usingizi kilingeni. Kumchimbia na kumhesabia mashimo yanayomtosha hata asiye mdeni au mpinzani wake. Mja kuchukia sababu ya kuchukia tu…Nawe Mungu mbona ukatupa mapenzi tuumizane kwa hisia na matarajio tusiyoweza kumudu?

Kutesekea wanaotutesa. Nakuomba yakifa mapenzi mengine yote uniachie ya mwanangu'

"Mama unaumwa!" Nafuu alibabaika alipomwona mamaye alivyotoa jasho huku uso umejaa makunyanzi kama ya nyati na mishipa ya pajini kututumka. ''Mmh, hapana mwanangu" Dharura alijibu huku pumzi zikimtoka kama mpigana masumbwi ulingoni. ''Nikupe maji?'' Nafuu alikimbia na kumletea mamaye maji kwa kikombe kuukuu cha plastiki. "Usijali mama, Kalatu akiachiliwa kesho utarudi kazi. Utapata pesa za kuninunulia sare ya shule nirudi tena shuleni.

Nataka kusoma niwe daktari rubani ama daktari mwalimu. Mtoto akigonjeka shuleni nampa dawa hapo hapo. Si kumtuma nyumbani. "Mama, ni kweli zahanati ya kijiji haina dawa? Nafuu alimhoji ''Ndio nani alisema hivyo?'' Mama akamwuliza. "Hanna rafiki yangu alipelekwa huko, daktari akamwambia zimeisha lakini akamwelekeza kwa zahanati ya Dr. Mwamba." Binti akamjibu mamaye. "Kweli?''mama alisaili. ''Eeh! Halafu baba yake akamwambia mama kuwa zile dawa za Mwamba zilikuwa na nembo ya hospitali ya umma." "Dunia ina maovu mwanangu. Ishi utayaona." Dharura akamjibu mwanawe. Nafuu akakumbuka lile embe moja akapinda shingo juu kuliangalia kisha akamwambia mama, ''Mama, nachukia yule nzi aliyetaka kuliuma lile embe.'' Mama mtu alishtuka kidogo kwa mshabaha wa mawazo yake ya chuki na ya mwanawe. Alihofia kama alitamka baadhi ya mawazo yake akasikia.

Alianza kutambua kuwa Nafuu alizungumzia sana juu ya mwembe na tunda lake moja. Kwake yeye hakuona ajabu kwani wakati mwingine miembe huangusha maua na isiwe hata na tunda moja. Kilichomgutusha ni jinsi mtoto huyo alivyojifananisha na embe lile.

Kwa kiasi alijaribu kuchunguza msemo wa mwanawe. Mbona mti mkubwa kuangua tunda moja? Matawi na majani yamejaa. Majani yakiwa mengi huongeza uzalishaji wa chakula kutumia mwangaza. Mti ulivyo na uwezo wa kutengeneza chakula kingi ndivyo ulivyo pia na uwezo wa kuangua zaidi. Matawi nayo uhimili uzito wa majani na matunda. Shina nalo hubeba uzito wa matawi, majani na matunda. Mvua isipokunya majani hujitolea mhanga. Yakajipukutisha kuokoa mti. Ukifika wakati huu huwa hayang'ang'anii kubaki. Yanang'ang'ania kupukutika kwa heshima na hadhi kama wazalendo waliopigania uhuru walivyojitoa vitani tukawa huru. Haya majani huishi upendo wa dhati kwa mama mti yaani *''For better for worse.''*

“Waama adui mkubwa ni yule anayepigana na mizizi. Ukiona mti usio na matunda wakati wa majira yake si ukaidi; chunguza mizizi. Ukiona hauna matawi au majani yenye afya, chunguza mizizi. Chelewesha hukumu yako. Kuna adui anayestahili si chuki tu bali vita. Kweli, huu mwembe wangu una shida…ndio, ukimwona mzee ametimua mbio jua kuna kioja! Adui wa pili ni yule wa matunda. Kila ua linapochanua analiparamia na kuliangusha. Tunda linapochomoza uani analipatia ulemavu. Huyu ni adui wa kizazi. Adui wa juhudi; wa maendeleo hasa! Tunda halina hatia kuubeba uhai wa jamii ya mti wake, kukibeba kizazi cha halafu. Aidha, halina hatia kuburundisha mwenye kupanda mtunda. Kumtia tabasamu ya ufanisi. Hasidi wa sampuli hii hastahili msamaha. Laiti mwenyewe angalijua angaliliambia tunda, “Tunda langu jihadhari. Adui ni wengi, usilaghaike kwa kicheko. Kicheko si penzi.” Mwanangu yuko sahihi kusema mwembe huu una shida.

***

“Sasa mzee uliyavulia ngoja uyaoge,” Mwenge alimwambia Kalatu. “Mimi sina pesa. Elfu mbili kwa hili genge langu kwangu ni nyingi. Hizi pesa tena si eti ni cheti. Ukikakaa tena utarudi kuchukua nyingine. Hivi mbona huna imani? Nipewe hicho cheti pia mimi nakihitaji. Tangu nilipochukuliwa vipimo hospitalini pamoja na wafanyikazi wangu bado hatujapata. Kila mara ni kuja kesho kuja wiki ijayo.” Kalatu alijibu kwa hasira za kadri. ‘‘Basi huna budi kwenda kortini kwa kuhatarisha umma leo.” Mwenge alifoka. ‘‘Haidhuru.” Kalatu alisema huku akitoa simu mfukoni na kumpigia Mbalu shemeji yake. Alimweleza kifupi yaliyomsibu na kumaliza gumzo. Kitambo kidogo simu ya afisa yule ikakiriza.

Baada ya mazungumzo yao Mwenge aliregesha simu mfukoni kwa hasira iliyokuwa wazi machoni. Midomo yake ilichezacheza kwa hamaki. “Mbona una kisirani mzee wewe. Unampigia Mbalu kwa nini? Ondoka hapa! Huu ushemeji wako na mkubwa unakutia kiburi naona. Alafu kujia cheti chako na cha hao vipanya wako kesho. Askari walimfungulia Kalatu akatoka korokoroni. Alikuwa karibu atapike kutokana na uvundo wa kinyesi na mkojo ulitoka kwenye choo kilichokuwa wazi. Aidha, kutokana na msongomano wa watu pale harufu ya jasho na midomo ilikuwa nyingi. Kalatu alishangaa kama vituo vya polisi si mahali pa umma panapostahili usafi na ukaguzi wa huyu Mwenge.

Hakuwa na wakati wa kujibizana na askari waliomrushia cheche za matusi.

Dharura alikuwa pale kwake alipomwona Mzee Kalatu na kuchangamka. "Haiya! Ni wewe au mzuka wako. Je, umempa pesa? Ngapi?'' Aliuliza kwa hamu. ''Hata! Nilimpigia Mbalu simu akamwambia aniachilie bila chochote." Kalatu alimwambia. "Shukuru Mola una shemeji. Ningeshikwa mimi ningeozea ndani.'' Dharura alidakia. "Si Chui ni mzee wa mji wetu wa Tunu?'' Kalatu akamtania. "Chui huyu ni chui mwenyewe. Huoni alivyonitimua kutoka kwake ati tunakula sana na kuleta msongamano chooni. Na unafikiria ni kula ama ni kule kumkataa rafiki yake Kabondi aliyekuwa tayari ashaanza kula vyake." Dharura alieleza. ''Kweli ungekuwa mke wa sita!'' Kalatu alicheka. ''Nani? Kwani bwana ni pumzi eti nitakufa bila. Masaibu ya Mbaara yalinifika hapa…Acha nile taabu bila kulalamika. Nikipata nashukuru nikikosa pia nashukuru. Bora nisikose amani.

Kalatu alipofika nyumbani kulikuwa na kidogo cha kufurahia. Tendi mkewe alikuwa pale akilia, alikuwa amepokea simu kutoka Chuo Kikuu ambako Karani mwanao kifunguamimba alisomea kuwa hakuwa na hali. Alijaribu kujiua kwa kujirusha kutoka ghorofa ya tatu ya bweni Chuoni Njeru.

Hii ni baada ya kupoteza pesa zote alizopewa kulipia karo katika kamari ya *Betpesa*. Nabii wa soka kama lilivyokuwa jina lake pale shuleni, alibashiri mechi kati ya Algeria na Senegali waliokuwa fainali za *AFCON*. Kutokana na tajiriba yake ya ubashiri alikuwa na hakika kama mauti kuwa Senegali ingenyakua ushindi. Algeria ilikuwa imewekewa ubashiri wa *7.53* nayo Senegali ikipewa *2.09*. Bila kupigwa na mshipa akachuka simu yake na kuhamishia elfu thelathini na tano katika akaunti yake ya *Betpesa*. Pesa zile zote aliziwekeza kwenye ubashiri ule akitarajia kima cha shilingi elfu sabini na tatu mia moja na hamsini! Angekuwa tajiri. Sifa zake zingepanda mara dufu.

Kweli jina nzuri ni taa gizani hung'aa. Ilikuwa si kitambo alipochaguliwa rais wa chama cha wanafunzi pale chuoni. Wazazi wake walipofikiwa na habari hizi walifurahia ghaya na kujiona waliomzaa kiongozi wa kupigiwa mfano. Heshima yake ilipanda hata kwa wahadhiri wake. Naibu chansela angemwita mara kwa mara kujadili hili na lile kuhusiana na maswala ya wanafunzi ili kuzuia migomo ambayo ilikuwa ikisambaratisha na kulemaza masomo katika shule na vyuo nchini wakati ule. Wangepigwa picha ambazo kijana huyu angetuma mitandaoni mbalimbali ya kijamii ikiwa na maelezo mafupi. "*Vice chancellor and I*

*had a fruitful meeting today at his office on matters students wellbeing.''* Mitandaoni alikuwa na wafuasi wengi ajabu. Huku kulikuwa kule kunawa mikono ili kula na wazee kweli. "Nikimaliza shule nataka nimwonyeshe Mbalu uongozi ni nini.'' angejiambia nafsini mwake. Kauli yake chuoni ilifuatwa kama injili. Sifa hizi na zile za masomoni zilimpa kibarua kigumu kwa idadi kubwa ya wasichana waliotaka kuhusishwa naye. Angestaajabia wengine wakipigana juu yake bila ya yeye kuwafahamu vyema.

Sasa dimba la fainali likaanza. Senegali iliutwaa umiliki wa asilimia tisini wa mpira katika kipindi cha kwanza. Kipindi cha kwanza kilikaribia kuisha hakuna aliyeliona lango la mwenzake. Karani alikuwa pale tabasamu imemvaa usoni akipiga funda la maji polepole. "Muda tu kidogo nitaifilisi betpesa kama juma lililopita…watajua hawajui!'' Alijiambia huku akianza kupanga atakavyozitumia zile pesa ambazo tayari alikuwa ameziona kibindoni. "Mara hii nataka nimpeleke mrembo wangu pwani tena akaogelee ahisi ana mpenzi. Baada ya ziara hii yule kiroboto anayemzungukazunguka atatia akili kabla sijamharibu ile sura yake kama ya nyani mgonjwa; mbaya kuliko dhambi na ya kutisha zaidi ya jinamizi. Kutoka kwa elfu thelathini alizoshinda wiki jana hakuwa na hata senti mfukoni. Alimstarehesha nyongo wake mkalia ini zikaisha. Hii ni baada ya kumpeleka Diani *beach kupata* raha ya wakuu. Asichokijua ni kuwa mapenzi ya chuoni yalikuwa mapenzi ukungu. Mapezi ya pesa. Mifuko inapotoboka ile kadarasi ya mapenzi na mahaba hufikia kikomo na ikakuachia kovu la moyoni.

Hakuwa anasikia hata kelele cha mashabiki wenzake waliokuwa kama kusanyiko kubwa la wendawazimu. Hali hii ilikuwa kila mahali wakati ule; katika vilabu, hotelini na hata maboma ya watu. Kweli wazimu wakisoka ulikipanda kizazi cha kiume siku hizi! Wakati wa mechi kubwa kama hii asilimia kubwa ya wanaume wa makamo na vijana walikuwa viwamboni. Kama Karani, baadhi ya hawa pia walingojea vinono. Kuna waliokopa hata madeni waliyotarajia kulipa baada ya 'bet kuiva' kama walivyouita ushindi.

Kipindi cha kwanza kilifika kikomo na wachezaji kuenda kwa mapumziko na nasaha. Vijana walisikika wakitaniana "Leo tutawatandika msahau majina yenu…! Kutakufa mtu leo…! Mtasaga meno hasa…!'' Ubabe ulishamiri pale hata pale kipenga cha kuashiria kipindi cha pili kilipopulizwa. Wote walipiga makofi kuwakaribisha wachezaji uwanjani tena. Timu zilikuwa zimewabadilisha wachezaji, wakaja wapya kurudufu nishati ugani.

Wakati huu Karani alikuwa mmoja wa waliosikika zaidi. Huu ulikuwa ulingo wake. Algeria iliimarika kwa kiasi japo pia Senegali walijenga ulinzi mkali wa *4-4-3*. Kule dakika ya themanini na tatu, mchezaji maruufu wa Algeria alichezewa visivyo kwenye lango la wapinzani wake. "*Penalt! Penalt*!'' Wanaalgeria walisimama kwa furaha. "Penalt!'' Neno hili lilimfikia Karani kama pigo la rungu ya kimasai akilini mwake. Alijua hatari iliyobisha hodi. Kila mwasenegali alijiinamia roho mkononi. Mshambulizi maarufu Baghdad aliipiga ile penalti. Alfred mlindalango wa Senegali alienda kushoto mpira nao ukaingilia kulia.*''Goooal! Goaaal!''*

Vifijo vilihinikiza ukumbini mle. Hata waliokuwa wamelala waliamshwa na kelele ambacho kingewafufua wafu. Ungemwona Karani uso ulivyojaa makunyazi kama ya nyati. Macho nayo kayatoa pima kama panya aliyenaswa mtegoni. Kijasho chembamba kikaanza kumteremka kando ya masikio na kushukia mashavuni. Makwapa na mgongo vikageuka vijito vidogo.

Mpira ulikwisha. Algeria kifua mbele; moja mtungi. Algeria wakatwaa kikombe.

Karani macho yalianza kumsaliti. Aliona vitu viwiliviwili, mpaka mlango wa kutokea. Akajaribu kuamka, akajihisi kama anayeelea angani. Alishtukia akiwa katika zahanati ya chuoni akipewa huduma ya kwanza. Baada ya ukaguzi wa kina muuguzi akamruhusu kuondoka. Pale nje ya zahanati kulikuwa na umati wa wanafunzi uliomgojea kiongozi wao. Alipotoka alishangiliwa kwa kelele na makofi ya dhati na ya uzandiki. Alihepeshwahepeshwa na rafiki yake Mwangi hadi chumbani mwake kuepuka umati uliokuwa sasa bila shaka umemtia mdomoni. Mmoja alisikika akisema, "Wazazi wana shida ati, wanazaa nakusomesha burukenge kwa sura ya mtoto. Ni vipi unaweza kubashiri na kiasi hicho cha pesa? Upuuzi!'' Wengine walicheka wengine wakamkemea.

Mwendo wa saa saba usiku kulisikika kishindo katika sehemu ya chini ya bweni la Kena, kishindo kama kitu kilichoanguka. Haukupita muda kabla ya wanafunzi kuchomoka nje kama risasi huku wamevalia mavazi ya ajabuajabu. Wengi walitoka kama wanaspoti lakini walioshangaza zaidi ni wale waliotoka kama wachawi. Kusudi likiwa kuokoa maisha yao. King'ora cha hali ya hatari kililia. Nyakati zile kundi la sinautu lilikuwa tisho kuu nchini, hivyo jambo lililowajia wanafunzi akilini ni kuwa walikuwa wameshambuliwa. Lo! Waliofika chini kwanza walistaajabu kumwona Karani akimwaga damu kichwani. Alikimbizwa hospitali kuu ya Kalawa magharibi kwa ambulensi. Moja kwa moja

mpaka sadaruki. Madaktari walimshughulikia. Keshoye mwendo wa saa kumi na mbili asubuhi alifungua macho lakini hangeongea kwa kuchanganyikiwa. Mara hii naibu wa chansela alikuwa kando yake si kama mkuu wa chuo ila kama rafiki wa kijana huyu. Habari za kisanga hiki cha Karani zilimshangaza sana kwani alimjua kuwa kijana mwenye uwezo mkubwa wa kukabiliana na mazito. Akajituma kuja kuangalia mwenyewe kilichomfanya simba kula nyasi. Chansela alikuwa mfupi mnene ajabu aliyebeba nyama ovyoovyo. Alipotembea ni kama aliyebingiria; alikuwa mduara wa mtu hasa. Umbile la mkuu huyu lilisawiri kabisa cheo na hadhi iliyotarajiwa kwa kiongozi yeyote mwafrika. Hapo chansela akanyanyua simu na kumpigia baba mtu, simu ikawa haipokelewi.

Kalatu alizipokea habari hizi kwa moyo wa chuma. Hakutaka kumwonyesha mkewe hofu iliyomtamalaki moyoni. Dharura alipofika asubuhi siku iliyofuata alikuta hali ile. Alilia sana. Alimpenda sana mtoto huyu kwa bidii zake. Daima karani alimchukulia Nafuu mwanawe kama mnuna wake. Hangekosa zawadi ndogondogo kwake alipotoka chuoni. Akakumbuka vile kijana huyu alivyojitolea kumsaidia kujenga kile kibanda alichoishi sasa akatoka migombani.

“Msijali Mungu atamponya.’’ Aliwafariji Kalatu na Tendi waliotokwa na nguvu. Akawakusanya watu waliofika pale kwa Kalatu kujua hali ya mambo akiwemo Mbalu kwa dua. Wakapanga kutembelea kijana huyu hospitalini. Walipomwomba Mbalu kuwapeleka kwa gari lake. Alidai kuwa gari halikuwa na mafuta. Isitoshe, alikuwa pia na mkukato na viongozi fulani si kitambo kutoka wakati ule. Baada ya kuleta akili pamoja walikodi magari mawili madogo aina ya *Probox.*

Fahamu zilikuwa zimemrejea Karani, akayakumbuka mambo, akagubikwa na majuto na aibu kubwa. Alijiona kama mtu aliyemkosea kila mtu. Kwanza wazazi wake waliojitolea kwa vyovyote kumsomesha. Aliwakosea wanafunzi aliowaongoza kwa kutokuwa kielelezo chema. Aliwakosea wanatunu wote waliomwona kama mwokozi wao dhidi ya hila za mjomba wake. Alijikosea mwenyewe kwa kutaka kujitoa uhai. Alihofu watakavyomchukulia wazazi wake ambao tangu hapo alijua walikuwa njiani. Maumivu yalikuwa mengi. Alikuwa na plasta shingoni na bendeji kichwani. Mguu wa kushoto pia ulikuwa umevunjika. Kwa bahati nzuri uti wa mgongo ulikuwa imara. Licha ya haya majeraha yote alijikaza kisabuni ila maumivu ya akilini hayangevumilika. Akatoa kilio pale kitandani, kamasi na machozi vikapigana busu tayani.

Wazazi wake Dharura na majirani wengine walifika pale hospotalini. Nguvu zilizosalia zikamwisha kijana huyu. Akapasa sauti, "Mnisamehe wazazi wangu…nimewaumbua. Sistahili kabisa kuhusishwa nanyi". "Ah! acha hayo mwanangu." Kalatu alimwambia Karani. "Cha muhimu ni kuwa uko hai. Nashukuru Mungu kwa hilo." "Ndio Karani, cha msingi ni upate nafuu urudie masomo yako," Mamaye alisema. Dharura alijipa shughuli nje alipoona machozi yakikosa adabu na baadaye akajiunga nao.

Mbalu Mbunge wa Tunu aliketi katika hoteli ya Mzalendo. Mezani kulikuwa na sahani yenye mayai mawili na Soseji. Nyingine ina matunda mbalimbali yaliyokatwakatwa vipande vidogovidogo. Mkononi alishika glasi ya maziwa huku akitumbulia gazeti macho.

"Mheshimiwa hujambo?''Akatoa macho gazetini kumwangalia Mwenge. "Ah! Sijambo *officer."* "Karibu *breakfast.*" Mheshimiwa Mbalu alimkaribisha rafiki yake mkuu. ''Sasa naona kwa nini wewe ungali barobaro". Mwenge alimtania. ''Nawe huachi utani hata asubuhi. Unaonaje?'' Mbalu alidakia. ''*You are growing younger men.*'' Wote walicheka. "Unajua mimi ni kiongozi, mpaka niongoze katika kula chakula bora. Nahitaji Wanatunu wenye afya si wanyongewanyonge.'' Mhudumu alikuja kuchukua oda ya Mwenge. ''*This is on my bill doc."* Mheshimiwa alisema. ''Asante. Mmmh…nasikia nini kuhusu binamu yako Karani?'' "Achana na huyo mjinga *alibet* na *fee bet* ikamchoma." Mbalu alisema kwa kicheko cha dharau. ''Alafu?'' Mwenge aliuliza. "Akajaribu kujitoa uhai kwa kujirusha kutoka ghorofa ya tatu ya bweni chuoni. Sasa yuko hospitalini *in a vegetative condition.* Kupona kwake labda mwujiza."

Mheshimiwa huyu alisema kwa kiburi cha haja. ''S*oo insensitive of you*. Unaongeaje kuhusu mtoto wa dada yako?'' Mwenge alishangaa sana. ''Aah! Acha hayo, wewe bado umefungwa kwa kamba za familia na ujamaa! Alikuwa anaringa na hicho cheo chake chuoni. Sasa mwone. Hawa ni wale vijana wanatoka shuleni na kujidai kushindana na wazee wao. Uongozi haujaumbiwa kila mtu." Mbalu alisema kwa sauti iliyoashiria kuridhikika. ''Mheshimiwa anaogopa upinzani wa binamuye.'' Mwenge alisema huku akinyanyua kikombe cha maziwa kukielekeza mdomoni. "Nani aogope Kiroboto? Burukenge mlevi akiwa wapi? Nasikia yuko safarini kukutana na Abrahamu." Mbalu alisema kwa raha ya aina yake. ''Nilidhani ulivyomtetea baba yake ni kwa sababu ya uzito wa damu?''

"La, uzito wa akili! Ni mikakati ya uongozi. *Have you read the 48 laws of power? That's my creed.''* Mheshimiwa alidakia kwa kiburi. *"*Naona sasa nyinyi viongozi akili siku moja itawaua. Mnapuliza mnauma.'' Mwenge alimwambia rafikiye. Mbalu alisema kwa kiburi kilichomwudhi kidogo msena wake. ''Walitaka niwapeleke kumwona. Mimi nami ni nani? Nikacheza kama mimi. Siwezi kuwabeba watu kama

kina Dharura kwa *Range Rover* yangu. Utajuaje kama hawatakuachia mbegu ya chawa, viroboto au kunguni? Halafu tena nani ana gharama ya kuosha gari ili kuondoa kutuzi la hawa wanakijiji wachafu kama nguruwe wanaowafuga?''

"Mradi wetu unaendeleaje?'' Mbalu alisaili akibadilisha mkondo wa maongezi. "Kila kitu kiko shwari. Nimehakikisha huna mpinzani, Malele ashafunga kazi. Mji mzima ni wako sasa. Kichinjio kitakuuzia nyama karibu yote. Oda za shule na magereza sasa zitakuangukia. Jukumu ni lako sasa la kufungua matawi ya buchari yako kila mtaa. ''Ulimfanyaje?'' Mbalu alitaka kujua.'' Hilo dogo. Nyama yake ilipata kasoro. Leseni yake ikaharamishwa. Mwenge alieleza kwa mnogono. ''Ile kemikali ya kuhifadhi nyama bado iko?'' Mbalu aliuliza. ''Nimewapa vijana wako juzi ikabaki kidogo hata hivyo, haina neno, tutatafuta nyingine tu. Kama nilivyokuambia, ukitumia dawa hii nyama yako inabaki freshi kwa siku kadhaa." "Na madhara yake kwa watu?'' Mbalu alitaka kujua. ''Ah! Mkubwa, unafaa uchague kama unataka watu au pesa! Mwenge alimkazia macho rafiki yake. ''Nachagua pesa lakini pia kura zinaweza kufa.'' Alitania Mbalu. ''Watu wetu wanazaana kama mchwa hawawezi kuisha; hata kwa bomu la kinyuklia!'' Mwenge alisema na wote wakacheka.

''Kweli ndugu ni kufaana. Nyege nayo kunyegezana. Nawe mheshimiwa kumbuka ahadi yako. Natarajia kuwa waziri wa afya wa jimbo hili karibuni," Mwenge alimkumbusha. ''Jambo ndogo sana kwangu hilo.'' Mheshimiwa alimhakikishia Mwenge.

***

Nafuu alionekana mchangafu siku hizi. Afya na mavazi yake pia ni ishara tosha ya mabadiliko katika mapato ya mamaye. Shuleni hakosi tena kwa sababu ya hiki au kile. Aliutia wembe wake makali masomoni na kama wasemavyo kinolewacho bila shaka hupata. Hili lilimtia matumaini sana mama yake aliyeinua genge la Kalatu kuwa miongoni mwa mikahawa bora pale Tunu. Alimshauri Kalatu kubadilisha jina la mkahawa huo kuwa Tumaini *Hotel*. Wateja pale hawakuisha, upishi wake bora ulifanya mwujiza huu. Lugha yake nzuri ya ucheshi iliwafanya wateja kujihisi nyumbani. Si wengi wa wafanyakazi wa hoteli wangekubali kupika na kupakua chakula bila kulalamika kama alivyofanya mwanamke huyu. Kutoka Mwenge aache kumsumbua Kalatu, mambo pale yalikuwa shwari.

Kalatu aliweza kumlipia Karani karo aliyopunja kwa kamari na sasa hadaiwi. Naye Karani akija nyumbani angemuauni pale hotelini. Alimshauri baba yake jinsi ya kuweka rekodi za mauzo na gharama zote hili kuweza kukadiria faida au hasara.

Nafuu alipotoka shuleni angepita pale kazini kwa mama. Akala chajio na Kalatu kumwekea andazi za kufungua kinywa siku iliyofuata mfukoni. Dharura siku hizi anajiweka kama mwanamke wa umri wake. Mavazi yake japo ya bei nafuu daima yalichukuana vyema na umbo lake la kilaika, mapambo na viatu vyake. Mwili wake wa wastani, sura yake jamala isiyokauka na macho yake maangavu yaliyojaa nuru ya ujana vilimzubaisha kila aliyetazamana naye. Ngozi yake laini kama ya mtoto na ya rangi ya maji ya kunde vilifanya aonekane kabisa asiyekusudiwa kuwa mwanadamu bali malaika. Kuwepo kwa mwanamke kama huyu duniani ni ile hitilafu takatifu ya kimaumbile ambayo hutendeka mara mojamoja baada ya karne nyingi. Wapo wanaume waliofika pale Tumaini kando na kununua chakula, kutanabahi urembo wa kiumbe huyu.

Kasoro aliyokuwa nayo ni moja tu; umaskini. Ana miaka ishirini na saba sasa. Licha ya umaskini, Dharura alikuwa mwenye juhudi kuu. Kwa pato lake dogo, alijijengea nyumba ya wastani yenye vyumba vitatu. Aliipamba alivyoweza ikapendeza. Mama huyu pia kutokana na kutangamana na watu wengi pale kazini, amekomaa kijamii na kisiasa. Alivyozichambua siasa za eneobunge la Tunu, jimbo na hata nchi nzima ziliwaduwaza wengi. Kutoka kwa mama mdogo asiye na kisomo cha haja, hadi mchambuzi wa maswala mazito ya kijamii na kisiasa ni sawia na kuzaliwa kwa mara ya pili kwake. Alijihisi huru huria akajiona bora na kujiheshimu. Aliyekuwa mumewe sasa alikufa kifo cha ndani kwa ndani. Watu walimsuta alivyopoteza bahati ya maisha. Mara kwa mara angefika pale hotelini kuhakiki fununu alizosikia. Akala akaenda zake. Alipojaribu kutia mengi kando na biashara alikutana na mwamba. Dharura hakuwa tayari kurudi jela. Isitoshe, tabia ya Mbaara ilikuwa ile ile tu. Alikuwa amevishiba vituko vyake. Alichoka kuonekana duni maishani. Kuoleka kwake katika umri wa miaka kumi na minane tu kunaweza kuwa kulikuwa chaguo la pekee wakati huo. Hii ni kutokana hali ya umaskini walioishi nao na bibi yake. Kupata cha kutia mdomoni kulikuwa karibu mwujiza. Hii ni baada ya ami zake kuliparamia shamba lao mara tu baada ya kifo chake na mama. Ami zake wawili walihamisha mipaka ya mashamba yao kulibana lile la akina Dharura lililokuwa katikati ya yao na kuliacha likiwa kama ujia wa kwenda msala. Bibi alipowaonya dhidi ya tendo hili alikemewa kwa kuambiwa kuwa mwanamke hakuwa na haki

ya kuzungumzia mashamba. Isitoshe, hakuwa na shamba lolote. Shamba lilikuwa la baba yao! Katika jamii yao urithi ulikuwa wa mwanamume. Lililowatia hari zaidi ya kunyanyakua shamba la marehemu ndugu yao ni kuwa hakuwa na mtoto wa kiume. Kwa hivyo, hata kuacha kikataa walimozikwa wazazi wa Dharura na ambamo yeye Dharura alikuja kuishi baada ya kufarakana kwa ndoa yake, ilikuwa zao la huruma isiyomithilika. Bibi alipatwa na kihoro. Alihofia kuangamia kwa kizazi cha mwanawe aliyempenda zaidi.

Ingawa alikuwa maskini kati ya wanawe watatu alikuwa mwingi wa ukarimu na utu. Alimfaa mama yake kwa kila hali wakati wengine walimpuuza na kumdharau. Chui alikataa kabisa kuwasitiri na kuwalea kina Dharura baada ya kifo cha wazazi wao. Hili ndilo lililomfanya bibi atoke kwake. Siku ambayo Chege aliuawa na umati pamoja na mkewe, ilimpa donda sugu la moyoni lililotoka damu kila uchao. Alijifunga kibwebwe kuwalisha wajukuu wake wawili japo kwa shida kutokana na umri wake mpevu. Ulifika wakati hata hivyo akalemewa kwa ugonjwa wa macho uliompofusha. Hapo ndipo Kanini aliona ku moto na kutoroka akaadama mahaba. Dharura akazurura popote akisaka vibarua ili kumlisha na kugharimia gharama za matibabu ya bibi yake. Alipopata alifurahi, alipokosa alirudi mabega yamemshuka. Katika hali ile bibi angemwita karibu akaishika mikono yake na kuitemea mate akamwambia. "Mjukuu wangu kukosa na kupata vimefana kwa namna fulani. Ukikosa leo kumbuka ulichopata jana na ushukuru. Ukipata kumbuka kuna kukosa ushukuru pia. Siku moja utajaza maghala mwanangu.'' Maneno haya yangemtia moyo zaidi Dharura.

Siku moja alikuwa ametoka kibarua yapata kilomita tano kutoka kwao. Alimkuta kijana mmoja mtaroni kando ya barabara amelewa chopi. Alikuwa akisonya na kuguna. Alipojaribu kuinuka alianguka na kuzidi kujisiriba matope. Dharura alishangaa ni vipi kijana mdogo kiasi kile alivyoamua kuyaharibu maisha yake kwa konyagi. Alimhurumia sana. "Kaka yangu mbona unajiharibia maisha kwa kileo hivi. Ona ulivyomshida nguruwe katika mchezo wake!'' Alimuuliza yule kijana kwa sikitiko. "Maisha? Ulisema maisha? Mimi nina maisha gani? Maisha niliyaua kwa viganja hivi." Mbaara alisema huku akinua viganja vichafu ajabu. "Nahitaji kileo, la sivyo majuto yatanilipua akili." Dharura alizidi kushangaa ni lipi hilo jamaa huyu alilojutia. Akamshika mkono akamtoa mtaroni alikokwama.

"Nashukuru sana dada yangu. Wengi wamenipita hapa kwa kicheko, wewe umenifaa. Una moyo wa dhahabu rafiki.''

Hivyo ndivyo mtu na mumewe walivyokutana. Asubuhi ya siku moja Dharura alipokuwa shughulini, alikutana na Mbaara kama hajalewa. Hapo ndipo alipopewa aliyotaka na asiyotaka kusikia. Alishangaa jinsi Mbaara alivyoharibu bahati ya maisha kwa anasa na utashi wa ujana. Hata hivyo hakumhukumu. Naye akampa simulizi ya maisha yake. Kabla hajamaliza Mbaara alianza kulia. “Mbona walia kaka?” Dharura aliuliza. “Simulizi yako inanihukumu. Nilijaliwa kila kitu maishani nikakiharibu. Wewe ukajaliwa kidogo ukakihifadhi. Najutia nilivyomtelekeza mama yangu hadi akafa. Naomba jambo kwako. Uniruhusu nikusaidie kumwuguza bibi yako angalau nipate kupunguza adhabu inayoningoja jehanamu. Kwa hili huenda Qurdusi ataniruzuku.

Mbaara na Dharura walianza kuonekana pamoja wakisaka vibarua. Walichopata walinunulia bibi chakula na dawa. Kwa kiasi Mbaara aliweza kudhibiti ulevi. Bibi siku moja jioni aliwaita wawili hawa akawaambia. “Wanangu, majaliwa yamewaleta pamoja. Ishini pamoja. Muda wangu sasa umefika wa kupumzika. Ishini kwa kuelewana. Siku chache baadaye bibi aliaga. Wakamzika kwa majonzi. Wakabaki wawili; mume na mkewe.

***

Ni mwaka wa nne sasa tangu Karani alipojiunga na Chuo Kikuu cha Njeru kusomea shahada ya Uanahabari. Alikuwa wakati huu katika harakati za kujiandaa kwa mtihani wake wa mwisho. Tangu alipoponea kifo kwa tundu la sindano amekuwa mtu tofauti. Alikuwa katika mstari wa mbele kuwarai wanafunzi na vijana wenzake wajihadhari na kamari huku akijitumia kama mfano bila aya.

Pale aliporudi chuoni kutoka hospitalini, alikuwa ameamua kujiuzulu kutoka kwa wadhifa wake kama rais wa Chama cha Wanafunzi jambo lililokutana na upinzani mkali kutoka kila pande wa wahadhiri na wanafunzi. Kwa msaada wa mhadhiri mmoja wa Sayansi ya Siasa aliweza kujua jinsi ya kutumia hali ile kuibuka tena. Akashika nasaha ile kwa mikono miwili. Wiki iliyofuata aliwaita viongozi wengine wote kwa kikao na kuwaomba ushirikiano wao. Naibu wake hata hivyo, hakufurahishwa na jambo lile la Karani kuendelea kudumu kama mwenyekiti. Hata hivyo, wengi wape. Uungwaji mkono wake ulikuwa mkubwa.

Kando na hayo, Karani alikuwa na jambo lililomtia wasiwasi. Baada ya shule angeenda wapi. Moyoni alitaka akae pale Tunu awasaidie

watu wake. Alihisi msukumo mkali wa huduma kwa jamii. Na taaluma yake ya uanahabari je? Hangesita kujiuliza. Hii ni kinyume na vijana wengi wa hirimu yake waliokimbilia mijini. Kwake yeye mji mkuu ulikuwa Wanatunu japo alihofu kutopata kazi pale. Ami yake Mbalu alizidi kuwanyanyasa watu wake jambo ambalo lilimsumbua. Dan mwanawe Mbalu na mwandani mkubwa wa Karani alimfichulia mengi mabaya kumhusu babaye. Alimweleza vile alivyoona haya kuwa na mzazi kama yeye. Ndiye aliyemwambia Karani kuhusu kemikali hatari iliyohifadhi nyama katika buchari za baba yake. Karani naye akamwonya baba yake dhidi ya kununua nyama kwake bila kumwambia sababu. Mwenda mwanawe Mwenge pia alikuwa mwanachuo wa Karani.Japo si mwingi wa maneno alimpasha Karani kwamba achunge sana kwani simba jike alimsubiri sana pale nje kumrarua. Aliyasikia haya kwa babaye akimnongonezea Sara mamaye vile Mbalu alimwogopa binamu yake kisiasa na kwamba angeweza hata kumdhuru. Hayo yote Karani aliyatia moyoni kama siri asimwambie mtu.

Mwaka ule alipomaliza chuo Karani, Nafuu alijiunga na shule ya sekondari ya Kalawa iliyokuwa kilomita tatu hivi kusini mwa Tunu. Kalawa ilikuwa shule ya kutwa maarufu kielimu na kimichezo. Nafuu alikuwa na matumaini makubwa ya maisha. Msichana huyu anakumbuka alivyotaka kuwa daktari mwalimu sasa akajicheka. Sasa alishafanya uamuzi wa kitaaluma. Alitaka awe mwalimu wa sekondari. Japo kazi ya ualimu haikuwa na pesa, alihisi kwamba alihitaji ile kazi ambayo ingemtangamanisha na vijana wengi. Pia alihisi kuwa ualimu ulikuwa uzi ulioziunga shughuli zote zilizohusu jamii. Alitamani kuihudumia jamii moja kwa moja.

Japo waliachana kiasi kwa umri, Karani na Nafuu walikuwa na mengi yaliyowaweka pamoja. Dharura alifurahia urafiki huu kisirisiri kama mzazi. Alifikiria na kutamani jambo fulani kuhusu wawili hawa.

Baada ya mtihani wa mwisho wa muhula wa kwanza, Nafuu aliibuka kideda kwa alama ya A. Akabeba zawadi nyumbani. Mama alifurahi. Kalatu akafurahi, si kwambii Karani.

***

Usilolijua kweli ni usiku wa giza. Muda huu wote Dharura alikuwa akifanya kazi pale hotelini, Tendi mkewe Kalatu hakufurahia. Aliona hatari kwa ndoa yake. Maendeleo ya mwanamke huyu, pamoja na ule urembo wake vilimtia Tendi kubuhuti. Alimwangalia Dharura akaona

mwewe anayenyatia vifaranga wa kuku asiye na habari. ‘Niko macho sana!’ alijiambia nafsini. ‘‘Vipi anavyomudu mavazi na vipondozi vyote hivi na mshahara wake mdogo? Anajiweka kuliko mimi mke wa tajiri wake. Huenda anaiba ama analipwa zaidi ya ninavyojua.” Alizidi kuwaza.

Hakupenda urafiki wa Karani mwanawe na yule mtoto wa Dharura. ‘Atanipokonya bwana na mtoto pia mchawi huyu! Mpaka niuwahi udongo ulimaji. Siko tayari kwa upinzani mie.’ Mgogoro ulizidi mawazoni.

Siku moja Kalatu aliugua akawa hajiwezi. Ikawa na nafasi aula kwa Tendi aliyechukua nafasi yake pale kazini kutekeleza mpango wake. Dharura aliacha kipochi chake kwenye kaunta alipofanya shughuli zake na kukichukua jioni. Aidha, hangeingia pale bila ruhusa ya Kalatu. Ilikuwa hivyo kwa kila mfanyikazi pale. Ilipofika jioni aliitisha Tendi kipochi chake, akamwita Nafuu wakaanza safari ya nyumbani. Hakufika mbali kabla ya simu yake kukiriza. Tendi alimtaka arudi mara moja bila maelezo yoyote. 'Kumetendeka nini kurejeshwa kwa amri hivyo?' Alijiuliza huku akirudi pale kazini. 'Mke wa bosi ni bosi haidhuru.' Alikutana na macho ya Tendi yaliyotoka pima kama gololi. ‘‘Leo nimekupata peupe! Kumbe hivi ndivyo unavyofanya kila siku. Utanitambua leo hawara wewe!’’ ‘‘Ati nini? Wasemaje Tendi?’’ Dharura aliuliza huku pumzi za hasira na mshangao zikibanania kooni kulifanya liwe kavu kama jiwe la jangwani. ‘‘Acha hamnazo mwanamke. Huwezi kuvuna usikopanda.” Tendi alifoka akimkaribia Dharura amtie mikononi. Vurugu hizi zilimwamsha Kalatu aliyekuwa ndio ametoka hospitalini kupiga foleni kwa saa kadhaa na kujitupa kitandani. Karani na Nafuu pia walijitoma hotelini rabsha zilipokidhiri. Kulikuwa na wateja walioachwa vinywa achama wasijue waingilie wapi hata pale walipoona wawili hawa wamekaribiana. “Tendi!” Kalatu aliita kwa amri. ‘‘Nini kina mama mnasimamana kama majogoo mbele ya watoto?" "Si ni huyu mwizi hapa, nimeuza leo elfu saba mia saba. Ninachokiona hapa ni elfu nne mia saba. Tulikuwa wawili hapa kufikia wakati alipoondoka”. Kufikia hapo Karani hangekaa pale. Akamkonyezea Nafuu wakatoka nje. ‘‘Tendi chunga maneno unayotoa kwa Dharura kwani hata ushahindi huna." Kalatu aliomuonya mkewe. ‘‘Hivyo mimi ndio mwizi? Huwezi kuniamini mimi mkeo. Ebu mwambie alete hicho kipochi.’’ Dharura hakungoja kuambiwa. ‘‘Hiki hapa!’’ Tendi alikichukua na kufungua mfuko wa kando. ‘‘Nini hii? Kalatu nini hii? Nilikwambia huyu ni mwizi huniskii. Unamtetea tu kama…’’ “Kama nini Tendi!” Kalatu akamkata kauli. “Naona ghala lako la heshima ni tupu.”

Dharura akashindwa kuudhibiti mdomo wake, ukapanuka wote, macho nayo yakawa ya lumbwi, mkononi nako kashikilia kichwa kana kwamba kilimlemea kwa uzito. Nguvu zilimtoroka, kumbukumbu za maonevu ya Mbaara na Chui zikafanya lile kovu alilofunika kwa maneno mengi na vicheko siku zote kutoka damu "Jamani sijachukua pesa za mtu mie. Mwenyewe kanipa pochi hiyo.'' Alijitetea. Kalatu alikuwa ameelewa kuwa Tendi hakumpenda Dharura ila si kwa kiasi hicho. ''Dharura hajaiba kitu! Hawezi. Nimekuwa naye hapa kwa miaka yote hii sijapata kasoro naye.'' Mume wangu fungua macho. Hata mumunye huharibikia ukubwani. Hivi wewe unadhani mapeni unayompa yanamtosha kumlisha, kumrembesha na kusomeshea mtoto na pato jingine hana!'' ''Oh! Naelewa sasa. Ndio maana umeniwekea pesa kwa pochi yangu ili niitwe mwizi? Kukaa kwangu vizuri ni donda kwako?''Dharura alifoka kwa hasira ''Nani kakuwekea wewe…?''Tendi alijaribu kujitetea ''Ngojaa…mbona umeenda moja kwa moja kwa mfuko wa kando? Tena mimi ni mpumbavu vipi nitaiba pesa niziweke kwa pochi alafu nikuachie hapo? ''Sema hunitaki hapa kwako na sitabisha ila kunitusi na kuniharibia jina sitakuachia ati!''Alisema Dharura kwa hamaki. ''Sitaki kukuona hapa nimesema!'' Tendi alifoka kwa msisimko.

"Nyamazeni!''Kalatu alikuja juu akielewa sasa mbivu na mbichi.'' Mimi sitaki kisirani kwa biashara yangu. Hivi hamwoni mnahujumu kazi. Ona wateja wanavyowashangaa. Riziki yangu iko hapa na sitaki wa kuichezea. Haya, leta hizo pesa, na pochi pia. "Dharura, naomba msamaha kwa zogo hili. Nichukulie. Hujaniibia chochote mimi. Hizi zimetoka kwa pochi ni za kwako, shika na uende nyumbani. Kazi nayo sijakufuta mimi." Kalatu alisema huku akitoka na kuelekea chumbani. Dharura naye akakanyaga hatua kubwa kubwa zenye vishindo akalenga lango la kutokea huku akimwita Nafuu kwa sauti wakielekea kiamboni. Karani akawasindikisha mpaka kwao kimyakimya. ''Mama nitarudia hapa. Pole kwa yaliyotokea. Huo ni msimamo na maoni ya mama wala si yangu wala baba'' alisema Karani kwa sauti ya upole.'' Usijali mwanangu naelewa" Dharura alisema

Japo aliudhika sana, Dharura aliyapokea yote kwa moyo wa ujasiri kwani alijua bayana kuwa dunia haikuumbiwa wenye mioyo ya mabua. Alijua siri moja; kutoweka maudhui. Alimsamehe Tendi, akamwona kama mwanamke yeyote aliyejaribu kulinda ngome yake. Aliapa kutorudi pale hotelini.

Pale nyumbani akajikalia asijue la kufanya. Mzigo wa mahitaji ya mwanawe ulikuwa barabara mabegani. Hakuwa tayari kuutua. Japo

alitahayari alijituliza. Hata kama upele hupewa msi kucha alikuwa tayari kuzitafuta zake.

Keshoye Kalatu aliamua kurudi kazini japo kwa maumivu ili kuliokoa dau lililotishiwa na mawimbi. Alimngoja Dharura asimwone. Alipompigia alimwambia kwake amekushiba na hangerejea huko. Alikuwa amemjua mfanyikazi huyu, kwamba akiamua jambo ni vigumu kumbadilisha. Ni kutokana na hili Tumaini ilikuwa miongoni mwa hoteli bora katika mtaa ule. Wafanyakazi wengine walihudumu chini ya maelekezi yake na bila yeye walikuwa toroli tu. Kwa hasira alitoka hotelini na kurudi nyumbani akamfokea mkewe vya kutosha. “Sasa ulimfukuza Dharura nataka uifanye kazi aliyokuwa akiifanya nikulipe. Unaanza leo… sasa hivi! Twende!’’ Sauti ile ilikuwa ngeni masikioni mwa watoto wa mzee huyu. Mama akajua si wakati wa ubishi, alinyanyuka akajitandata leso na kumfuata.

Kama kawaida wateja walimiminika pale Tumaini kwa tumaini la kupata kiamshakinywa. Wengi wa hawa ni wale bado hawakuwa wamekisikia kioja cha jana. Chai haikuwa tayari. Wafanyakazi walikuwa katika mgomo baridi. Ndio sasa wanafinyanga kinyunya cha mahamri. Siku chache wateja waliyeyukia mbali. Tumaini ikakosa tumaini. Hata Karani kwa elimu yake hakuwa wa msaada. Mkewe mtu alimenyeka kwa kazi pale, mara amejichoma, mara chumvi nyingi chakulani, mara kimeungua huku. Akajuta sana.

Maji yalimzidi Tendi. Pesa zilikuwa shida pale nyumbani. Mumewe naye akageuka simba, mawazo nayo yakaanza kumzidia. ‘‘Mume wangu nataka tuongee.’’Alianza kwa woga. “Si unaongea? Sema usemacho nataka kulala". Kalatu alisema kwa hamaki. “Niliongozwa na wivu mume wangu, wivu wa mapenzi. Nilimshuku Dharura visivyo. Najutia kosa langu. Kazi aifanyayo kweli ni kubwa. Nisamehe mwenzio. Nipeleke kwake kesho nikamwombe radhi’’ ‘‘Sijamkosea mtu mimi, ulivyomkosea kamwombe msamaha.’’ Kalatu alisema kwa mkato na kulala.

Keshoye mapema Tendi alikuwa mlangoni pa Dharura. “Karibu Tendi." alimwambia mgeni wake. ‘‘Sijui nimefanya nini mara hii nikawa mwenyeji wako asubuhi hii mbichi.’’ Dharura aliuliza kwa dharau. ‘‘Naleta kheri wenzangu. Najutia kosa langu. Hukustahili niliyokutenda. Naomba msamaha." Tendi alijieleza kwa unyenyekevu.’’ ‘‘Hakuna neno Tendi. Japo sina mume najiheshimu sana. Tena mimi japo ni maskini bali sijawahi kuangalia kitu cha mtu kwa tamaa. Nashukuru Mungu kwa hilo. Mwenzangu uliniumbua si mbele ya wateja tu bali hata ya watoto wetu

Karani na Nafuu. Nafuu anakuheshimu Sana. Haidhuru, nimekusamehe dadangu."  Dharura alisema huku akifuta machozi kwa ncha ya kanga aliyojitanda. Pale akabadili msimamo wake wa kutorudi kazini.

Kalatu alipomwona siku iliyofuata, alichangamka kama kawaida yake. Matumaini ya Tumaini yalirejea.

***

Kanisa hili la kisasa limekuwa katika kila kinywa pale Tunu. Mwema, mhubiri mashuhuri sasa pia ana gari kubwa aina ya *Landcruiser V8.* Jumba lake la kifahari pembeni mwa uwanja huu wa kanisa halina mfano wake isipokuwa lile la Mbalu. Limeshehenezwa vitu vya dhamani kubwa. Jumapili kanisa hili hujaa na kuwatapika waumini wengine nje. Siku hizi hufanya ibada mara tatu kila Jumapili ili kupunguza msongamano wa waumini wenye kiu kuu ya neno pale. Kilichowavutia watu zaidi ni ile miujiza iliyofanyika hapa. Watu waliponywa magonjwa sugu. Wengine wakaombewa wakapata wachumba na watoto. Kuna wale walioponyewa biashara zao. Shuhuda nyingi zilitolewa hapo kila Jumapili watu wakamshangilia ‘Bwana’. Naye Mwema akasisimuliwa kuwaombea kondoo wake hata zaidi. Alisikika akiomba kwa sauti za kutisha, na akirukaruka na kuradarada huku na kule mkono wa kulia akiuinua juu mara kwa mara kumpa upako huyu na yule. Alipofanya vile umati ulishikwa na jazba. Aliposema ‘pokea!’ kwa sauti yake nzito umati ulimomonyoka. Wasaidizi katika huduma hii walishughulika kuwazuia waumini wasilaliane na kuumizana. Wengine wa walioanguka walisikika wakipiga kelele kisichoeleweka, naye mhubiri angefoka *“TOKA! MWACHILIE!”*

Sauti nyororo ya Dharura ingesikika ikiimba nyimbo za kuabudu wakati wa huduma kama hii. Alikuwa miongoni mwa waimbaji bora Mwema aliojivunia. Cha ajabu ni kuwa walioombewa ni watu wanaojulikana ila waliotoa shuhuda walikuwa wageni waliotoka mbali. Nabihi huyo angesafiri Ningeria au Ghana na kurudi na nguvu za ibada mara dufu. Kadhalika angerudi na maji ya baraka, leso, hanchifu, mikufu na pete za neema na kuuzia waumini.

Jumapili hii baada ya ibada, mtumishi wa Bwana akamwita Dharura kando. Hili halikuwa ngeni kwa kuwa kiumbe huyu ndiye aliyekuwa kiongozi wa waimbaji pale. Wakatembea polepole kuelekea kwa jumba la Pasta.Walizungumza hili na lile na kila baada ya maneno machache ingekuja ‘*Amen*’ au ‘*Haleluya*’. Pale sebuleni Dharura

akapakuliwa chai ya maziwa. Muda kiasi mambo yakageuka. Mwema akamsongea Dharura pale kochini alipokuwa amejibweteka. Akaona haya si yale ya amen na haleluya, akasonga mbali naye. Mwema akasongea tena. Nabihi akasimama akitabasamu kizandiki na kukiumauma kidomo cha chini kitundu macho yamemuiva. ‘‘Dharura, macho ya Nabihi yameona urembo wako. Mtumishi wa bwana anakupenda.’’ Mwema alisema akijaribu kumshika kiuno. Dharura akamzuia kwa nguvu. ‘‘Acha hayo mtumishi, nakuheshimu sana, tena sijawahi kufikiria uhusiano mwingine nawe isipokuwa ule wa kihuduma pale kanisani. Mimi ni mke wa mtu bado.’’ Dharura alisema kwa dalili zote za kuudhika. ‘‘Mtu gani? Yule kinyangarika mjalaana mchafu kama fuko. Mtu aliyeharibu mali ya wazazi kwa ulevi na anasa hakustahili kamwe. Tena mliachana naye kitambo." Mwema kwa kiasi aliudhika. “Nakuonya kuongea hivyo kuhusu baba ya mtoto wangu. Tena nikikualika katika swala la ndoa yangu utanipa ushauri. Kwa sasa koma kabisa. Ninavyojua sijapewa talaka na hata hivyo sina nafasi ya mwanaume mwengine." Dharura alihisi kudharauliwa na mtu huyu aliyemjua kama askari trafiki wa njia nyofu ya mbinguni. ‘‘Aah! Acha hizo mrembo, hivyo huna hisia za…’’ Mwema alimwuliza akimsongea. ‘‘Sina! Nasema sina hata chembe! Sasa naomba kuondoka nachelewa nyumbani.’’ Dharura alisema akipinduka na kuutazama mlango. Kabla hajaufikia Mwema akamrukia akamshika kwa nguvu naye dharura akapiga ukemi ambao ulimezwa na jumba lile usitoke nje. Machoni mwa Mwema alionyesha kulitekeleza azimio lake kwa vyovyote. Alipofanikiwa kuunasua mkono wa kulia, Dharura alimpiga sehemu fulani mwilini akamwachilia na kujikunja kwa maumivu naye akaukimbilia mlango.

Alifika nyumbani kuchelewa na mwenye hasira za mkizi jambo lililomshangaza Nafuu.

Usuli wa Mwema kwa kweli haukujulikana kwa kuwa hakuwa mwenyeji wa pale. Maneno mengi kuhusu Mwema yakawa hewa; yakasambaa na kusagaa kote. Ndimi nazo zikayasiaga na kuyafinyanga kuyapa umbo na sura mpya kabisa.

***

Tangu kazi yake iinuke tena Kalatu ni mzee mwenye furaha. Anafunga saa tatu unusu usiku siku hizi. Wafanyakazi wengine wakiondoka hubaki pale akipika chai na kwauzia vijana na wazee waliopenda kupitisha muda pale kwa maongezi au kutazama mpira runingani. Siku moja alisikia

vijana wakiongea jambo lililompiga mshipa. Hakuamini Mwema alikuwa mbaya kama alivyosawiriwa na mabarobaro wale. Tena na Dharura, la, haiwezekani kwani hakuona mabadiliko yoyote kwa huyu mfanyikazi wake. Keshoye Dharura alifika ofisini mwake kama ilivyokuwa kila wakati. Alijivunia kazi ile na kuwaambia vijana waliokusanyika pale kila jioni wajivunie kila walichokifanya. "Jivunie chako, cha mwenzio chakusaidiani? Kazi ni kazi bora kipato na amani. Si kila mbeba vitabu ni msomi. Ufanyavyo na kisomo chako ndio shughuli nzima. Ni wangapi wana shahada za biashara na si wanabiashara? Wangapi wenye shahada katika kilimo na hawalimi wala kujihusisha na kilimo chenyewe? Ni ujinga kufa njaa hali una nguvu. Ukipata ya kuchimba choo chimba, ukipata ya kulima lima. Muradi upate ganje! Hutapungukiwa na masomo yako. Mtu hula jasho lake si stakabadhi za elimu."

Alivyochangamka asubuhi hii Kalatu alikosa pa kuanzia. ''Baba Karani hujambo?''Alimsalimu mwajiri wake kwa bashasha za kawaida. ''Leo mbona hivi?'' Dharura alimsaili Kalatu. ''Naona mbuzi wako yu hai mpaka sasa. Ama umeokoka na kuasi mauaji ya vuimbe wa Mungu?" Wote walicheka.'' ''Si bado mapema? Karibuni atakuwa chunguni ni vile yule afisa wa kupima nyama amesema atakawia kidogo." Kalatu alisema akiendelea na kukitia kisu chake makali.

"Dharura nisamehe kwa kukuliza hili…mmh…ninayoyasikia yana mashiko au ni porojo za wanatunu tu?'' "Kuhusu nini vile?" aliuliza tayari amejua mkondo wa mazungumzo. ''Ya nabihi Mwema ni kweli?" akauliza Kalatu. "Ndugu yangu ni kweli. Hatuna Pasta pale. Amefanikisha ukondoo usoni ila ndani ni yule hayawani. Ole wetu sisi maskini tunaoamini hali tumefunga macho na vichwa kuinamisha, mikono nayo hewani kana kwamba tunasema 'tule fisi tule tumejikabidhi kwako'. Dharura alieleza mwenzake. "Inaonekana amekufika kooni." Kalatu alisema huku akicheka kidogo. "Kalatu muumini wa siku hizi yumo taabani awe wa dini gani. Wanaotuhubiria na watiwe katika mizani ya imani ya dini husika kabla ya kuwaaminisha nyoyo zetu kutuunganisha na Muumba. Wengi ni wanabiashara na makanisa nayo yamekuwa vioski. Wamechukua kutojua kwa watu kwa manufaa yao wenyewe. Tuyaache haya au yatalemaza kazi asubuhi hii," Dharura akasema. ''Ndio maana nilisema siendi kanisa la mtu. Nikae kwangu nimwombe mungu wangu hapo basi," Kalatu alisema. ''Hivyo navyo si vyema. Ushirika katika imani ni muhimu. Sote tu dhaifu. Tukiwa pamoja tuna nguvu ya sala." Dharura alisema kwa ukakamavu. "Aya sasa Nabihi Dharura nimekupata!" alisema Kalatu.

# Sura ya Nne

Jiji la Takuja liliyumbayumba na kila mwenyeji alikuwa mashakani. Kulisikika mlipuko mkubwa katika mojawapo ya hoteli kubwa pale. Mlipuko huu ulifuatwa na milio ya risasi kisha ukimya wa dakika chache ulitawala. Milipuko kadhaa iliyofunika mayowe ya waliokuwemo mle ilifuata. Haukupita muda kabla ya taarifa kwamba lilikuwa shamulizi la kigaidi na kuwa magaidi wa Sinautu walikuwa wanawatumia mateka wao kama ng'ao dhidi ya polisi.

Katika kadhia hizi wengi walipoteza maisha, wengi waliumia, mali ya kima kikubwa kisichojulikana ililiharibiwa.

Haikuwa imepita miaka mingi kabla ya lile shambulizi lililoshtua ulimwengu mzima. Hii ni pale wanamgambo wa Sinautu walipovamia Chuo Kikuu cha Mwangaza kule kaskazini mashiriki mwa nchi. Siku hii nyeusi katu haitafutika katika kumbukumbu zangu.

Mwendo wa saa kumi unusu alfajiri hivi chuo hiki kilivamiwa na wanafunzi zaidi ya mia moja sabini kuangamia. Malaika wasiokuwa na uhasama wala deni na yeyote waliporwa roho zao na maafriti wafyonza damu. Kitendo hiki kiliniuma, nikajawa na chuki, nikatamani nafasi ya kulipizia watoto hawa kisasi. Niwahujumu hayawani hawa mara dufu. Laiti la kuku lingempata mwewe. Hawa hawangeitwa watu wala wanyama. Ulisikia wapi simba wakiwaua swara mia na zaidi kwa kutwa moja? Simba wana utu ati! Wao huua kupata lishe si uraibu. Hawaui kwa starehe zao. Muulize mmoja wa hawa maafriti atakwambia kuwa anafuata matakwa ya dini fulani. Dini wanayoifuata yenyewe imewakataa na kuvilaani vitendo vyao mara si moja.

Nanjala, mamaye mmoja wa wanafunzi waliofariki hangeficha machungu yaliyojikita ndani ya moyo wake. Anakumbuka alivyomenyeka na kazi za sulubu kumkidhi mwanawe tangu mumewe aiage dunia katika ajali mbaya ya barabarani. Alivyolala njaa na kutembelea mararu muradi mwanawe asome aje kumfaa maishani. Mwone alivyovaa sononeko usoni. Hana mwana, hana mume. Kwake maisha yaligeuka shubiri. Dira yake ilikuwa huyu mwanawe Seku. Alikumbuka maneno ya mwisho ya marehemu mumewe pale hospitalini Takuja.

*''Mpenzi, muda wangu nawe ni wa kuhesabu. Kulingana na daktari hapa sitoki hai. Nahisi pia sina nguvu tena. Ila najua kitu kimoja. Nakupenda sana mke wangu. Nampenda pia Seku mwana wetu wa kipekee.*

*Hatukujaliwa watoto wengi lakini kwangu nahisi sina nakisi. Umenitia nguvu sana Nanjala. Sipendi kuwaacha lakini wa mungu haufutiki. Najua bila mimi maisha yatawawia magumu ila usikate tamaa. Seku atakuja kukusaidia siku moja. Msomeshe uwezavyo. Akiwa wa umri mweleze vile baba yake alivyompenda kwa dhati ya moyo wake. Usiache akate tamaa maishani.*
*La..la mwisho mke wangu. u…si...ridhiwe. Bado na...ku...pe… nda. Nitakupenda haa.ta ka. tika ma.u.. ti"*

Sasa Najala anajiona kama aliyeonewa, akaona kama maisha yanamwadhibu. Maisha yake ya shida na dhiki isiyomithilika yakapita akilini kama kanda ya video huku ametazama juu kana kwamba anamshtakia mungu akaanza kuimba:

*Mbali nilipoanzia, hadi hapa kufikia,*
*Mengi nimepitiaa, mitihani ya dunia,*
*Nikapata furahia, hata ikaja karaha,*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

*Ukiwa pamwe udhia, bezo na matusi pia,*
*Magumu yote pitia, yote nikavumilia,*
*Pakulia nililia, kwingine katulia,*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

*Maishangu ya awali, kawa kama haluaa,*
*Upendo kapata kweli, tulipoifunga ndoa,*
*Mungu 'nipa dawa kweli, moyo wangu kutibia*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

*Wakati tunapokula, upendo ulitawala,*
*Mapenzi tukaridhila, hata pia lipolala,*
*Bila kuengaengala, penzio likatawala,*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

*Majibu yakatokea, zawadi tukapokea,*
*Nasi bila kuchelea, mtoto tukamlea,*
*Ukata ulipomea, tukakaza kumlea,*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

*Mwana kaleta furaha, nyumba raha ogelea,*
*Sikujua ni buraha, kwa muda ingepotea,*
*Ile kapotea raha, machungu yakatokea,*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

*Habari nilopokea, mvua ya mpepea,*
*Kuwa mume kapotea. ajalini kajifia,*
*Majonzi kanyemelea, uyabisi kunijia.*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

*Mara huyu mara yule, ataka anitawale,*
*Utamaduni ni ule, uridhi kudumishele,*
*Haki ziko kwake yule, menishika kama shale,*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

*Mwanangu hayupo tena, eti jana kavamiwa,*
*Chuoni melala ona, hapo wakashambuliwa,*
*Naumia sa waona, raha kwao kama miwa,*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

*Taisha lini kilio, na moyo upoe pia,*
*Nautamani ujio, wake ziraili pia,*
*Niepuke watesao, shida zangu kupapia,*
*Dunia wee mbona chuki nami.*

Sasa watu walimzingira Nanjala.Wapo waliomhurumia, wapo waliomtumbulia macho tu bila hisia zozote. “Tulia mama yangu. Huenda mwanao akawa hai. Hakuna aliyejua waliofariki bado.’’ Jamaa mmoja wa makamo alimtuliza mjane huyu. Kisa cha Nanjala ni kimoja tu kati ya vingi vilivyotokana na uvamizi huu.

Mzee Mulinge na mkewe Kiriro hawakutoa mikono yao mashavuni. Hawakujua furaha tangu mwanao Musembi atoke hospitalini. Mwana huyu ni miongoni mwa majeruhi waliosafirishwa kwa ndege mpaka hospitali kuu ya Takuja. Kwa miezi mitano hangeweza kuamka. Alikuwa mwenyeji wa sadaruki. Alipoziduka alikuwa hana uwezo wa kiakili, kuona, kusikia na hata kutembea. Aliyumbisha kichwa huku na kule tu na

kuuashiria kwa mikono jambo ambalo madaktari walisema kuwa ni ishara ya kuendelea kupona.

Mulinge aliumia sana siku ile daktari wa Musembi alipomwita ofisini mwake na kumjulisha kwa mshauri saikolojia kabla ya kusema naye. “Mzee wangu tuna habari kwako. Kwanza unamwonaje mwanao kufikia sasa?” Daktari alimwuliza angalau kumfanya astarehe. “Nashukuru sana daktari, namwona angalau anayumbisha kichwa, mikono na pia kuboboya kiasi, natumai karibuni atarejelewa na hali yake twende zetu.”

Mulinge alisema haya hali ameyatunga macho sakafuni kana kwamba yale aliyosema yaliandikwa pale au sakafu hii ndiyo iliyoshikilia imani ya maneno yale. “Kweli unayoyasema, mwanao ana bahati sana kuwa hai. Mwili wake umeshangaza yeyote aliyemhudumia kwa uwezo wake wa kupigana na magonjwa. Kama madaktari tulifanya tulichoweza. Imefika wakati ujue jinsi ya kuishi na kumshughulia mwanao afikapo nyumbani tutakapomruhusu kwenda hivi karibuni. Musembi kulingana na uchunguzi wetu, huenda atarudi nyumbani tofatuti na matarajio yako. Uwezo wa akili yake umeathirika kwa kiasi sawia na ule wa kuona, kusikia na kutembea. Inavyoonekana alianguka kwa kichwa pengine katika harakati za kujiokoa. Sehemu fulani ya ubongo ilifikiwa na damu. Jeraha hili linaonekana kuathiri neva zinazopeleka hisi kutoka kwa macho hadi ubongoni. Aidha, masikio yake yalipasuliwa viwambo vya masikio na milipuko ya mabomu. Tunahitajika kumfanyia uchunguzi tuone kama oparesheni nyingine moja au mbili zinaweza kurudisha uwezo wa kutembea. Kwa sasa tutampa kitimaguru mtakachotumia kumtembeza hapa na pale.’’ Maelezo haya yalifika wakati yakaacha kuwa na maana. Mawazo ya Mulinge yalianza kuzunguka. Daktari alifika mahali akagundua alikuwa anajiongelesha akafupisha maelezo yake. Mzee huyu alifikiria mahitaji ya mwanawe mapya na gharama yake kubwa akahofu sana. “Na hawa madaktari nao wana mambo, anamaanisha nini kuwa Musembi ‘ana bahati’. Hawa ni wale tu hata mtu akifa katika upasuaji husema upasuaji ulifana ila tukampoteza mgonjwa.’’ Mulinge akapiga taswira ya jinsi mambo yangekuwa magumu kwake na mkewe ambaye alikuwa mgonjwa wa shinikizo la damu. Wadogo wa Musembi bado walihitaji karo. Alishangaa jinsi shida zilivyomwandama kama kivuli. Kweli upele humpata msikucha. Wakuongeza hili wakasema kuwa, mkata hendi mkele angenda mkele kapakia jahazi mtele na hurudi na upele.

Ufasaha wa misemo hii Mulinge aliujua kwa kina kwani ilisawiri maisha ya adha yaliyomwanadama.

Masaibu aliyopitia ujanani mwake pale wazazi wake walipokatwakatwa na jirani yao Tanuri kwa sababu ya mpaka wa shamba hayana mfano wake. Aliachiwa mzigo wa kuwalea wanuna wake jambo lililomfanya kuacha shule vile tu alikuwa amejiunga na kidato cha kwanza.

Kwa ushawishi mkubwa aliokuwa nao Tanuri, hata chifu hangezuia akina Mulinge kuingiliwa. Mulinge akaishia vibaruani; mara mijengoni, mara hotelini muradi ndugu zake wawili wale na wasome kwani alishaamua kuwa mhanga. Hii ndio sababu alioa katika umri wa miaka arobaini na mitano. Ndugu zake hawa baada ya kupata shahada zao wakamwona kama mkoma wasimfae kwa lolote licha ya kuwa katika kazi kubwa zenye mishahara minono. Sasa ni mzee wa miaka sabini na mitano. Aliona mbele kweusi na nyuma kweusi. Akili ikaacha kufanya kazi. Akabaki kujipuna kindevu tu. ‘‘Mzee Mulinge,’’ yule mshauri alianza. “Najua una hisia mseto akilini mwako, “usihofu mwenzangu, nitapanga kikao na familia yako tusemezane jinsi Musembi anafaa kushughulikiwa.” Aliyoyasema kutoka hapo hayakumwingia mzee Mulinge. Alichosikia ni kwaheri ya wale viumbe. Akasimama na kuundea mlango bila neno. Daktari alimwita kumkubusha kicha cha funguo alichokuwa ameacha pale mezani. Akakirudia kama roboti na kutoka.

Mkewe Mulinge alipiga Moyo konde, akamfaa mwanawe kwa kila lililohitajika. Miaka kadhaa imepita sasa na alishazoea majukumu yake juu ya mwanao. Musembi amerudiwa na akili yake na uwezo wa kuona na kuongea lau kwa kiasi. Angeweza kujiendesha, akaenda haja na kujiosha. Alijiunga na vikundi mbalimbali vya watu kama yeye na kujikubali kabisa. Pia alipata ufadhili wa masomo na hivi karibuni atakuwa mwalimu. Mwulize Mulinge atakwambia kwamba mtu huona na kuamini anachotaka. Yeye na mkewe waliamua kuona uwezo wa musembi ila si ulemavu. Walimpenda na kumdhamini bila kumwaibikia. Wakafunga masikio yao kwa ulimwengu wenye mawaidha kinzani wakafuata ya daktari na yule mshauri saikolojia. Ushauri wa watu wengi heri uchawi; utakubomoa badala ya kukujenga.

Likupatalo patana nalo bila kijisaza; hujazaliwa hujaumbika. Sasa Mulinge alikubali msemo wa daktari wa Musembi kwamba alikuwa na bahati. Kamati ya kuchunguza shambulizi hilo la chuo kikuu iliundwa na

rais. Ripoti ya kamati hii haikuona mwanga wa siku. Wengi walitania kuwa ilihifadhiwa kuja kutolewa siku ya kiama pamwe na ile ripoti nyingine ya Muumba mwenyewe itakayoamua wa peponi na wa motoni.

Walioponea chupuchupu walimshukuru mungu kwa ibada na sadaka. Majeruhi waliishi na makovu mwilini kama shuhuda. Swala nzima la ugaidi ilikuwa ni swala tete lililozungumzwa kwa sauti za chini kama siri ya kilinge. Kama uji moto habari hii haikupaparikiwa. Hata ungepata habari zilizomfaa polisi ulikuwa na sababu za kuhofu. Waliofanya hivyo walilalamika kupokelewa kwa shaka. Walihangaishwa na wengi kusingiziwa wao ni wanamgambo waliotumiwa kuchunguza vituo vya polisi. La mno ni kuwa iliaminika kuna askari na makachero waliokuwa katika kundi hili.

Hata pahali pa ibada hali ilikuwa sawia. Kule pwani ya nchi kulikuwa na pasta maarufu aliyekuwa mwanamgambo. Alihubiri na kufisidi dini dhidi ya nyingine. Alionyesha na kudhibitisha vile wote wasiofuata dini fulani walivyofaa kuuawa. Aliwaagiza waumini wake kuwaangamiza wasodini. Wapo waliona upotovu wa mahubiri haya wakatoka wasirudi tena pale. Wakaguria maabadi mengine. Baadhi walimrekodi kwa simu na kutuma mitandaoni ikavifikia vyombo vya usalama. Wengi walimkosoa waziwazi naye hakusita kuwatishia pia. Kutokana na ukali wake alijishidia jina majeneza.

Chuki ya kidini haikufaa kabisa kama bado Mungu ni yule mmoja wa upendo, upole na umoja. Dini zote zimejikita katika guzo hizi muhimu. Aidha, ibada yangu haiwezi kuadhiri ile yako. Kwenda kwangu jehanamu hakuwezi kuadhiri safari yako ya mbinguni. Kutembea na aliyevaa tambara hakuwezi kufanya suti yako nzuri kuchakaa. Waliokuwa na dini moyoni na akilini walizidi kupinga mahubiri potovu na kuyapuzilia kama mtazamo wa mtu binafsi.

Majeneza alikuwa mfadhili mkubwa wa kundi la Sinautu janibu hizo. Kando na hayo alitumika kuwashawishi vijana wadogowadogo kujiunga na kundi hili. Angewapa vijana hawa pesa na kuwaahidi nyingi zaidi watakapojiunga. Wasio na kazi waliambiwa kwamba kulikuwa na kazi kibao na zenye malipo ya kutamanisha. Hao wangenaswa na utandu wa tamaa yao na kuishia katika msitu wa Mbuyu. Msituni humo mambo yalibadilika. Walinyimwa hiari wakabaki roboti kufuata maagizo tu. Wakapewa mafunzo mbalimbali kama kutumia bunduki, gruneti na hata kutengeneza mabomu. Aidha, waligawanywa katika makundi na kupewa

kazi za nyanjani; kuna wale walifanywa makachero. Kazi yao ilikuwa kuchunguza maeneo ya kushambulia. Pia wangechunguza mienendo polisi na vyombo vyote vya kiusalama. Walipanga mipangilio ya kushambulia na kuchora ramani ya maeneo lengwa zilizoashiria njia za kuingilia na kutorokea. Kundi la pili ni lile la washambuliaji. Waliketi na makachero wakapewa mipangilio na ile ramani. Kutokana na uhaba wa vijana siku hizi wanaopatikana walipewa mafunzo yote; kuchunguza na kushambulia.

Kama kaida kazi ni ujira. Vijana hawa walipodai mshahara wao walipigwa na kutishiwa. Walishakula kiapo kutumikia sinautu hata katika hatari ya maisha. Aliyeonekana kujua haki zake alipigwa risasi mbele ya wenzake ambao wangesinyaa. Hapo ndipo ilipowapambanukia kwamba ile haikuwa kazi tena bali utumwa; minyororo ya kujifunga wenyewe. Wakaishi kwa machungu ya ningalijua.

Baada ya muda Majeneza akamea mkia wa nge kila alipokwenda bila kujua. Kutwa moja alipatikana amelishwa risasi kadhaa kifuani. Wakaadamana wa kuandamana, wanahabari nao wakapata posho kotoka kwa habari hii moto.

Doreen aliamka na kujipata hospitalini na bibi yake kando. ‘‘Bibi niko wapi? Nilifikaje hapa?” Alifadhaika mtoto wa watu. Akajaribu kuinuka akahisi uchungu mwingi tumboni akapiga kite. ‘‘Tulia mwanangu tulia. Shukuru Mungu uko hai. Nilikuleta hapa kama umezirai. Unakumbuka mama yako akikuletea sharubati pale tulipobarizi roshani? Muda kidogo ulianza kulia maumivu ya tumbo.’’ Bibi alimsaidia Doreen kuvuta kamba nyuma.

‘‘*Okey, I remember now*! Na mama yu wapi sasa. Alinileta hapa pia?’’ Alisaili huku shaka fulani ikijijenga akilini mwake. ‘‘Doreen usijali, muradi u hai. Unahitaji chakula, maji au matunda hivi?” Bibi alikwepa mkondo ule wa maswali.

“*Come on shosh*. Mimi si mtoto kulengwa hivyo. *Tell me the truth, mathee alinileta hapa hosi?”* Doreen alimkazia nyanya yake macho. ‘‘Si wajua mama yako nawe shingo ngumu. Hata gari lake kulitumia ilikuwa muhali. Ilinibidi nimzabe kofi anipe funguo. Tulikuleta hapa na Dan. *I had to drive for once in ten years to save you darling!* Ila nakusihi usimbebe mama yako. Msamehe. Kitoto ulichohimili kimetoka. Yaaminika ni *Food Poisoning.*

“Nilijua tu ni yeye. Mama yangu ni mnyama. Mbona anitendee kama adui. Mbona aniamulie maisha yangu. Sina hiari kama mtoto?” Doreen alilia kwa machungu. ‘‘Yaani hata hakujali kama ningefariki akijaribu kudumisha *status quo.* Heri waliozaliwa katika umaskini. Angalau wanaheshimiwa na kudhaminiwa. Heri umaskini wa mali kuliko umaskini wa upendo na amani. Ni kweli kupata mimba ningali chuoni ni kosa. Lakini ni makosa gani huyo malaika niliyebeba alitenda kunyimwa nafasi ya kuishi? Mbona mwanadamu achukie kiumbe dhaifu kama huyo? Mbona awe mwamuzi wa kukipa au kukipoka nafasi ya kuishi? Kwa nini mama kanishirikisha katika mauaji?” Doreen alizidi kuumwaga moyo wake huku nyanya kamtumbulia macho ya imani. Alijua kwa kufanya hivi mtoto huyu angepona.

‘‘Nachukia vyeo na mamlaka. Kama si hivi tungekuwa na wazazi. Hatungekuwa tunatumiwa kama vyombo na nyenzo za kuumbia mamlaka na jina, Nimeishi nawe bibi tangu utotoni mama aliponizaa na kuniacha

nikiwa na miezi sita kukimbiza hizo shahada za nga’mbo. Miaka mitano baadaye ndio angekuja na “*How have you been my daughter*.” Nikama kama mtu aliyerudi tu kutoka sokoni. Miaka mitano! Nyanya miaka mitano… Hivi mimi titi la mama sikulijua. Hata kumtambua kwenyewe sikumtambua; wewe ndiwe niliyeita mama muda wote huo. Uhusiano wangu na mama ni kama wa mpagaji na mwenye nyumba. Isingekuwa wewe bibi, hata mambo muhimu ya utu uzima singejua, Kwa vyovyote, wewe ulifaa kuhisi aibu anayodai kuhisi mama sasa.

Baba naye ni kiguu na njia akisaka kura mpaka usiku wa manane. Alipoingia bungeni tulimwonea runingani kama watu wengine. Alipokuja nyumbani wikedi alikuwa amengojewa mara kama mgeni wa heshima katika michango mbalimbali, mara mikutano na wanachama wa *C.D.F*, alimuradi kuwe na jambo lililomfanya kupitia tu nyumbani bila ya neno na wanawe. Uongozi gani huu bibi? Kazi gani hii? Ya kuzima moto kwa jirani kwako kukiteketea?

Dan kaka yangu heri mimi. Babu aliendа kusiko kurudi miaka mingi iliyopita. Hana wake. Ni kama msibaba. Hajapata kiumbe wa kiume wa kumlea kwa makuzi ya kiume. Anabambanyabambanya tu tabia. Si bure amekuwa bomba la pombe. Ni bure ameitwa Wamunyota mtaani. Waama asiyejua aendako hapotei njia. Popote afikapo ndipo hapo.

Bibi hivi niambie, nitarudi, nitarudi kwa hiyo jehanamu ya nyumba kutazamana na mama uso kwa uso? La, la, sitaki kuambiwa nilimvunjia mzazi heshima.’’ Doreen aliongea mengi. Alikuwa na haki. Alikuwa mwenye donda jipya moyoni na lililovuja damu. Alihisi usaliti wa wazazi. ‘‘Aah! Nawe acha kufanya hasira mwanangu. Nitazungumza naye,” bibi alimtuliza.

Ni katika juhudi za bibi kudhibiti hali hii mgoto uliposikika mlangoni. Mwenda aliingia mle amebeba matunda mbalimbali. ‘‘Dorry vipi?’’ Alisaili huku akimbusu pajini. Doreen akaangua kilio. Mwenda akalia, bibi naye akajiunga nao, ikawa kwaya bila mwelekezi.

‘‘Mtoto wetu hayupo tena. Mama anahusika kwa hili.’’ alisema kati ya kekevu za kilio. ‘*‘Haina noma beb. Sir God atatubless na mwingine*. Bado nakupenda hata kama wazazi wako ni wagumu kiasi. Nishaongea na wangu, hawana shida tena.’’ Mwenda alimtuliza nyonda wake.

Muda wote huu daktari mmoja alikuwa pale. ‘‘Hii hali inaitaji mshauri nasaha. Acha nimpigie *Dkt*. Mercy Mbalu.’’ Alisema haya akinyanyua simu yake ya mkononi. ‘‘La!’’ Wote watatu wakasema kwa pamoja.

Siku tatu baadaye Doreen aliruhusiwa kwenda nyumbani. Naye alishaamua kuwa pale kwao hapamweki tena. Alijipatiana kwa dunia imle imbakishe, impende, imchukie. Haya yalikuwa mamoja kwake wakati ule. Dunia nayo siwajua mti mkavu, huparagwa kwa nyenzo na tahadhari. Yakini msichana huyu alihisi uyabisi mtimani. Aliona chuki kwa kila kitu, hata nzi kutua utosini mwake wakati ule alihisi na kuona dhihaka.

***

“Kumpa chui kazi ya kulinda mbuzi wako ni kuingia hasara kwa hiari. Jameni tufungue macho ya mwili na fikra. Matongo na maluwiluwi tuliyotiwa makusudi na wanajinufaisha kwa upofu wetu natutoe. Kudanganywa jua la mtikati sasa na iwe historia. Mla ni mla leo, mla jana kalani? Hizi ahadi zimekuwa mwangwi. Zimekuwa njaa iliyowapa watoto wetu utapiamlo na kutuangamizia wazee. Ahadi hizi zimegeuza barabara kuwa hospitali wanakojifungulia kina mama zetu, zimekuwa sadaruki wanakofia wanatunu.

Wanatunu hoyee! Wanatunu hoyeee! Uongo marufuku! Ubinafsi marufuku! Ufisadi marufuku!’’ Sauti nyororo na dhabiti ya kike ilipasua anga ile katika jukwaa moja mjini Tunu. Sauti hii si geni tena Tunu. Sauti yenye mawazo na mitazamo shawishi: iliyojaa ukakamavu na ujasiri. Dharura alishaamua kumpigia debe Karani aliyewania kiti cha ubunge. Kupigania kiti hiki dhidi ya mwamba kama Mbalu kweli ni kama kumgusa punda tako. Karani alijua hili, Dharura pia alijua sawia na wote waliojua siasa za eneobunge hili. Lakini hili halikuzima hari yao hii nadra.

“Wanatunu sasa wamepevuka! Wamechoka! Wamechoshwa na ahadi sizizofika. Ahadi za Mbalu za asali na maziwa zimechelewa kwa kitambo sasa. Ameziweka kwenye mgongo wa kobe makusudi. Daima zimo jiani zaja. Hatutishwi tena kwa mapigo wala mauti. King’ora cha mwamko mpya kishalia. Hatuna bundi kuamka. Mwanatunu, mbwa hafi akiona ufukwe!” Dharura alizidi kunena. “Kijana huyu Karani hana pesa. Hana ushawishi wa kitaifa. Alichonacho ni nia ya kuwanasua kwenye kinamasi cha uhawinde. Hatoi sera tofauti na zile mlizozoea. Ahadi yake

ni moja; kutoa ahadi kwenye mgongo wa kobe na kuzitia kwenye mgongo wa farasi. Kwa kufanya hivyo mtaona hospitali yetu kuu ya Kalawa inayokaa sasa kambi ya wakimbizi ikiimarika. Mtaona dawa katika zahanati zetu hazitamea mbawa tena. Hakutakuwa na kununua maji kwa shilingi ishirini kwa mtungi wa lita ishirini. Mto Heri na Kalawa yatosha kusambaza maji kwa mifereji kwa kila boma ya mwanatunu kama tutoa hizo mashine zinazolia usiku na mchana msitu wa Hidaya. Barabara zetu zitakuwa na lami kutokana na mgao tunaopata kutoka kwa serikali kuu kupitia serikali ya kaunti. Hizi fedha zimekuwa zikiingia kwa mifuko ya watu wachache tunaowajua. Wakati wa kampeni kama hizi tunarambishwa kwa kupewa pombe, chumvi na majora ya leso. Tunu hoyee! Karani hoyee!'' Watu walipiga makofi kwa msisimko mkuu.

''Sasa nalialika jabali lenyewe, mwamba usioyumba, simba wa Tunu asiyeogopa vitisho. Tunu ni mtunda. Sasa umetuzalia tunda njema. Karibu Karani karibu, karibu tunda letu.'' Dharura alimpa Karani kipasa sauti na kuketi.

Msisimko mkuu ulihinikiza soko nzima la Tunu. Shughuli zote zilisimama. Waliokuwa mbali wakajongea karibu angalau kupata nafasi ya kumtazama kijana aliyejitolea mhanga. Wengi walijitia ulingoni kama yeye wakaishia ufuoni kabla ya uchaguzi. Wengi walimhurumia kijana huyu Karani kwa kuhofia hatima mbaya.

"Sasa huyu kijana amejitia ujuaji wa kumpa bafe dole atatoboa?'' Mzee mmoja mkongwe alimwuliza mwenzake. Unakumbuka Tufani, aliyekuwa mkurungenzi mkuu katika kampuni ya maziwa ya *Ng'ombe Dairies*? Alipatikana ameelea mto Kalawa siku mbili kabla ya kupiga kura. Kama hatima ya Tufani haimpigi mshipa, basi yeye ni msomi mpaka anajua yaliyomsibu Ndatu Kilinga. Mkulima mkubwa wa majanichai. Alifumaniwa nyumbani kwake usiku mkuu, mkewe na mabinti zake wawili walibusu risasi baada ya kutendewa yasiyosemeka. Ndatu naye akakatwakatwa vipandevipande vilivyotapakazwa kila mahali katika soko lili hili. Mbwa wakapata mana. Mhadhara wake wa mwisho ulikuwa kwenye jukwaa lili hili hapa. Anafaa aogope sana mwana wa Kalatu. Hastahili uhayawani wa Mbalu. Watu anaowapigania watamsahau tu baada ya siku mbili tatu za kubeba matawi na mabango na kupayuka kama mbayuwayu walevi katika barabara za miji. Aidha, baada ya kutumainishwa na vyombo vya usalama kwamba 'Tutachunguza,

tutafuata kila dokezo kuwapata waliohusika na kuwafungulia mashtaka kwa mujibu wa sheria.'

Karani anafaa ajue siri ya ndege wa angani kuwa wengi ni ule woga wao. Hawajisalimishi kwa adui. Na ajue tena kwamba, woga ndio huishi kuonyesha magofu ya zilizokuwa nyumba za mashujaa. Kwa shujaa huenda kilio, kwa mwoga huenda kicheko. Haina haja mtoto wa watu kutuliza''

Yule mzee mwengine alimgeukia, ''Heri vile hukuzaliwa wakati wa ukoloni. Tungekuwa na wabeberu hata leo. Mitazamo na hofu yako ni sawa lakini mtu hawezi kutupoka haki zetu za msingi muda huu wote. Tumemwogopa na kumwabudu kitambo sasa. Imetosha. Karani kama ni wa kufa atakufa na mwengine ataibuka. Mwishowe huyu baradhuli atatupa ile heshima ya nyuki na mrina asali. Kile kiko sasa hakifishwi hakimo kwa Karani bali kwa kila mtu isipokuwa wachache kama wewe.''

"Tunu hoyee!! Tunu hoyee!!'' Karani alipasa sauti tulivu yenye mnaso wa aina yake. "Yangu mwenzenu si mengi. Mama yangu hapa amesema yote. Ninachotaka kutilia mkazo ni kimoja. Kwamba sisi sote tu safarini. Hatima yetu ni moja. Kufikia panapo ndoto zetu kama wanajamii wengine. Watoto wetu kusoma katika shule zenye maji ya kutosha na miundo msingi. Kutibiwa katika hospitali na zahanati zenye madaktari, wauguzi na dawa. Ndio, tumo safarini kukutana na uhuru wetu. Tutembee bila kuhofia kabari njiani. Tuongee bila kukatwa ndimi. Bila vitisho. Naam, tuwekeze bila kuhofia mioto isiyoeleweka kula hazina zetu, bila kuogopa na mabuludoza. Tule nyama isiyo na kemikali sugu angamizi. Wanatunu mpo?" Karani alisita kutadhmini athari ya maneno yake kwa watu. "Tupige siasa za sera si za bunduki na mapanga. Siasa komavu sisizo na kusiribiana kinyesi na za hujuma; siasa za demokrasia.

Safari hii si yangu ni yetu. Tuianze bila kutahayari na tutafika. Hata kifo changu hakiwezi kuwashika mguu. Kifo cha Musa hakikuwazuia wana wa Israeli kufika Kanani nchi ya ahadi. Najua mnahofia hatima yangu. Nahofia hatima ya wanatunu kuliko yangu. Wanasiasa wengi chipukizi wameangamia kwa njia tata kufikia sasa. Roho za hawa mashujaa wetu hazijapumzika hata zione ukombozi wa Tunu. Damu yao na iwe kafara ya mwisho mwanatunu angetoa kupata haki yake ya msingi. Umefika muda tuamue kwa kauli moja kwamba haki haifi! Tuzidi kuipigania mpaka tuipate. Wiki ijayo ni uchaguzi.

Sikwambii unipigie kura. Pigia usalama wako kura. Pigia uhuru wako. Pigia elimu ya mtoto wa mwanatunu. Naam, pigia afya yako na maono yako!’’

Ilikuwa katika harakati za Karani kumaliziamalizia hotuba yake Dan alipokuja mbio na kuelekea jukwaani alipokuwa Karani. Akamnong’onezea jambo fulani. Hakudiriki kumaliza gumzo ile ya dharura kuliposikika mlio wa bunduki kutoka upande wa nyuma wa jukwaa. Watu wakapiga mayowe na kuanza kufyatuka kila upande kama viroboto.

Karani alishtuka kuona Dan anamporomokea. Alikuwa mwenyeji wa risasi mgongoni. Watu wachache waliokuwa wamejificha chini ya jukwaa walitoka kujiunga na Karani na Dharura wengine walipoyeyukia kusikojulikana.

“Nyinyi tuachieni hali hii. Torokeni. Hii risasi haikuwa yake, ilikulenga wewe Karani. Tokeni hapa ila msiende nyumbani, ingieni mafichoni mpaka hali itegenee. Hizi ni ghadhabu za simba jike,” mmoja wa wale watu alitahadharisha.

***

Hii ni siku ya tano tangu Dan ajeruhiwe na kukimbizwa katika hospitali kuu ya Sifa mjini Takuja. Sifa si hospitali ya akina mimi na wewe; ni hospitali ya wenye nchi. Mbalu amefika jukwaani Tunu kuhutubia watu ila ameshtushwa na watu wachache waliokuwemo. Hii ni baada ya siku mbili za kulevya watu na kusambaza majora ya leso na chumvi. Kwa mara ya kwanza akaingiwa na wasiwasi. Miaka yote hii mihadhara yake imefurika watu. Alikasirika. Hangeweza kuwahutubia ‘vipanya’ wachache kama wale. Alimwachia mmoja wa vinara wake wa kampeni kufanya vile, naye moja kwa moja hadi nyumbani.

Pale upweke ulimpiga pambaja vilivyo, akahisi kama mkoma. Mkewe alishajenga kibanda mjini Takuja kumhudumia mwanawe kwa karibu. Doreen naye aliyoyomea kusikojulikana. Bibi naye alihamia pwani kwa kitindamimba wake. Pale ni yeye na Kite -mbwa wake- tu walitamalaki mastakimu yale ya kifahari. Hakujua alikaa sebuleni kwa muda gani lakini kwa hakika ilikuwa kitambo. Alikuwa kazama katika bahari ya mwazo. Alikumbuka wapinzani aliowaangamiza akaona fahari

iliyochanganyika na hofu. Hofu ya Ng'e kujing'ata kwa mkiawe. Akawaza na kuwaza tena.

'Wale wajinga hawangefanya kazi safi? Niliwatuma kuinyoosha njia yangu ya kurudi bungeni wakaishia kumjeruhi Dan… Na huyu kijana wa Kalatu mpaka awe mchawi. Amekingwa na werevu huyu. Itakuwaje amemteka Dan bakunja hata akamwona yeye bora kuliko babaye. Karibu hata amfie!'

Mbalu alisongwa na mawazo. Japo yeye na mwanawe wameishi kama wafanyakazi wawili katika ofisi moja ambao hawakuwa na budi kuonana, alimdhamini Dan kama mridhi wa mali yake ya ndani na nje ya nchi. Ndiye mkongojo wake wa siku za uzeeni. Ndiye atakayemfunga macho na kumzika. Alishangaa kama Dan alijua hili Mbalu aliamua kufanya kikao na mwanawe pindi atakapotoka hospitalini. Mpaka amtie akili na kumjukumisha mwana huyu.

'Doreen alitokomea wapi jamani? Hakika hayuko kwa akina Mwenda kwani ningekuwa nimemwona kule. Hayuko pia kwa jamaa zangu ama za mama yake. Tungekuwa na taarifa kufikia sasa. Simu nayo kazima, makachero nao ni kama wameshindwa na kazi yao.'

'Lazima nimlaumu mama na nyanya yake kwa kutompa makuzi mazuri. Makosa zaidi ni kwa Mercy kukitoa kile kidudu alichokihimili. Haidhuru, kingeishi tu muradi niwe na mwanangu nyumbani. Nitamsaka!' Mbalu alinyanyaswa na mawazo yaliyomtoa jasho pajini na kushukia shavuni.

***

Mtaa wa mabanda wa Makesi ni mojawapo ya mitaa mitatu ya aina hii mji mkuu wa Takuja hujivunia kuwa nao. Hii ni baada ya miongo mingi ya kufyonza vijana kutoka vijijini na miji mingine humu nchini. Tangu kale, Takuja umekuwa sumaku. Hata enzi za mababu watu walisafiri miezi mingi kwa miguu kuja Takuja kutafuta kazi. Enzi hizo kazi haikuwa ngumu kupata, muradi umeona kuta nne za darasa ukajua Kiswahili na Kingereza cha haja. Hii ni kwa sababu hakukuwa na wasomi wengi kukidhi nakisi kubwa ya ajira katika makampuni ya wazungu, waarabu, wahindi na ya wafrika wachache waliopevuka mapema. Nakumbuka, tajiri mmoja kijijini mwetu aliyekuwa akifanya kazi kama

bawabu katika hoteli moja maarufu enzi hizo mjini humo. Kama tulivyohadithiwa na nyanya, alikuwa mwanamume wa kwanza kuvaa viatu na suruali ndefu kando na Padri Muntin wa parokia ya Kikatoliki eneo hilo. Aidha, mzee huyu alikuwa na jaketi lililopakwa rangi kama viatu! Nywele zake za kipilipili nazo aliziacha zikawa ndefu, akazichana zikasimama kichwani kama mpunga shambani. Daima hangekosa kitana mfukoni. Wazee waliyeyukia kwake kila jioni kusikiliza redio. Alikuwa mtu wa pili kuwa na redio maeneo hayo kando na kasisi Muntin.

Ungesikia baadhi ya wanakijiji wakishangaa, “Huyu mzungu ni mganga, itakuaje anase sauti kwa hiki kisaduku? Mpaka ni mganga.’’ Mwengine akadakia, ‘‘Mzungu ni jini hasa! Huoni anavyopaa angani na hii anayoiita ndege? Mpaka ni jini!’’ Hawa watu hujibadilishabadilisha. Huenda akajifanya nzi na aje hapa na kutuchunguza. Nguvu kama hizi ni za mizimwi.” Nkware angesikiliza tu akawacheka. “Mzungu ni mtu wa kawaida kama sisi ila amesoma. Inatufaa tusome pia. Nishaanza masomo yangu tayari.” Nkware aliwaarifu. ‘‘Toba! Masomo gani hayo yanayomdunisha mwafrika na tamaduni zake. Masomo haya ya Muntin dhidi ya tohara za wasichana wetu na ibada zetu za kiafrika ndiyo masomo? Mmoja wa wazee pale alichemka kwa hasira na kuapa kwa miungu ya baba zake kuwa hangesoma wala kusomesha wanawe.

Nkware alianza kuwapikia kahawa iliyopatikana tu Takuja pale barazani alipokuwa likizoni. Aliporudi kazi mkewe akaachiwa lile jukumu jukumu la kuzima kiu ya wazee. Aliongeza tumbaku na uji wa mtama. Kutanabahi, kwake kukawa makutano ya wazee wa kijiji. Hata baraza ya chifu ikahamia pale.

Nkware aliporudi nyumbani baada ya miezi sita, alihitaji mtu wa kumhakikishia pale palikuwa kwake. Alikuta kiduka kilichoshiba bidhaa za kila aina si chumvi, sukari, tumbaku na vinginevyo. Isitoshe pale nje chini ya mwembe kulikuwa na viti na meza waliponywea uji wazee. Mkewe Nkware alimjukumisha binti yake kufunguamimba shughuli za jikoni isipokuwa kuwahudumia wateja wake. Mwulize kwa nini atakwambia wanaume huuma. Mtoto huyu alipomaliza upishi alimtoa mama yake dukani.

Nkware alikuwa mwepesi wa kuona upenyu wa kibiashara. Alipoenda mjini tena alirudi na bidhaa mbalimbali za kuuza kama vile shahani, vijiko, vikombe na vinginevyo ambavyo vilikuwa nadra pale

kijijini. Hivyo ndivyo alivyoacha kazi yake ya ubawabu na kuwa mwanabiashara mashuhuri. Hela nazo zikamkubali. *Nkware Shopping Centre* ikazaliwa. Akatoa watoto wake wa kiume malishoni akawapeleka shule ya kimisonari pale parokiani. Kwa mtazamo wa kiuchumi, Nkware alikuwa mkwasi. Mikutano muhimu ya kiutawala haingekamilika bila uwepo wa jamaa huyu. Wazo lake pale hata la kipuzi lilichukuliwa kama hekima ya Suleimani. Alikuwa kiungo muhimu cha jamii yake nafasi aliyoitumia vyema kujikuza kibiashara.

Lakini hakuna mchele usiokuwa na dume. Katika safirisafiri zake, Nkware alitangamana na watu wengi mjini; waafrika kwa wazungu wanaume kwa wanawake. Kuna huyu Kanene. Msichana wa kutamanika. Kama ni umbo alikuwa nalo. Kimavazi alijichagulia mavazi yaliyoafiki umbo lake. Kanene alikuwa ameajiriwa na mhindi mmoja pale Takuja, mtaa wa Jionee katika duka kubwa la jumla. Alikuwa mtani na mwingi wa bashasha. Wakachukuana sana na Nkware kitabia. Muda ulivyosonga ndivyo ulivyowaunganisha viumbe hawa wawili. Ikawa Nkware hakodi tena nyumba afikapo mjini. Akawa anawekwa rumenya.

Baada ya muda Nkware akaanza kukohoakohoa na kujihisi mnyonge. ‘Lazima ni malaria’ Alijiambia. Akachemshiwa matawi ya mwarobaini na mshubiri akanywa. Siku zilivyozidi ndivyo maumivu ya tumbo na kichwa yalimlemea.

Mwili wake uliotutumka kama ngoima sasa ukaanza kuyeyuka. Vidonda vidogovidogo vikauzunguka mdomo wake. Hili lilianza kumshtua. Akaanza kuwagongagongea waganga milango. ‘Mahasindi wangu wasiopenda maendeleo sharti wamenitilia hewa yangu sumu. Wameanza kuokota vumbi ya nyanyo zangu.’ Alifoka kimoyomoyo. Nkware aliwahakikishia na kuwaahidia mahasimu wake dhahania vita vya Negasaki na Heroshima. Sasa Nkware alisimikwa sawasawa. Kila asubuhi kabla ya harakati za siku angerauka kukoga kwa maji yaliyochanganywa na dawa. Kadhalika alipuliziapulizia nyingine katika duka lake.

Ni miezi miwili sasa tangu alipokanywa kulala kitanda kimoja na mkewe wa miaka mingi. Hakufaa kuonana macho kwa macho na mwanamke asubuhi ama siku yake ingepata ukuba. Uwele huu wa ajabu ulimfanya kupunguza safari zake za Takuja kuendea ‘*mzigo’* kama alivyoita bidhaa zake. Siku moja alijikakamua akafika huko. Alimwendea

Kanene dukani asimpate. Kudadisi aliarifiwa kuwa kimanzi yule alikuwa ameiaga dunia kutokana na ugonjwa usioeleweka. Alirudi kijijini mabega yamemshuka kama kuku aliyelala nje kwenye mvua kali ya masika. Alitafuta mtu wa kumfariji asipate. Akatamani mtu wa kumfungulia mtima wake uliotishia kupasuka asipate. Ushirika wake na yule msichana ulikuwa siri ya wawili. Hapo akajua kuwa siri ni nanga. Akamuua kujikaza kiume. Nkware hakuishi sana baada ya safari hii. Kijiji kizima kiliomboleza mtu mashuhuri aliyeona mbele. Mwaka mmoja baadaye mke wake alimfuata kwa ugonjwa wenye dalili zilezile. Nawe si wajua kuwa mti mkuu ukigwa wana wanyuni huyumba? Watoto wake waliparamia mali kwa pupa na papara. Haya yote yalitoka katika kumbukumbu za nyanya yangu kana kwamba ndio yanatendeka.

***

Makesi, kama lilivyo jina la mtaa huu kumejaa vituko na vitushi. Ni mtaa uliowavuta watu wa kila aina; wazuri na wabaya. Isipokuwa tu matajiri. Wenye kipato wangesikika wakiapa, ‘‘Heri kutumwa jehanamu kuliko kutumwa Makesi.” Majengo katika mtaa huu kwa kiasi yaliafiki usemi huu. Ni tajiri yupi angepita mtaa wenye vibanda vya mabati kuukuu na maboksi na hata vyandarua vya mbu. Akienda wapi? Mtaa uliotapakazwa vinyesi vilivyofungwa kwa karatasi za nailoni na maji machafu yanayonuka kupindukia yanayopita katika vijito vidogovidogo. Hata mtu ataliegesha gari lake wapi? Kufumba kufumbua gari lenyewe litakuwa limegeuzwa vipuli. Hapa wageni hunuka ugeni. Hata panya wa pale anajua mgeni ati! Makaribisho ni kupokwa ulicho nacho jua la mti kati kandamnasi ya macho yasiyopepesa. Ukiwa Makesi usiulize nyama ni ya mnyama gani kwani hugharamiki sana kuila ukashiba. Chochote kinachopitia kwa moto huwa chakula.

Huu ndio mtaa Jimmy huita nyumbani. Alifika hapa akiwa na miaka miwili. Baba yake alioyapata fununu alikuwa mbunge alipokutana na mama yake. Wakati huo mama yake alikuwa ndio amejiunga na kimojawapo cha vyuo vikuu mjini Takuja.Ndoto yake ya kuwa mhandisi ilimea mbawa pale alipopatana na huyu bwana katika hafla ya kuadhimisha siku ya mtoto wa kiafrika pale chuoni. Mbunge huyu alikuwa miongoni mwa waliohudhuria hafla hii katika ukumbi wa chuo hiki.

Baada ya salamu za kawaida baada ya hafla ile mtoto wa mtu akapata rafiki karimu na mpole. Alijihisi malkia chuoni. Alikujiwa wikendi kwa magari yaliyokubali macho. Angeondoka kwa gari moja na kurudi na nyingine tofauti nzuri kuliko la awali huku amenunuliwa vitu vingi ambavyo baadhi hata hakuvihitaji. Msichana huyu akajihisi kileleni mwa mlima wa tunu na tamasha. Kitambo kidogo mitindo yake ya mavazi na nywele ikawa tofauti. Baada ya mwaka mmoja alikuwa mjamzito. Jimmy akazaliwa. Ufadhili nao ukafa. Mbunge akaingia mbugani. Nyumbani alikataliwa na kijalaana chake, akajipata mtaa wa Makesi. Alifanya vibarua angalau aulinde uhai wake na wa mwanawe. Ni katika pilkapilka hizi alipopigwa dafrao na gari lisilojulikana akajifia papo hapo. Jimmy mtoto wa miaka sita akawa msibaba. Msimama mtaani humo msiutu. Hakujua alikotoka mama. Hakujua jamaa yeyote. Akaanza kuchupa kutoka kibanda kimoja hadi kingine akiomba chakula. Hakuna msiba usiokuwa na mwenza. Moto ulizuka katika kimojawapo cha vibanda pale mtaani karibu na kile cha Jimmy urithi pekee wa mama kwa mwanawe. Hivyo ndivyo aliishia kulala nje na kupigania makombo na majibwa ya mtaa huu majaani hadi pale Kanini mmoja wa marafiki wakuu wa mama yake alipomwalika kuishi naye na wanawe wawili wa kike-Sussy na Jossy. Kanini amekuwa kama mama yake mpaka alipomaliza masomo yake ya kidato cha nne kupitia mradi wa elimu bila malipo na ufadhili wa mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali. Kutokana na misukosuko ya kisiasa nchini wafadhili walirudi kwao ughaibuni na kusitisha maono ya Jimmy kujiendeleza kielimu.

Msiri mkuu wa mama yake kijana huyu alikuwa Kanini.Naye aliamua kuzifungia siri zote kifuani mwake. Jimmy alishiriki vibarua hapa na pale kumsaidia Kanini kuwakidhi kimahitaji. Hangekosa kuitia kibindoni kiasi fulani kila alipofanikiwa. Baada ya muda kijana huyu alikuwa amekusanya elfu ishirini na tano mtaji alioutumia kuanzisha kibanda cha mboga na matunda. Wavulana wengi mtaani pale walimcheka walipompata akikatakata sukumawiki. Hakujali vile vicheko. Maishani mwake amechekwa kusimangwa na hata kupigwa. Hili lilimpa moyo mkuu. Hakujali watu. "Cheka tu ukipita asubuhi ukirudi jioni niletee hizo pesa zako nikupe mboga." angewaambia watu hawa kimoyomoyo.

Jioni pale kibandani pale palifurika watu. Wapo wa matunda, wapo mboga. Kazi ilipozidi aliomba msaada wa mama Sussy. Japo

angeona aya, hangekosa kumsaidia. Wateja wake walimpenda kwa upole wake Jimmy angewakopesha walioharibikiwa hali wakalipa baadaye. Kuna wale waliomlaghai ila hili halikumfanya asiwafae waliomwendea. ‘‘Sina haki ya kumnyima mtu deni. Mimi pia nina deni kubwa la malezi ya Kanini. Tena hakuna mtu mraibu wa deni. Si jamaa yangu lakini Kanini amenilea kama mwanawe mpaka nikawa mtu.’’ Jimmy angejikumbusha kila alipoona madeni yakipanda.

Doreen alikuwa mteja mkuu wa Jimmy. Alipotoka kazini alipita pale akanunua mboga. Kazi yake ilikuwa ususi. Alizunguka mtaani Makesi akiwasukia watu nyumbani kwao. Daima alivaa *T-shirt* zilizobeba jina la biashara yake. ‘*THE ME IN ME SALOON*.’ Watoto wa pale walisoma maandishi haya kama ‘Meime Saloon.’ Wengi sasa walimjua kama Meimes. Doreen likabaki jina la Krismasi tu. Yeye pia alilizoea hilo jina hadi alipoitwa Doreen aliyeshtuka kiasi kwa kudhani ni mtu wa nyumbani aliyemtambua. Hata Jimmy alimjua kama Meimes.

Meimes aliyazoea maisha ya Makesi na kuyapenda. Alijihisi mwanamke huru. Sasa aliyaendesha na kuyadhibiti maisha yake ameyaasi yale ya kuongozwa kwa hatamu kama farasi. Maisha ya kufungiwa kama ng’ombe wa maziwa zizini. Hakuwadata wazazi wake hata kwa sekunde ila bibi na ndugu yake. Alihofia alivyoendelea bibi yake. Hata hivyo hangediriki kumtafuta kwa njia yoyote. Hakuwa tayari kurudi zizini. Alishabadilisha nambari yake ya simu na kufunga mtandao yake ya kijamii ambayo ingewasaidia watu kumsaka. Kadiwia mpya alikuwa ameisajili kwa kitambulisho cha bibiye alichokuwa amekifotoa.

Japo maisha ya pale mtaani yaliyajawa na ubeidui na utovu wa nidhamu, Doreen alijiheshimu na kumheshimu kila mtu. Hakuna aliyeweza kujua wala kushuku kijana huyu ni mtoto wa mwanasiasa mashuhuri. Alipotafutwa kwa redio na runinga na magazeti angeshikwa na kiherehere kwani kimbelembele fulani huenda angemtambua. Hili halikutokea kwani hata ni nani katika eneo hili alishughulika na matangazo kama hayo. Kupotea kwa watu halikuwa jambo geni pale.

Jimmy na Meimes walijenga uhusiano wa kaka na dada. Kitambo kidogo Jimmy akaanza kumtazama kwa macho ya mwanamume. Meimes hakuserereka ilipofika kutoa msimamo wake. Angemwambia Jimmy, ‘‘Kaka yangu, macho daima huona ya nje; sura na umbo. Hisia huona moyoni. Hofia sana kupenda na kuchukia. Unachopenda si anachopenda

mwenzio. Ninachohofia sicho uhofiacho. Moyo wangu kaka ni shehena kubwa. Shehena ya hisia mseto. Nikiwa dada yako nitashukuru upeo wa kushukuru.''

Jimmy hakung'amua maana ya maneno haya ya Meimes. Yalionekana kutoka kwenye moyo wenye usiri mkubwa. Alivyochagua maneno yake pia yalimshangaza. Hangebisha aliridhia wawe alivyotaka. Waliishi kufaana kwa hali zote. Kanini hakufurahishwa na usuhuba huu. Alihofia Jimmy angepata jiko kabla ya angalau kupata kozi ya kumkimu kimaisha. Alifurahishwa sana na nidhamu ya kijana huyu. Angewapigia Jossy na Sussy mfano wa Jimmy. Ila alitaka kujua jambo kwa Jimmy.

Jioni moja baada ya kazi pale kibandani alimwita Jimmy na kumwambia ''Mwanangu, unajua ndiwe mwanangu wa pekee wa kiume. Siku zote nikuangaliapo hupiga dua na kumshukuru Mungu. Umenitii ukanitumikia kama mwana. Umejaliwa hekima ya kupambanua mambo. Ulifanyapo jambo huwa halina hila. Siku za hivi juzi nimekuona na huyu Meimes, si kanisani si nyumbani. Hata dada zako sasa wanamjua. Lakini hujaniambia ninalofaa kujua hadi nikaamua nivunje kimya hiki. Je, una nini naye?'' Kijana huyu hakulitarajia swali hili ila alijibu, ''Meimes ni rafiki tu si mpenzi.'' Kanini hakuridhika na jibu hili. ''Kuwa na rafiki wa kike si jambo mbaya muradi mwishi kwa kuheshimiana na wala si kwa hari ya ujana. Ukupigao ndio ukufunzao. Mimi na marehemu mama yako ni ushahidi uliowazi. Singependa mmoja wa wanangu awe kama sisi. Hatukupata labda malezi na makuzi kuhusu mahusiano." Kanini alimweleza mwanawe.

''Wewe mama unajua baba yangu? Anaweza kuwa hai?'' Kanini hakulitarajia swali hili kutoka kwa Jimmy. Lilimpiga masikioni kama radi na kumwingia moyoni kwenye kovu. Nawe ya mwenye kovu si wajua? Nguvu zikamtoroka mama huyu. Macho hayakumtazama tena mtoto huyu. Akalia! Nitamwambiaje baba yake alimkataa angali kijusi tumboni? Ninitamwambiaje bado yu hai na mtu mashuhuri? Akamgeukia Jimmy na kumwambia, ''Twende nyumbani mwanangu. Jibu la swali lako ni msumari moto. Sitaki nikundanganye, subiri mpaka niwe tayari.'' Wakashika njia kwenda nyumbani safari iliyotamalakiwa na ukimya baina ya viumbe hawa. Kila mtu aliyaogopa macho ya mwenziwe.

Usiku huo hawakupata usingizi wawili hawa. Jimmy hakusubiri hata kipindi alichopenda cha runinga 'Maria.' Aliona msabaha mkubwa

wake na Maria yule mhusika mkuu. ‘‘Kaka unaumwa?’’ Jossy, kifunguamimba wa Kanini alidadisi. “La, ni mavunevune ya kazi.’’ Alijibu akiinuka na kuelekea chumbani kwake. Pale kitanda kiligeuka ulingo wa miereka. Jimmy na mawazo, mawazo na yeye. Alielekea kushindwa. Hakuna swali lililopata jibu kati ya mengi aliyojiuliza. Kadri alivyotafuta majibu ndivyo alivyohema kama mnyanyua vyuma. Alipinduka na kubinuka. Akachukua simu yake na kuzama mtandaoni *Whatsapp*. Alishangaa Meimes bado hakuwa amelala pia. Hakumbuki walizungumza kwa muda gani. Alinyakuliwa na usingizi hali ameishika simu mkononi.

Jimmy alijiona kwenye jumba moja la kifahari mjini Takuja. Jumba lake. Jumba hili lilikuwa uridhi kutoka kwa baba yake. Cha kushangaza pia ni kuwa yeye na Meimes walikuwa ndugu. Alipokuwa pale sebuleni kwenye kochi, akamwona kipepeo mmoja maridadi ameingilia dirishani upande wa kushoto. Alikuwa mwenye madoadoa meupe na meusi.

Alivyokaribia alipokuwa Jimmy ndivyo alivyobadilika. Mara akatua kochini karibu naye. Kufumba na kufumbua alijiona ameketi sako kwa bako na mama yake mzazi. Mama alikuwa na tabasamu kubwa usoni. Alikuwa amelivaa rinda alilolipenda lenye madoadoa meupe na meusi. Jimmy aliruka na kumpiga pambaja, ‘‘Ah! Mama yangu mpenzi nimekupeza miaka mingi. Nimetamani nikue nawe, niamkie kupata hili tabasamu lako. Lakini sasa nina furaha umerudi.” Jimmy alimwambia mama yake kwa uchangamfu wa ajabu.

“Mwanangu, dunia ni kama mpira wa soka. Mawanadamu hana hiari upande anakoelekezwa na majaliwa. Hata hivyo, ana hiari ya kuishi katika majaliwa anamojipata. Una uwezo Jimmy. Ndio uwezo mkubwa wa kuzama na kuibuka upigwapo na mawimbi mazito na dhoruba za maisha. Daima usijidharau wala kujidunisha. Ishi bila kijihurumia. Kata kamba za ugumu wa jana yako. Jana ikikuita usiitike. Mwanangu twende nje nikuonyeshe kitu…Ona ona lile jua. Limeishi tangu mwanzo wa nyakati. Limeona mengi. Naam, limeshuhudia dhuluma ya mwanadamu dhidi ya mwenzake. Limeshuhudia huruma kuu ya mtu kwa mwenzake pia. Usiku ujapo, mwezi hushika hatamu na kuendeleza rekodi ya jua. Hakuna litendwapo gizani ukwepa jicho hili la Mungu. Ipo siku mwangu, ipo siku jua na mwezi vitapewa uneni. Vitasimualia kila tukio vimshtakie Mungu. Siku hio kila mtu atapewa haki yake. Ishi kutenda mema

mwanangu, nayo mema yatakufuata. Usimsahau Kanini na ndugu zako. Mtunze na ndugu yako Meimes. Mwondolee machungu yaliyo moyoni mwake. Mwambie bibi anamkwazia sana. Anagoja kumwona tu apumzike." Mama mtu alimalizia. ''Hata Meimes yuko chumbani mwake, ngoja nimwite akusabahi! Meimes!! Meimes! MEIMES...'' "Jimmy una nini?" Kanini ambaye hakuwa amepata usingizi mpaka saa ile aliuliza kutoka chumbani mwake.'' "Oh, ni ndoto tu mama niko sawa." alijibu hali ameshangazwa kabisa na ndoto hio. Ilikuwa mnamo saa kumi unusu hivi za alfajiri. Alitamani arudi katika ulimwengu wa ndoto tena akae kidogo zaidi na mama yake. Usingizi nao ukamwampaa. Na mbona alimwita Meimes ndugu yangu? Ana machungu gani? Ama ndio maana hakutaka urafiki wa ndani name? Potelea mbali.

***

Doreen alikumbuka kaka yake akatamani kuongea naye amjulie hali. Alimpesa sana bibiye. Ni miaka mitatu sasa. Mpaka amekonga sana. Akakumbuka kwamba alitoroka nyumbani wakati wa kampeni. Hajapata kujua kama Karani alinyakua kiti cha Mbalu babaye au la. Alihofia baba yake alimtenda kama alivyotenda wapinzani wa awali. Alichukua simu na kuingia mtandaoni kwa mara ya kwanza tangu atoke nyumbani. Mara akapanua kinywa kwa mshangao, Karani ndiye aliyekuwa mbunge wa Tunu. Aliendelea kusoma, ''God no! Si ndugu yangu Dan. *Someone tell me this is not true!''* Aliendelea kusoma. *''Daniel Moyo Mbalu, mwanawe wa aliyekuwa mbunge wa Tunu kule jimboni Pemba, hatimaye ameruhusiwa kwenda nyumbani baada ya miezi sita hospitalini. Daniel alipigwa risasi katika mhadhara wa mheshimiwa Karani rafikiye wa utotoni na mpinzani mkuu wa baba yake. Duru za kuaminika zinasema kuwa alikuwa amefika jukwaani dakika chache kabla ya kupigwa risasi. Uchunguzi wa mapema unasema kuwa shambulizi lile lilimlenga Karani na si Daniel. Mshukiwa mmoja kwa jina Nduli tayari ametiwa mbaroni kuhusiana na tukio hili na anasadia katika uchunguzi. Sasa Dan amepoteza uwezo wake wa kutembea kutokana na uti wake wa mgongo kuharibiwa vibaya. Bwana Mbalu amepata pigo kubwa ikikumbukwa pia binti yake bado hajulikani aliko mara tu alipotoka hospitalini kwa maradhi yasiyojulikana..."* Meimes akaacha kusoma kile kilichoelekea kumfanya apoteze sasa uwezo wa kuona vyema. ''Huyu Nduli siye niliyemwacha akiwa bawabu wetu? Huu ni mkono wa baba. *''This is pure karma.''* alisonya huku akigonga meza kwa viganja vyake.

Hakumhurumia baba wala mama. Walipanda mchongoma kwa hiari wavumilie utamu wa miiba. Meimes akaratibu simu yake kuficha nambari yake na kumpigia Dan.

Dan alikakata simu lakini akashindwa kukata tabasamu usoni. Hangezuia. Kuzungumza na dada yake kulileta nafuu kubwa rohoni. Kulimzimia kiu ya mapenzi. Viumbe hawa wawili walipendana kwa dhati ya mioyo yao. ‘‘Mungu ni mkubwa!’’ Alijisemea huku akisukuma kitimaguru chake kumlaki mama. ‘‘Umeshindaje mwanangu?’’ Mama alimjulia hali. ‘‘Leo salama mama, karibu.’’ Dan alijibu. ‘‘Leo unamwekamweka kwa furaha. Nini cha mno?’’ ‘‘La, sineno’’ Dan akajibu.

Upande mwingine Meimes alizusha pumzi. Hajui kama afurahie ahuzunike. Alifurahia kujua hali ya nduguye. Vilevile alihuzunika kujua kakaye hawezi kutembea tena. Hizi hisia mseto zilibishania nafasi moja nafsini mwake. Katika hali hii, alitanabahi muda ulikuwa umesonga sana ilikuwa saa tatu asubuhi. Hangetambua mapito ya muda kama mmoja wa wateja wake hangempigia simu.

Meimes sasa anapata hata kazi za kuwapamba maharusi na kutia kibindoni hela za haja. Hali yake kiuchumi imeimarika sana kutokana na watu wengi waliopendelea kupondolewa nyumbani. Kwa siku angeweza kupata hata elfu mbili au hata tatu hivi. Aliamini katika kuweka akiba.

Alitazamia kuukabili mustakabali wake vilivyo bila kumtegemea yeyote maishani. Siku ile Karani aliposhinda uchaguzi wa eneombunge la Tunu. Ilikuwa furaha si furaha, watu walifurika mitaani kwa vigelegele chereko na kayaya. Walibeba mabango yaliyosheheni maandishi mbalimbali: ‘UHURU TULIOTAKA’, Nyingine zikasoma, ‘NIA NZURI HATIMA NZURI’, ‘KANANI NA KARANI’ Kuna hili alilobeba Dharura. ‘TUNDA LETU’ ambalo lilinasa macho pevu ya wanahabari. Kesho yake gazeti moja la Pemba liliangazia sana bango hili.

Karani naye alibebwa na kubigitwa na mabarobaro kwa nyimbo za kishujaa. Ilikuwa fahari kubwa kwa Kalatu na mkewe. Walijiona waliozaa Masihi. Walikumbuka walivyomsomesha mwana huyu kwa kipato duni. Jinsi walivyolalia mate na kuamkia mate. Jinsi madeni yalivyokuwa nembo iliyowatambulisha katika maduka pale mtaani. Walishusha pumzi na kupiga dua ya shukrani. Kweli shida si ngozi ya

mwili ufika wakati ikaisha. Mama Karani alihisi ana kila sababu ya kumshukuru Dharura. Alimwonea fahari mwanamke huyu ngangari kwani isingekuwa ushawishi wake Karani hangefua dafu. Nafuu kwa upande mwingine alifurahi kuwa sasa na rafiki kama Karani. Sasa yeye ni rafiki mkubwa wa mheshimiwa. Alifunga macho akafikiri jambo fulani akatabasamu. Kwake Karani furaha ya ushindi ilimwingia japo kwa tahadhari. Alijua fika ana jukumu kubwa. Dawa ya jukumu nayo moja tu; kujukumika. Kwa muda fulani alihisi uzito wa jambo hili akahofia. 'Je, nitafanya yote niliyoahidi. Nikishindwa je? Na ikiwa shida haikuwa Mbalu ila makateli fulani nitawezana nao?' Alinyongonyea mheshimiwa alipokosa majibu. Dharura aliona haya kwa kumtazama usoni tu. Hakuwa tayari kufedheheka. Aidha, hapakuwa na nafasi ya woga. Walishayavulia mpaka wangeyaoga. ''Sikiliza kijana.'' Alisema akimtazama Karani kwa uso mkali na mkavu. ''Ukubwa ndio huo ulioutaka. Wewe leo si ni mheshimiwa? Jua jambo moja, kazi ya umati sasa imeisha. Imebaki yako. Hata mimi narudia maisha yangu ya kawaida. Aliyebadilika hapa ni wewe. Tunu iko barabara mabegani mwako. Chunga kuserereka. Kishindo chako cha kuanguka huenda kikawa kikubwa kuliko cha Mbalu." Akanyanyuka na kuanza kwenda. ''Mama nakuhitaji, nahofia hilo umesema la mwisho. Naomba uwe mshauri wangu. Usiniangalie kwa macho ya ukubwa. Mimi ni yule tu mwanao. Nikienda kombo usisite kunikosoa.'' Karani alisema vile kwa unyenyekevu wa kitoto.'' ''Ukinihitaji unajua pa kunipata.'' alijibu akiendelea na kwenda.

Alishangaa kwa nini Dharura aligeuka vile. ''Nitapambana, lazima nipambane!'' Alijipa moyo.

Alihisi kuwa alihitaji mtu wa kumchangamsha akili kiasi muradi ajiondolee mawazo ya kazi yake mpya. Alichukua akapigia watu fulani kisha akachukua gari kuelekea Kalawa *Resturant.* Njiani alipiga kuagiza vyakula na vinywaji.

Dan alipopata simu ya Karani alifurahi sana. Akijitayarisha na kumwagiza Ali kumwendesha. Alimkuta Nafuu ndio anafika. Kama kawaida Karani alimrukia Dan kwa pambaja. '*'How are you my good friend.''* Siku hizi simu yako imekataa kunipigia kabisa. Leo unalipa faini ya kupotea.'' alimchangamkia rafikiye. ''Niko tu kaka. Wajua wakubwa si rahisi kuwapata, hupatikana kwa mwaliko tu.'' Dan alisema na wote wakacheka. ''Ah, huyo si mimi labda jirani, niko kwa kila mtu kila

wakati. Mkijua vile nimewadata nyinyi viumbe wawili Dan huwezi kusema hivyo.'' Karani alisema.

Kwa yaliyofuata kutoka hapa ni maongezi ya kirafiki yaliyoakifishwa na vicheko vingi. Dan alipata pia nafasi ya kuwaeleza jinsi maisha yalivyomlemea nyakati nyingine. Vile hata faragha yake imebanwa na hali yake hiyo. Aidha, alihishi kana kwamba ndoto zake maishani zilidhibitiwa pakubwa. Karani na Nafuu walisikiliza haya kwa imani. Kwa mara ya kwanza Karani alihisi kujilaumu kwa hali hio ya rafiki yake. Dan alitambua hivyo upesi. ''Karani niko sawa, usijilaumu kwa hali yangu hii. Tulaumu siasa mbaya. Baba alitaka njia ya mkato kurudi bungeni. Nilikuwa nimemkanya dhidi ya kukufanyia maasi, ndipo akaamua kuyapanga kwa siri kuu. Kwa bahati mbaya au nzuri nilipata taarifa kuchelewa. Nikakupigia simu hukuchukua, nikaamua kuja mbio kukutahadharisha. Sikujua niliharakisha kuja kupokea risasi ya kwako. Heri hivi. Watu wajue mkuki kwa nguruwe pia mchungu kama ulivyo kwa mwanadamu." Dan alisema haya kwa wepesi wa moyo. Karani alihisi mapenzi ya dhati katika maneno hayo. Akanyanyuka akampiga pambaja huku chozi likimteleza shavuni.

"Dan *trusts me* nitafanya niwezalo kulipa upendo huu ulionionyesha. ''Alisema haya huku amepiga goti moja mbele ya Kitimaguru cha Dan huku amemshika bega. Wakati huu Dan alisafiri mawazoni mpaka zile enzi za chuoni. Alikumbuka juhudi za Karani kumvua katika kinamasi cha dawa za kelevya. Anazikumbuka nasaha zake zilizojaa uhalisia uliorashiwa mapenzi ya undugu. Mwanzomwanzo alimpuuza Karani kama kijana mwengine yeyote wa bara asiyependa kujaribu usasa. Dan aliingizwa katika matumizi ya dawa hizi akiwa shule ya upili kidato cha pili na rafikiye mmoja aliyekuwa mtoto wa waziri wa afya. Sasa alikuwa mraibu sugu wa afyuni. Hangemakinika kujumuisha moja na moja apate mbili bila kuionja. Karani kwa kutumia cheo chake na mtagusano wake mwema na watu wengi, alimtafutia mshauri nasaha ili kuyapiga jeki maaso yake. "Mimi kusema ukweli siwezi acha *unga''* Alimwambia yule mshauri. "Unaweza tu kuniambia nipunguze. Unga ni poa bora uitumie kijanja. Uutumie kwa focus. Kwa mfano nikitaka *kuconcentrate for long* mpaka nipige *puff*. Hadi nikitaka kuomba unga hunileta karibu sana na Mungu." Yule mshauri alimsikiliza kwa utulivu bila kuonyesha hisia zozote. Alikuwa na kibarua kigumu kwa kuwa wazazi wake Dan hawakushughulika kwani waliona ulevi kuwa sehemu

ya maisha ya kawaida ya vijana. Alijitolea hata hivyo. Dan akamponyoka makononi kwa uraibu wa dawa za kulevya. Kwa hili tu Alimhusudu Karani. Marafiki kama yenye ni kama wamebaki wawili tu duniani yeye na mwengine mmoja kule India!  Alimpenda kwa dhati. Adui wa Karani alikuwa wake pia.

Baada ya kurejea kanisani, Dharura alichukua nafasi ya mwumini wa kawaida. Yeye na binti yake walisali wakajiendea. Huku si kusema aliridhika na unafiki ule wa Mwema, ila mara hii alijua siri ya simba mwenda pole.

Mwaka mmoja baada ya uchaguzi kitumbua cha Nabihi kiliingia mchanga. Jumapili hii Mwema baada ya kuhudumu siku nzima, alikuwa amechoka tiki. Alijipumbaza kochini kutazama taarifa ya saa moja jioni kwenye runinga yake kubwa ajabu. Yaliyotangazwa yalikuwa yale ya washukiwa wawili wa wizi kupigwa risasi. Kwingineko Jamaa fulani kujitia kitanzi baada ya mzozo wa kinyumbani. Walimu kutishia kugoma na kulemaza shughuli zote za elimu kulalamikia mishahara duni.

Mwema alikuwa katika hali hii ya kusinyika taarifa fulani iliposomwa ikashika na kunasa akili. Mwili wake nao ukawa mkufu.

Mwema alisonya kwa hasira iliyochanganyika na woga. ‘‘Nani huyu aliyenichimba kiasi hiki? Nala jasho langu. Tena silazimishi mtu kutoa mimi…lakini walipataje habari hii? Huenda nikashikwa mara hii. Lazima yule mganga Okwonkwo alinindangaya. Si alisema nikitumia ile dawa yake -fungafunga- siwezi tambulika… sasa ona…ona. Lazima Dharura anajua kinachonila."

Mzee Kenga hakupitwa na habari hii. Yeye hajawahi kushiriki kanisa lolote japo alimwamini Mungu. Alienzi na kutambua haki na usawa. Mambo ya Mwema yalimpa mawazo mazito. “Imani ni ngumu mpaka sasa maneno hayajatosha kuelezea maana yake hasa. Unachoamini hudhibiti hisia na mawazo yako. Hudhibiti utendakazi wa mtu na maisha kwa jumla. Lakini wakati mwingi hatuchagui imani. Tunarithi kutoka kwa wazazi wetu ama walimu wa dini. Hii imechangia kuishi katika imani tusizozielewa na ambazo hatuna uhuru wa kuzifanyia utadhimini makusudi kwani unapofanya vile unadaiwa kukufuru. Tumerithi na kurithisha nyara za imani. Kuna jambo ambalo hutawala imani zote. Wazee na walimu wa dini huwa katika mstari wa mbele kueneza imani. Tunachokichukua ni chapa kamili ya imani zao. Ni chungu vipi sasa kwa waumini kutambua kwamba kiongozi wa imani yao ndiye aliyeifisidi. Hutamausha na kuvunja moyo. Huchochea maasi yasiyomithilika.

Itakuaje aliyeijua njia sasa kapotea? Heri kuchezea kazi ila si imani ya mtu! Mtu hufia imani ati! Haihalisi mtu mmoja kuchezea watu kama mtoto achezeavyo tiara.” Mgogoro huu akilini mwa mzee Kenga uliashiria mengi yaliyofikiriwa kuhusu Mwema.

Mkono mrefu wa serikali sasa ulimfikia nabihi, ukamtabiria kwa mujibu wa sheria. Kanisa liliyumba. Lilikuwa kama basi ambalo dereva wake amezirai hali ameushika usukani. Likawa lile jahazi la kuzama. Waumini wakatazamana wasijue la kufanya.

Siku moja Dharura alipata wageni wasio wa kawaida kwake. Wazee wawakilishi wa makanisa yote matatu. Alihofia walijua mchango wake katika taarifa zilizoenea na kusambaa. Hata hivyo nadhiri zake hazikumsuta.

‘‘Bi Tija, tumeleta heri kwako leo. Tunalo ombi moja kwako. Kwamba utusimamie kanisa letu hata pale kesi dhidi ya Mwema itakapoamuliwa. Tumeona unaweza.’’ Alishtushwa na maneno haya ya wageni wake hawa. ‘‘La! La, si Mwema alikuwa na wasaidizi wake, mbona wasishikilie hiyo nafasi?’’ Dharura alibisha. ‘‘Tunajua hayo yote dada, ila si wajua kuwa ukimsalimu mwenye tope mkononi tope hukupata pia.’’

Baada ya ushawishi wa muda mrefu, Dharura aliomba muda wa kuliwazia swala lile. Baada ya majuma machache waumini na washiriki wa karibu wa Mwema walianza kuyoyomea kusikojulikana. Nao wazee wale wakamua kumrudia Dharura. Haikuwa rahisi walivyodhani. Alikubali kushikilia ile nafasi muradi tu atamwachia Mwema nafasi yake arudipo. Ujio wa Dharura kama kiongozi wa kanisa lile ulizua msisimko wa aina yake, waliomjua mwanamke huyu walijua kanisa limepata kiongozi.

Kesi ya Mwema ilienda sambamba na ile ya Mbalu. Mbalu alikuwa ameshikwa kwa amri ya kiongozi mkuu wa mashtaka ya umma nchini. Alishtakiwa kwa ufisadi na jaribio la mauaji. Tangu ang’atuke kitini mambo yalimwendea mvangemvange. Yakawa yale ya kifo cha nyani. Mkewe Mercy siku hizi amekuwa mlevi kupindukia. Huja usiku wa manane akipayuka maneno yasiyoandikika. Alikuwa mtunzi wa nyimbo na mashairi alipobugia vileo. Akiangalia maisha yake aliyaona kaka tupu la yai. Alihisi ombwe kubwa moyoni.

Ni miaka mingi tangu Mbalu na Mercy walipolala chumba kimoja. Hapa ni pale mkewe alipopata fununu kwamba mumewe alikuwa anatoka nje ya ndoa jambo ambalo alilikana na kuapa kwa miungu ya mababu zao. Mercy alimjua mtu wake. Alijua aliposema ukweli na aliposema uongo. Mara hii aliona uongo usoni mwake. Akaamua kumpa uhuru aliohitaji na asiohitaji.

Siku hii Mercy alikuja kwa kishindo. Mbalu hakuwa amelala hivyo alisikia vituko vyote vya mkewe. Walakini hakutaka kuzua zua usiku ule. Hakutaka kumsumbua Dan aliyeonekana kasumbuka tayari. Pia hakuwa tayari kwa maneno yasiyochunjwa.

Dan aliumwa na maneno ya mama. Aliuma kidomo cha chini kwa maumivu. Hakuzuia kundondokwa na chozi. Chozi chungu la moto kutoka moyoni. Alijiona mkosi na mjalaana aliyestahili kunyimwa uhai asiuone uso wa nchi. Kibaya zaidi ni kule kuitwa kiwete na mama mzazi. Dan akaamua kumpigia dadaye kumweleza nia yake ya kujitoa uhai. Alikuwa dhabiti katika uamuzi wake huu na ilivyoonekana hakuna kitu kingeubadili. Meimes hakuamini maneno hayo yalitoka kwa Dan. Akachukua simu akaandika ujumbe mfupi na kuwatumia Mwenda na Karani.

*Hujambo? Mwandani wako Dan ana mawazo ya kujitoa uhai muda wowote kutoka sasa. Amenieleza hayo muda mfupi uliopita. Shughulika uwezavyo. Mimi niko mbali.*

*Rafiki yake Meimes*

Iilikuwa saa kumi unusu Jumamosi ile. Wikendi kwa wengi huwa siku ya kulipa deni la usingizi wa wiki nzima. Mwenda alijinyoosha na kubingiriabingiria kitandani kama jongoo. Alinyanyuka na kuangalia saa kwa simu yake.  Aliona onyesho la ujumbe mfupi ila hakushughulika kusoma kwani siku hizi arafa hizi ni kero kuu. Kwa siku unaweza kupokea arafa karibu kumi na kati yazo ni moja au mbili zilikuwa na umuhimu. Alisimama akaenda msalani na kurudi kitandani. Bahati mbaya usingizi ni kama aliuacha alipotoka. Mwenda akanyanyua simu yake tena kuangalia mpalingilio wa mechi za UEFA wikendi ile. Kabla ya kuitua simu aliamua kuupitia ule ujumbe mfupi. Aliruka kama aliyeumwa na Ng’e. Mwenda alijipata sebuleni mbio, jambo lililowashtua watu asubuhi ile. ‘‘Kwema Mwenda?’’ Baba yake alaisaili. Hangeweza kueleza kwani

pumzi zilimwenda mbio, akamkabidhi babaye ule ujumbe. Baba na mwana wachukua gari na kuelekea kwa Mbalu. Walimpata Karani ashafika ila amezuiliwa hata asipate kuelezea sababu za ujio wake pale kwa mpinzani wake hasimu.

Mwenge aliwaeleza walinzi kifupi kilichojiri. Shughuli katika boma hili zikachukua mkondo mwingine. Kilio si kilio majonzi si majonzi vilitanda pale. Pale kwa mara ya kwanza, Mbalu akaishiwa na nguvu akalia kwa sauti kuu ya uchungu aliyekuwa pale kumfariji hakuwa mwengine ila hasimu wake wa kisiasa Karani. Alihitaji kufarijiwa hata hivyo, hata kama kungetoka kwa mchawi! Askari walifika pale baada ya muda mchache na kuanza uchunguzi wao. Walipata kichupa kidogo walichoamini kilikuwa na kile kilichompa Dan nauli ya kuandama njia ya kusiko na kurudi. Mercy alilia. Kwa mara ya kwanza alihisi mapenzi kwa mwana huyu katika mauti yake. Uchungu wa mwana wa uzazi ukazalika moyoni. Sauti ilipotea macho nayo yakavaa miwani miekundu. Kamasi na machozi vilibusiana tayani. Miongoni mwa vitu walivyovibeba askari wale ni pamoja vijibarua vitatu alivyoviacha mezani. kimoja kwa Doreen, kiingine kwa baba na kingine kwa mama yake. Viliandikwa kama ifyatavyo:

*Kwa mpendwa Doreen,*

*Dorry msiri wangu. Kwangu umekuwa kila kitu. Ulinifaa pakubwa. Umenifanya niishi mpaka leo. Nakumbuka utoto wetu ulivyojaa furaha. Tulicheza tukasahau upweke wa kuwa mayatima walio na wazazi kama ulivyopenda kusema. Nilitamani tuishi katika hali ile daima. Ulimwengu wa wawili. Shuleni pale watoto wengine walikataa kucheza nasi tulicheza wawili. Masomoni tuliwabwaga kwa vishindo.*

*Maisha ni kuisha mpenzi. Mtu akifikia hatima yake hana budi kujisalimisha kwa ulimwengu wa pili. Nisamehe dada yangu. Niridhie uamuzi huu wangu upate amani na nayo roho yangu istarehe. Najua uchungu nitakaokuachia. Nimekuachia uvundo wa ukiwa. Laiti ningalibadilisha hali hii. Ninavyoishi hapa kwetu na huu ulemavu wangu nimekosa hamu ya kuishi. Wanarika wenzangu wameajiriwa wameoa na kusonga na maisha. Mimi hapa nilipo hata haja za msingi sijiwezi. Wazazi wangu wamenipuuza. Kila nikitolewa nje na Ali kuwasabahi marafiki, chajio kilikuwa kukemewa. Wanaaibikia ulemavu walionisababishia. Kunifungia nyumbani ni afadhali kuliko kunitafutia*

*kazi ya kufanya. Kikundi cha walemavu cha Pemba kimewahi kufika hapa kikiomba nijiunge nao kisipewe makaribisho. Mwanadamu ni uhuru. Mwanadamu ni mwengine. Nimeamua niwaondokee wazazi wangu si kwa uoga wa maisha ila kwa kuheshimu nafasi yao. Mimi kwao ni kama mgeni aliyezidisha mwaliko wake.*

*Nitakupenda Dorry hata katika kifo. Hata ulimwengu wa ng'ambo ya pili. Tafadhali ukijaliwa watoto waambie walikuwa na ami aliyewapenda hata kabla ya kuzaliwa kwao. Tuonane siku ya kiama. Buriani mpenzi dada.*

*Wako wa heri na shari Dan.*

Barua kwa baba:

*Kwa Mheshimiwa Mbalu,*

*Wakati sasa umefika baba. Muda wa tadhmini na darubuini ya moyoni. Kufuata kilicho muhimu kwako. Heshima, cheo na utajiri wa mali na sifa. Sifa ambazo zimekuwa pumzi na nishati ulizohitaji kuishi. Umekuwa kwa misingi yote mwanamume katika jamii. Wamekusifu wengi isipokuwa aila yako. Tabia yako imeishi kuibua mgogoro wa kisayansi. Daima wanyama hudhamini zaidi watoto na wanyama wa kundi lao. Hata simba na ukali wake wote ule huwatunza wanawe. Hukaa karibu nao Huwakinga. Hucheza nao. Huwapa mafunzo muhumu ya kuishi nyikani kando na malezi.*

*Sijakuwa karibu nawe kama mtoto wa kiume na baba yake. Nimeishi kukujua kama tu mfadhili mkuu. Ulitununulia vyote tulivyohitaji na tusivyohitaji ila hukutupatia baba. Nakumbuka ukinichapa nikiwa mtoto nilipokwambia utununulie baba na mama wengine tuwe tunakaa nao kama tulivyokaa na bibi mlipoondoka kwa vipindi virefu. Yalitosha kujua tumekula, tumekunywa, tumevaa na kusoma. Nashukuru kwani haya uliyafanya vyema.*

*Laiti mali uliyotafuta ingeipa familia yetu amani, mapenzi na usalama wa wazazi kwa watoto. Mali hii haikutupa umoja. Siku zote tulikuwa heri kinyesi cha mbuzi; mboleavunde hasa. Hapo ulipo mwenyewe huna raha na mali uliyotafuta kwa mikono yako.*

*Na je, inaridhisha siasa uliyocheza baba? Siasa iliyonilemaza? Sasa mimi kwako ni aibu; kinyesi usoni mwako. Tena naibana nafasi yako uliyoilinda kwa uchu. Nakuondokea baba. Maisha niliyoishi yalikuwa yako kwani niliishi ulivyotaka si nilivyotakiwa. Uwe na kheri baba. Na kama hili tendo langu litakugeuza na kukugutua, waite wenzako kama wewe, wenye mali na vyeo faraghani.*

*Wako Dan.*

Barua kwa mama:

*Kwa mshauri nasaha Mercy Mbalu,*

*Mama nakutuma safari fupi. Safari ya hisia. Safarini omba kumbukumbu ziandamane nawe. Zitakuwa mashua katika safari yako katika bahari ya mawazo. Nenda kamwulize mkunga aliyekusaidia kunizaa swali moja. ''Je, niliona uchungu wa uzazi?'' Mwache asimulie labda uchungu wa kunizaa uliuzika pamwe na kitovu usiukumbuke tena.*

*Au labda ulinipata bila kutarajia, ukachelewa kuniavya, naye mkunga akakataa kishirikana nawe kuninyima uhai. Tangu hapo ukaniamulia adhabu isiyo kikomo.*

*Safari ya kurudi itakupa funzo. Huenda penzi la mama likafufuka. Utaona ulivyowatesa uliowaita wanao. Mama siku zote hung'ang'ana kuwakinga wanawe dhidi ya dhuruba za Maisha. Wakilia hulia nao. Mama huwa wa mwisho kuanguka akiwalinda wanawe wakati wa hatari. Mama huweza kusimama na kujenga boma. Huvumilia pasipo kiwango. Kwa misingi hii mama, utarudi na jibu. Utatadhimini uone kama jina tulilokuita lilikufaa.*

*Mshauri nasaha mtajika jimboni. Aliyewashauri na kuwabadilisha wengi. Ila aliyefanya kazi kama taaluma tu, si wito. Ama ni mtu karimu aliyewapa maji wenye kiu hali koo lake limekauka kama jangwa. Laiti ungejinasihi mama leo hii hungelia kama kweli utalia.*

*Leo nafa sijaona mama kwako. Niliona mwanamke msomi na mwenye bidii katika kazi yake. Aliyejistahi kama mke wa mheshimiwa, jambo lililokufanya umtendee maasi dada yangu. Ulihofia taaluma yako itiliwe doa na mimba ya mwanao, ukachagua heshima dhidi ya mjukuu wako asiyekuwa na hatia. Hivyo ndivyo nilivyompoteza dada na bibi yangu kukamilisha sura kamili ya jehanamu nyumbani humu walimoniacha.*

*Sikuwa nifanye ninayotaka kufanya ila maneno yako ya usiku yamenisukuma. Kwende mema kwako mama.*

*Ukitoka safarini kutana na wanawake wengine wasomi wenye nafasi na vyeo kama wewe na uwape semina.*

*Wako kiwete Dan.*

Mnamo saa tano asubuhi, Meimes alikuwa ametumiwa ujumbe kumwarifu kifo cha 'rafiki yake'. Habari hizi zilisambaa kila mahali, mitandaoni. Alipata habari hizi akiwa kibandani kwa Jimmy. Meimes alipasua kilio, akajirusha chini na kumboleza kwa huzuni mkuu. "Mbona kaka yangu. Mbona umetenda hivi? Waniachia nani jamani? Nitaishi vipi bila wewe? Laiti ungalinisikia ungalikuwa hai leo mpenzi.'' Jimmy alijaribu kumtuliza rafikiye kwa juhudi ila alielekea kuwezwa. Watu walimzunguka Meimes aliyekuwa amejulikana sana pale mtaani kutokana na kazi yake ya nyumba kwa nyumba. Walimhurumia msichana huyu mzuri wa sura na tabia. Jimmy alizidi kushangaa ni vipi hajawahi kumtajia ndugu au hata mmoja wa aila yake katika mazungumzo yao mengi. Akafunga kibanda na kumchukua nyumbani pamoja na majirani wengine waliokuwa katika kundi lile. Pale kwa Meimes palijaa waombolezaji. Wengine walilia wakitamka maneno na kuzungukazunguka huku na kule wakishika mara kichwa mara kiuno kama wanaocheza ngoma ya kitamaduni. Baadhi ya waombolezaji walijitwika jukumu la kuwapikia wengine chai. Wazee waliofika pale waliitana faraghani kisha wakarudi wakawakusanya watu pamoja wakatoa rambirambi rasmi kwa mwezio Meimes. Meimes hangefikiria kwamba angerudi nyumbani kwa namna hii. Hakuwa na budi. Mpaka angemzika kakaye.

Usiku wa kuamkia mazishi mabasi matatu yalitoka Makesi kuelekea Tunu. Yalifika keshoye saa sita unusu kama mazishi tayari yameendelea kidogo.

Kujitoa uhai siku hizi ni kama fasheni. Limekuwa jambo la leo hapa kesho pale. Mabadiliko ya taasisi za jamii kama familia ni jambo moja kati ya mengi yanayolaumiwa kusababisha vifo hivi. Si bure kuona mzee wa miaka sabini na zaidi akijitoa uhai. Mpaka kuna chembechembe muhimu maisha ya sasa hayana. Kulingana na takwimu za W.H.O takriban watu laki nane hujiua kwa njia moja au nyingine kila mwaka. Hii ina maana kwamba mtu mmoja anajiua baada ya kila dakika arobini! Wengi wa hawa huwa vijana wa kati ya miaka kumi na mitano hadi ishirini na tisa. Takwimu hizi ni makadirio tu ikizingatiwa kuwa visa vingi haviripotiwi kutokana na unyanyapaa unaofuata familia za wahusika. Vifo hivi aidha vimechangiwa na mambo kadhaa. Kwanza ni dawa za kulevya. Vijana wanaotafuta kujitambulisha katika jamii wamo katika hatari hii. Hawa ni wale vijana wamesahaulika na wazazi wao

wenye shughuli nyingi. Pindi tu wanapobalehe wazazi wengi hupumzika na kuwapatiana kwa ulimwengu usio na huruma. Watoto hawa hushawishiwa na wanaonadi dawa hizi. Wanapokuwa waraibu hufanya chochote kupata hela za kukata kiu yao iliyoongezeka kila uchao. Huiba, hunyanganya na hata kuuza dawa hizi zenyewe kwa wanarika wenzao. Utumizi wa dawa hizi huathiri mifumo ya akili ya kufikiria na kufanya maamuzi jambo ambalo linalowafanya kufanya mambo yasiyo ya kawaida kama kuacha shule, kuwa na fujo, kubaka na hata wakati mwingine kuua. Hapo jamii nayo huwa na haraka ya kuwaelekezea lawama zinazowatia msongo wa mawazo. Kujitoa uhai kwao huwa suluhu rahisi kujitoa katika ulimwengu wa hukumu.

Pili ni kutamauka. Vijana wengi wamewekewa viwango na wazazi wao ambavyo wanafaa wavifikie. Mzazi humchorea mtoto ramani ya vile anafaa aishi. Sharti afuzu masomoni ili atoshe kuwa mtoto mwema. Vingine hana Maisha. Ashapoteza ufunguo wa pekee wa kufungulia tunu za maisha. Talanta kama za riadha, uimbaji, uchezaji wa soka hupuziliwa kama upotezaji wa wakati. Vijana wanapokosa kufikia viwango hivi hukumbana na unyanyapaa kutoka kwa walio karibu zaidi. Huitwa majina na kutumiwa kama mifano mibaya ya kuonyea jamii. Wapokosa watu wa kuwaelewa wanakata tamaa na kujichukia.

Dhuluma za kimapenzi. Vijana wanaodhulumiwa kimapenzi huwa na uwezekano mkubwa wa kujitoa uhai kulingana na wanasaikolojia. Mbaya zaidi kama wameambukizwa magonjwa ya zinaa. Dhuluma nyingi kama hizi huwa zimetekelezwa na watu wa karibu. Aidha, dhuluma hizi huwapata vijana wa kike kwa wa kiume. Wale wa kiume huumia zaidi kwani jamii bado haiamini kuwa wanaweza dhulumika kimapenzi. Hii si kusema kuwa wa kike hawaathiriki ila wao wanayo mifumo iliyostawi ya kutetea haki zao.

Usaliti wa kimapenzi. Kumekuwa na visa vingi vya watu wengi kuwaua wapendwa wao na kisha kujiangamiza kwa kile kinachotajwa kama kuwepo kwa mpango wa kando. Maafisa wengi wa polisi wamejiangamiza kwa njia hii pale wakubwa wao walipopeleka virauni kwa familia za wadogo wao.

Kupoteza kazi au jamaa yako. Ebu chukulia umepoteza kazi iliyotia chakula mdomoni na kulipa bili zako. Una mkopo wa benki unaotishia kutwaa ulichonacho. Watoto wamefukuzwa shuleni. Una

mzazi mkongwe anayekutazamia kwa matibabu ya kila leo. Ebu fikiria yule mtoto wa mzazi mmoja aliyefariki akiwa ndio anajiunga na shule ya upili au chuo kikuu? Ikiwa watu kama hawa watakosa ushauri nasaha wa kutosha jambo rahisi watakimbilia ni kitanzi kujitoa katika mawazo ya ndoto zilizoporomoka.

Vijana wenye ulemavu wa aina moja au nyingine wanafaa kuonyeshwa upendo na ukubalifu katika jamii. Wanapotengwa nao hujitenga.

***

Mbalu na Mercy hawakuwa washirika wa dini yoyote. Ilikuwa vigumu sana kupata kasisi wa kumzika mwanao mpaka wakajipata mlangoni kwa Dharura aliyewaonea imani. Dharura sasa alikuwa anaendelea na ibada wakati ujumbe wa Makesi ulipofika. Alisitisha ibada kwa muda kuwapa nafasi ya kuketi. Meimes alishuka kutoka basini amevaa rinda refuu jeusi lililomkaa barabara na kuonyesha umbo lake la kutamanika. Kifuani kwenye rinda hili kulikuwa ua jeupe upande wa kulia. Kichwani alifunga mtandio mweusi. Kuficha wekundu wa macho yake alivaa miawani mieusi. Mikononi alishika shada la maua meupe. Waliomwona na kumtambua walikuwa wazazi wake, bibi, Mwenda na wachache wengine waliokuwa na macho pekuzi. Alitafuta nafasi kwenye umati mkubwa wa watu na kuketi. Watu wake nao walimzunguka. Muda kidogo Dharura alisikika akisema "Tunatambua kufika kwa dada yake Dan Doreen, hivyo anaombwa ajongee hapa jukwaani panapo na familia yake. Wanamakesi walizidi kushangaa jinsi mtoto wa mtu mashuhuri kama Mbalu alivyotoka nyumbani kuzurura Makesi. Wengine ndio walipata kujua jina lake halisi. ''Labda kama rafiki wa Dan wa dhati Meimes yuko katika ujumbe uliofika pia anaombwa ajitambulishe.'' Aliendelea kupokea magizo naye akiyatangaza. Jina la Meimes lilikuwa la kwanza katika orodha ya marafiki ambao wangezungumza.

Mazishi haya yalihudhuriwa na viongozi wengi wa kisiasa akiwemo gavana wa Pemba Daktari King'ori. Karani alikuwa pale kama rafiki na kama kiongozi.

Dharura alifunga kwa maombi ya mwishoni pale shughuli zote za maziko zilipotamatika. Katika homilia yake alikuwa ameonya wanandoa dhidi ya misimamo migumu inayoweza kufungia mazungumzo. ''Familia

ni kufahamiana na kufaana. Si vita vya ni nani mwenye usemi.'' alisikika wakati fulani akisema.

Watu walifumukana mmoja mmoja wawiliwawili au kwa vikundi. Dharura alishamwona dada yake Kanini. Imepita miaka mingi tangu waonane dada hawa. Walikuwa na mengi ya kusema na kutatua.

Doreen aliwafuata wazazi wake sebuleni. ''Karibu nyumbani mwanangu. Tusamehe wazazi wako. Hakuna singizio la kutosha la kutowawajibikia nyinyi wana wetu. Tulighalifika na maisha, tukaandama mali na taaluma takapuuza majukumu ya uzazi. Kama mama yako nimeiumbua familia yangu. Nilishindwa kukupa mfano bora. Najuta. Najutia kwamba imechukua kifo cha Dan kumaizi haya. Nichukulie mama yako na unione upya, tupe nafasi tujirekebishe.'' Mercy alisema haya akilia. "Ni sawa mama. Nimewasamehe nyote. Naomba baba usiseme neno. Natuanze upya. Nimeumia kuweka chuki dhidi yenu. Imetosha. Kwa sasa naomba niwatambulishe kwa marafiki zangu ili waanze safari ya kurudi.''

Kanini muda huu wote alionekana mwenye hawafu. Akili yake haikuwa kwenye mazishi, kilichokuwa pale ni kiwiliwili tu. Hawezi kumbuka kilichosemwa pale isipokuwa hotuba ya Meimes tu. Alitoa pumzi nzito kila baada ya muda mfupi. Jimmy aliyekuwa kando yake wakati wote aliyaona haya. Aliposaili aliambiwa ni uchovu. Ukweli ulikuwa ulishampambanukia. Alijua jambo wasilolijua wengine.

Alipomwona Meimes akitoka nje ameandamana na wazazi wake kuwajia alivaliwa na woga wa asichokijua. ''Hii ndio jamii yangu ya mji wa Takuja mtaa wa vibanda wa Makesi. Tumeishi pamoja kufaana.'' Aliwaeleza wazazi wake waliojaribu kusukuma tabasamu angalau kuonyesha kuridhika. ''Pia, nimekuwa kama mmoja wa wana wa Kanini. Kanini hawa ndio wazazi wangu. Ninaye kaka kwa jina Jimmy Kariga. Jimmy wasabahi wazazi wangu.'' Doreen alimalizia na kumpa babaye nafasi.

Mbalu alikuwa na hisia mseto. Hakujua kama afurahi, asononeke au ahofie. Kwa mara ya kwanza aliona majaliwa katika utendakazi wake. Alikuwa ametazamana uso kwa uso na kiumbe aliyemkana miaka mingi iliyopita. Isingekuwa kuwa kifo cha Dan labda hangemwona Jimmy. Alimwangalia akampenda, alivyokuwa kijana mwenye nguvu na

mtanashati labda kwa makusudi ya Mungu kukejeli baba yake mtoro kwa kutowajibika. Leo hii aliamua liwalo na liwe. Cha kuvuja kivuje, sharti angekosoa kasoro zake za jadi. “Si hata yule mmerekani muuza maziwa Jeffries Randal alikuwa na watoto karibu mia nane na wateja wake miaka ya kendamia hamsini?” Alijitia moyo. Hakujali Mercy angesemaje sasa. Moyo ulimtuma kuungama. Alichohofia tu ni kukataliwa na Jimmy. Akiamua kuwa hukumhitaji baba je? Aidhuru, atakuwa amefanya fungu lake. Kanini tu ndiye aliyeelewa wazii wasiwasi aliokuwa nao mzee huyu. Hata yeye alikuwa na hofu kwamba Jimmy atakapomjua babaye angemwacha. Hakuwa tayari kumwachilia kijana huyu hata kwa dawa. Alimwita mama naye akamwita mwana tangu umri wa miaka mitano. Alikuwa na haki kwa huyu mtoto ikizingatiwa jinsi alivyosumbuka naye pamoja na wanawe wawili kwa kutegemea vibarua tu. Laiti angalijua hangalifika kwa mazishi yale. ‘‘Nashukuru kwa kuja kutufariji na zaidi ya yote kwa kuishi vyema na Doreen au Meimes kama mnavyomjua huko mjini. Lakini pia ni siku muhimu kwangu, siku ya kukosoa kosa la jadi nililofanya. Mke wangu nakuomba radhi mbele ya umati huu na mbele ya mwanao Doreen. Nilipoingia bungeni kwa mara ya kwanza nilizaa mtoto na msichana wa chuo kikuu. Niliwatelekeza kwa sababu nilihofia kuwa ndoa yangu ingeingia doa. Leo hii majaliwa yamenikejeli kwa kuniletea mwana huyu nyumbani kwangu. Jimmy Kariga njoo, wewe u mwanangu. Saida mama yako alikuwa rafiki yangu japo nilimtenda unyama. Nilimwachisha masomo kwa tamaa. Nisamehe mwanangu. Nimeipokea fimbo ya ulimwengu nikahisi uchungu wake.” Mbalu alisema haya akimpiga Jimmy pambaja. Watu wakashangaa, Doreen akashangaa zaidi. Kumbe damu huvutana ati! Alimpenda sana Jimmy. Alihakikisha amempitia kila siku pale kibandani akamsalimia roho nayo ikampoa. Mpaka ni hili penzi Jimmy alihisi pia ila hakulielewa vyema. Wana bahati watoto hawa hawakuvunja miiko kwa kutojua. Baba yao angeishi kujilaumu.

Mercy alifurahi amepata fidia ya Dan kwa sura ya Jimmy kinyume na ilivyotarajiwa. Alimwangalia akapendezwa naye. Kanini hapo hangezuia bomu la hisia kufuani. Aliwachukua Mercy na Mbalu chemba wakasema ya kusemwa.

Safari ya Makesi ikang’oa nanga, lakini bila Kanini. Mpaka angekuwa na neno na dada yake Dharura. Alipotoka Tunu alimwacha akiwa na miaka saba hivi mikononi mwa bibi yao mkongwe. Mama yao

alikuwa ashaiaga dunia miaka miwili iliyotangulia kwa lile shambulizi la wanakijiji. Mapenzi ya yule daktari wa hospitali ya Kalawa na ahadi za kimbinguni zilimpofusha akatoroka nyumbani. Hata hakuja kumzika bibi alipofariki.

Hawa dada wawili walikuwa na mengi ya kusuluhisha. Dharura alifurahi sana kumpata dada yake tena baada ya miaka mingi. Alimchukua kwake nyumbani na kumkaribisha vyema. Wakasimuliana adha za maisha mara walilia mara wakacheka kulingana na hisia za simulizi. Joto la kindugu likarejea.

Dharura hapati nafasi ya kupumua kutokana na majukumu yake mapya. Watu walijenga imani naye hata wakamsahau Mwema ambaye sasa alitumikia kifungo cha miaka kadhaa. Sintofahamu iliyoikumba kanisa kwa muda haikuwa tena. Baada ya uchaguzi wa viongozi wapya kila mmoja alishika wadhifa wake barabara. Kila tawi lilipewa kasisi msaidizi. Kina Kalatu, Mbalu na familia yake, na pia Kenga sasa walikuwa wakisoma dini kabla ya ubatizo.

Kwa ushirikiano na shehe Musa, Dharura alifanikiwa kuunda muungano wa wahubiri wa dini zote katika Pemba. Chini ya uongozi wa Musa kama mwenyekiti wamefanikiwa kupigana na uhuni maabadini. Aidha, waliandaa semina mara mbili kwa mwaka kutilia nguvu uwianao na mshikamano wa kidini. Itikadi kali dhidi ya imani moja dhidi au nyingine hazikuwa na nafasi. Njama nyingi za kigaidi ziliweza kutibuliwa na viongozi hawa pamwe na vitengo husika vya usalama. Kundi hili limevutia wafadhili mbalimbali katika sekta ya elimu na biashara. Uwezo wa kiuchumi wa kina mama wengi umeinuka kwa mikopo nafuu waliyopokea. Wafadhili hawa wamewasomesha watoto kutoka familia maskini bila kuzingatia dini.

Kina mama walianzisha mradi wa kutengeneza vikapu, mikufu na bangili walivyouza ng'ambo kwa msaada wa hawa wafadhili. Fedha walizopata zilikidhi baadhi ya mahitaji yao muhimu kama vile chakula na mavazi.

Dharura aliteuliwa katika bodi ya hazina ya maeneo bunge. Kwendako mema hurudi mema. Nafasi yake hii ilimtangamanisha na viongozi wengi akiwemo gavana wa Pemba. Hakukosa mikutano mikubwa ya maendeleo ya kaunti. Kiuchumi ameinuka, amefanikiwa kujenga nyumba nzuri na kumwachia mwanawe ile waliyokuwa wakiishi. Ila aliazimia kutokibomoa kile kibanda cha awali. Alikiweka kiwe kumbukumbu la alipotoka. Hata vyombo vyake duni alivyotumia vilikuwa katika makabadhi haya!

Nafuu binti yake ni mwalimu wa Kiswahili na Jiografia katika shule ya upili ya Vibonge baada ya kuhitimu masomo ya viwango vyote. Urafiki wa mwalimu huyu na mbunge wake ulizaa penzi. Nafuu aliuona

urafiki wake na Karani kama ule wa kawaida tu ila Karani aliona penzi. Waliachana sana kwa umri jambo alililoliwazia sana Karani. Lakini hangempa msichana mwengine nafasi aliyompa Nafuu moyoni. Alikuwa kwake rafiki na msiri wake mkubwa. Alipofunga macho mbunge huyu alimwona Nafuu. Hili halingekuwa jingine ila penzi. Nafasi yake kama mbunge ilimtagusanisha na vidosho wengi wenye sura, umbo, pesa na vyeo. Wapo waliojileta kwake na kijipendekeza.

Jamila alikuwa karani wa *Benchmark Motors*, kampuni kubwa ya kuuza magari Takuja. Walipatana alipokuwa akinunua gari lake la kwanza. Jamila alikuwa mfano aula wa urembo; kisura na kimavazi. Kwa hakika hakuwa na la kitiliwa dosari. Kifupi alikuwa hazina ya uzuri na urembo. Walizungumza na kuongea mengi. Walienda burudani za nyimbo na video pamoja. Mara si moja alimwambia Karani alivyompenda. Karani naye akajifanya mjinga wa mapenzi na mahaba. Kila kulipokucha hangekosa arafa ya kumjulia hali na kumtakia heri ya siku kutoka kwake Jamila.

Siku moja Karani akiwa ofisini kwake kulibishwa mlangoni na sekretari wake, akamkabidhi bokisi kubwa iliyodaiwa kuletwa na taarishi. Kufungua lile bokisi mlikuwa na shada kubwa la maua na chupa ya divai. Karani alijua mtu mmoja tu ambaye angefanya hivyo baada ya Dan kuaga dunia. Jamila. Alikumbuka katika sherehe ya kuzaliwa kwake siku moja. Dan alimletea fungu la sukumawiki kama zawadi. Watu walioalikwa walipasua vicheko. Naye akachukua lile fungu na kuanza kumchapa Dan kwalo na mwengine ambaye angecheka. Katika harakati hizi, lile fungu likafunguka. Loh! Hundi ya shilingi elfu tano ikaanguka.

Karani aliamua kutomdanganya huyu msichana asiye na hatia. Alistahili heshima. Si wote hupendwa ati! Laiti angehisi nusu ya alivyohisi Jamila ingekuwa nafuu. Alimwalika chajio kwa hoteli moja ya kifahari pale mjini. Wakala, wakanywa na kuogelea. Utani wao mwingi ulileta mwonekano wa wachumba waliopendana karibu kufunga akidi.

‘‘Jamila umekuwa zaidi ya rafiki, umenifanya nikajua mapenzi ni muhimu. Nimeishi kuogopa urafiki wa jinsia ya kike kutokana mila na desturi za kwetu. Sasa najua mwanamume anaweza kuwa na rafiki wa dhati wa kike wakaishi kwa heshima kama marafiki. Najua unanipenda kwa kila tone la damu yako. Nami nimejaribu kuchunguza hisia zangu. Sitakundanganya Jamila, sitaki nikutumie visivyo. Naomba unisamehe

kwa kuchelewa kupenda. Sijui nitapenda lini.'' Karani alimweleza Jamila kwa upole.

"Nakuelewa sana Karani. Kupata mwungwana sampuli yako ni muhali. Umezungumza yatokayo moyoni. Inauma sikuweza kuingia moyoni mwako kama mpenzi, hata hivyo ninayo hakika nimo kama rafiki mkuu. Nitaridhika kwa hilo. Ila nakuomba jambo moja, kwamba ukijaliwa kupenda unipende, usiponipenda vilevile huna deni.'' Jamila alisema yale akifuta chozi. Chozi la penzi.

Karani alinga'ng'ana licha ya msimamo dhabiti wa Nafuu kuwa hangekubali uhusiano wa kimapenzi naye. Hakuzaliwa wa kufa moyo. Akatumia mbinu nyingi kumshawishi na kila mara aliambulia patupu. Alibakisha moja. Hii ikishindwa basi atasalimu amri.

Jioni moja alimwendea Dharura pale kanisani kwenye ofisi yake nia ikiwa moja. Kumwomba msaada katika kumrai Nafuu kuukubali mkono wake. Hakuwa na hakika kama angekubali ombi hilo. ''Karibu mheshimiwa, inaoneka ukubwa haukuingii, wawezaje kuja kwangu ghafla bila taarifa?'' Dharura alianza maongezi. ''Inaonekana pia mama amesahau kuwa mtoto hahitaji taarifa kuja kwa mama yake.'' ''Basi kama ni salamu itakuwa heri nyumbani ndio nilikuwa karibu kufunga.'' ''La, sikutaka kuja nyumbani, nilitaka nikupate hapa. Nina haja na usaidizi wako. Unavyojua huu ni muhula wangu wa pili bungeni. Miaka inasonga, nahitaji kukaa nitulie kama mwanamume; nahitaji jiko.'' ''Sasa hapo Dharura ataingilia wapi? Ama kuna mmoja wa waumini wangu amemkosesha mheshimiwa usingizi? Kama yupo tumia ulimi, mnyanyase kabisa kwa matamu ya mapenzi mpaka ainue mikono. Kazi yangu ni kubarikisha tu.'' Dharura alitania na wote wakacheka. ''Ni Nafuu, binti yako ni mgumu ajabu, naomba umshawishi tu anipe nafasi, sitamshurutisha kupenda. Labda muda wake wa kupenda bado. Niko radhi kumsubiri.'' Karani alisema.

Habari hii ilimpa Dharura kiwewe. Akaanza kujiona mpweke mapema. Bila uwepo wa Nafuu ataishije? Hakujaliwa kuwa na mtoto mwengine. Alikuwa ameamua kutoolewa baada ya ndoa yake na Mbaara kuingia doa. Alijona sasa kama aliyejifunga na kujikwaza. Aliyejitia ngomeni. Kila uamuzi kama sime hukata kuwili. Mbaara amefika kwake mara nne sasa akitaka msamaha lakini hangeamini msamaha wa mtu aliyelewa chakari. Huo ni msamaha wa kilevi; msamaha uliolewa. Nafuu

siku hizi pia hampi amani. Siku chache baada ya mazishi ya Dan, alimwambia mama kuwa japo alihubiri vyema hakuona mshabaha wa mahubiri na mhubiri. Alishangaa ni vipi alivyohimiza kuhusu msamaha katika familia ilhali yake mwenyewe imevunjwa kwa kukosa huo msamaha. Pia alidai kuwa baba yake alilewa kwa sababu ya mawazo ya kuharibikiwa na maisha. Dharura alipoyachunguza maneno haya yalimgeukia mwiba uliomdunga kila mara. Kama mwanawe aliona vile, na watu wengine je? Mpaka angefanya kitu.

***

Doreen na mama yake siku hizi ni kama mtu na dada yake. Bibi kule pwani alimdata sana binti huyu, alisikia msukumo mkubwa wa kumwona mtoto aliyelea kutoka umri mdogo, alitumana aende akamsalimu. Bibi huyu alikuwa katika umri mpevu hivyo matembezi yalikuwa kwa shida. Aila ya Mbalu ikafunga safari kwenda pwani. Waliunganisha kumtembelea bibi na zaira ya wiki moja kule. Wangetembea mahali mbalimbali kuvinjari na kupata muda mwafaka wa kufurahia kuzaliwa kwa pili kwa familia hii. Mbalu alikuwa mwenye furaha pia kwa sababu ni siku akali tangu amwone mnuna wake. Maisha yaliwatenganisha ndugu hawa. Chumo alikuwa mwanabiashara aliyeshughulika na kuagiza bidhaa kutoka Uchina na kuviuza humu nchi kwa bei ya jumla. Alianza kwa biashara kwa kuchuuza bidhaa za rejareja kama vile: vitana, vikombe vya plastiki, saa za mkononi na vinginevyo. Hakuwa mwerevu shuleni kama Mbalu. Alipofanya mtihani wake wa kidato cha nne alipata alama ya D. Mbalu aliyekuwa chuo kikuu wakati huo aliufanya mwao kumkejeli. ‘‘Eti Chumo ulipata nini vile?’’ Angeanza kiutani. ‘‘Acha masihara kaka. Nitashinda siku zote nakwambia.’’ Chumo angesema akilenga mkondo huo wa mazungumzo. *“D for darling…D for darling…No no no! For David.’’MY DEAR DAVID HAS A DARLING DOG!!’’* Mbalu alimtania kaka yake aliyeonekana kutoudhika. “Kaka, baraka ni kama mmea, kila mmea una udongo wake unaposhamiri. Baraka yangu itapata udongo mzuri siku moja. D unayoidharau nitaifanya Dola!”

Siku hizi Chumo ni jina kubwa pwani yote. Barabarani humo, ukihesabu malori ya mashehena matatu, la nne nila Chumo. Maduka yake ya jumla hayana hesabu. Mara nyingi jamaa huyu huwa nje ya nchi kwa shughuli zake za kibiashara. Katika mazishi ya mpwa wake alitua pale Tunu kwa ndege.

Mbalu alifurahi kaka yake alikuwa nchini wakati ule. Wangepata nafasi ya mtu na ndugu yake. Doreen alipania kuwaona binamu zake. Alikuwa pia amepanga kupitia Takuja kwa reli mpya ya kisasa iliyounganisha Takuja na pwani ya nchi. Alitaka kumwona Jimmy na wengineo. Njiani walizungumza mengi, wakakumbushana mengi.

Bibi alifurahi kumwona Mbalu na familia yake. ‘‘Nashukuru mungu kukuona Doreen damu yangu. Nilihofia ningeaga sijakutemea mate. Nilikulea kama simba; kutoogopa maisha, kuliandama ulilolitia akilini, kufuata moyo wako. Naam, u kama mwamba unaokejeli dhoruba. Kwako nina mwana. Uwe na kheri mwana, ukitoka na kurudi. Baraka ziwe kwako kama kivuli sizikuache kamwe, za shambani na mjini, za mifugo na za mashamba. Mkono wako na uwe sumaku hata vya mbali unase. Ukishika sumu iwe dawa mujarabu ikuondolee madhila wakusudiayo mahasimu wako. Sumu nayo ikawarudie wenyewe ikiwa hatari kuliko awali. Ulimi wako nao na uwe hirizi iwaungao watu pamoja. Uwe macho ya ndugu zako, uwatoe kiwi. Kwende mema mwanangu kwende mema kwako.’’ Bibi alimalizia baraka zake akamtemea mate kifuani. Naye Doreen alikuwa akisema kila baada ya tamko bibi “Ngaiyai’’ ama amina kwa lugha yake ya mama. Familia ya Chumo pia ilipata mgao wake wa baraka hizi.

Nani angejua ile ndiyo ingekuwa buriani. Chumo alikuwa amemchinja mbuzi. Siku hii mkewe alikuwa ameandaa pilau maridhawa. Wakala, wakanywa, wakafurahia. Hewa ya pale ilinukia furaha ya kindugu. Baada ya chajio bibi aliomba kuruhusiwa kulala mapema. Hali ile iliwashangaza wote kwani siku zote alikuwa wa mwisho kwenda kitandani. Kabla ya kulala, angeshika kitabu chake cha maombi pamoja na rosari yake yenye punje kubwakubwa na kusali kwa sauti. Baadaye angeamka polepole akiimba wimbo aliopenda akielekea chumbani mwake, *‘Njuu moyo muturia nthi muuo…’*

Bibi siku hizi hulala mapema hivi? Haombi?’’ alisaili Doreen. ‘‘Ni machovu ya kusumbuana nanyi tangu mje. Tena huoni siku zimekwenda, pumziko kubwa li karibu. Usiku mwema wanangu.

Mercy na mkewe Chumo walibaki sebuleni. Watoto wakatoka nje kulikokuwa na uwanja wa voliboli na kando ya mbwawa. Waliweka viti muduara. Stori nazo zikanoga. Mara walicheka, mara walikurupushana, mara walirushana majini muradi kila dakika ilikuwa na kadhia yake.

Mbalu na kaka yake nao walikaa roshani mahali walipowaangalia watoto hawa kutoka juu. Divai ikapata shida pale. Keshoye hakuna aliyekuwa anataka kutoka kitandani kutokana na machovu na mavune ya jana. Siku hii walikuwa wamepanga kwenda Bahari Hindi kuogelea. Walijipanga timu mbili kwa mashindano. Team Chumo na Team Mbalu.

Mkewe chumo ndiye aliyekuwa wa kwanza kujinasua kutoka kwa gundi ya usingizi mnamo saa moja unusu. Alimuamsha Mercy wakaandaa kiamshakinywa. Walikiandika mezani. Kila mtu alikuwa ameamka sasa isipokuwa bibi. ‘‘*Eh guys*, karibuni, kila mtu ajipakulie sawasawa na njaa yake.’’ Mkewe Chumo alitangaza.

‘‘Mama yuko wapi, bado kitandani?’’ Chumo aliuliza huku akijititilia chai. “Mama nao na vitindamimba wacha tu.’’ Mbalu alidakia. Wote wakaangua kicheko. Mmoja wa wana wa Chumo alienda kumwamsha. Alibisha asifunguliwe, akaita asiitikwe. Alirudi kumweleza baba aliyeonyesha kushangaa. Akanyanyuka akaelekea chumbani kwa mama yake. Hofu ilitanda pale ghafla. Walihofia walichokifikiria. Hatimaye walivunja mlango wa chumba kile. Ukweli mchungu ukadhihirika. Wakaomboleza wakamzika pale kwa Chumo kama yalivyokuwa mapenzi yake kwa sherehe kubwa.

# Sura ya Nane

Juhudi za mtu ndizo humtofautisha kimapato. Juhudi zinaweza kuwa halali au zenye hila. Wapo walioziandama zile mbaya wakajipata pabaya. Wapo walioanza vyema lakini walivyoendelea, labda kwa kukosa subira wakajichanganya. Pema napo usipopema si wajua si pema tena? Ulifanyalo lifanye vyema ila bila dua hutafanikiwa. Usiyaangalie maendeleo ya mwenzio yakakuzuzua. Thamini kinachotia sahani mezani pako. Dumu kwa moyo wa shukrani. Kilichoamriwa kitakuwa chako. Muradi tu ujiweke kama mtu kitakujia.

Jimmy alijikaza pale kibandani. Kanini sasa aliacha kazi ya udobi akaja kumsaidia kuwahudumia wateja ambao waliokuwa kama nyuki kwenye maua. Ijapokuwa ana amani kwa kujua usuli wake wa kikwasi, haonekani kuwa tofauti na alivyokuwa awali. Halulegeza juhudi zake. Japo alipewa ahadi nyingi na baba, aliziacha ziwe ahadi tu. Akakumbuka maneno ya mama yake katika ndoto, ‘‘Mwanangu dunia ni mpira wa soka…hauna hiari unakoelekezwa na majaliwa…’’ Akaamua kusubiri majaliwa.

‘‘Watu wangu msalama?’’ Sauti ilitikoka miongoni mwa wateja. Sauti isiyo ngeni pale. Watu wakaelekeza maonzi kulikotoka sauti. ‘‘Meimes!’’ Watu walifurahi kumwona tena. Pale pakageuka jukwaa la makaribisho. Jimmy na dada mtu wakavaana wazimawazima, joto la kindugu likasambaa. Kanini alifurahia kumwona mtu aliyemwenzi sana. Yeye pia alifurahia kurudi Makesi japo alijua pale patamkosa. Japo alitamani kukaa pale penye watu karimu na wenye utu, alijua usalama wake sasa ulikuwa hatarini. Tena ashakuwa ‘mvulana’ wa Mbalu kama ilivyokuwa mila pale hapakuwa na mtoto wa kiume. Hili lilikuwa jukumu kubwa na halingefanywa kwa mbali. Alifululiza hadi kwake. Kuingia tu, mlango ulibishwa, alikuwa Jossy aliyetumwa na mama amsaidie usafi pale kwake. Baada ya shughuli za ndani pale alienda kwa Kanini. Aliwaeleza wote kuhusiana na nia yake ya kuhamia bara. Hawakuchukulia wazo hili kwa urahisi. Jimmy alibisha na kupinga sana uamuzi wa dada yake. Ungemwona mshipa ilivyojichora usoni kwa hamaki. ‘‘Tulia kaka yangu, wazazi wanahitaji sasa wa kukaa nao. Kovu la kufiwa na mwana bado lipo. Sio kwamba nawatoroka. La, naumia kutengana nanyi pia. Jimmy wewe ni ndugu yangu wa pekee. Nakuhitaji uwajibike kama kaka. Baba anakuhitaji umwondolee aibu, mpe upenyu

wa kujirekebisha. Jiaminishe kwake. Mama nawe baba ameniambia kuwa bado anakumbuka yote mliyoafikiana.'' Baada ya mazungumzo hayo Meimes alirejea kwake.

Jiani aliwapita vijana katika vikundi kama ilivyokuwa desturi. Waliomjua walimrushia maneno. *''Wewe mrembo unando nini huku? Mtoi wa mdosi kubangaiza ngetto. Acha kutuenjoy, izo doh tutakamia tuomoke pia.''* Maneno hayo yalimshangaza kuliko yalivyomshtusha. Alikumbuka siku za kwanzakwanza pale mtaani Makesi. Alitoka jioni moja saa kumi na mbili unusu hivi kununua mboga. Pale jiani aliwapata vijana wawili wavulana. Walipomwona, mmoja akapunguza hatua zake na yule mwengine akaendelea. Meimes alipoingia kati yao, yule aliyekuwa mbele akapinduka kutazamana naye na kumwendea, Meimes akasimama kumkabili. Aliyekuwa nyuma akampiga kabari huku amemfunga mdomo. Alijaribu kujifurukuta asiweze. ''Tulia mrembo tukupe mahaba ya mjini.'' Mosquito alisema huku wakimsukuma pembezoni kwenye giza. Kwa bahati nzuri ndio Jimmy alikuwa anarejea nyumbani kutoka vibaruani. ''Wewe Mosquito acha ujinga, mnamfanyia nini msichana wa wenyewe?'' Jimmy aliwafokea, akamfikia mmoja wao na kumkandika ngumi. Mara wakamwachilia na kuchana mbuga. Hivyo ndivyo mtu na kaka yake walivyokutana.

Meimes kwa kumbukumbu hizi aliharakisha hatua, nusu kutembea nusu kukimbia huku akiyatunga macho nyuma kila baada ya dakika chache. Alihofu vile hawa vijana wanaweza kumfanyia wakijua kama wanayojua sasa. Watu wengi wamefariki mikononi mwa watu kama Mosquito, wanawake wakafanyiwa yasiyosemeka na wengine wakaishia na mimba; alama isiyofutika ya dhuluma. Si ajabu katika Makesi kukutana na vijusi vilivyotupwa kandokando ya barabara na kila mtu akapita hamsini zake kama aliyeona mzoga wa mbwa. Siku ya kwanza ya Meimes kuona haya hakupata usingizi kwa siku mbili mfululizo. Aliota watoto wengi wadogo waliokuwa na mabawa kama malaika wakimzunguka wakimwaita mama. Haukupita muda mrefu kabla ya kuzoea haya kama wengine. Hapa Makesi, nywila ya maisha mazuri ni kulichagua na kuliandama linalokuhusu. La sivyo ungekuwa kwa kesi moja au nyingine. Labda ni kutokana na hili mtaa huu ukaitwa Makesi. Alikuja kuyaelewa maneno ya Kanini ya siku moja. ''Binti yangu, maisha ya Makesi si maisha. Wanaoishi humu ni wakataliwa wa mitaa mingine ya Takuja na nchi nzima. Utapata uhaini kwa vipimo vikubwavikubwa.

Ushawishi wa kwenda tenge ni mkubwa ajabu. Inachukua moyo mkuu kudumisha utu wako kwani utakayoyaona humu ni ya kuumbua. Ila sisi tuliojipata humu sharti tuishi. Titi la nyati huamwa kwa tahadhari mwanangu. Ukijua hili utaishi vyema hapa."

Kwake Meimes alikuwa na mengi ya kujivunia mtaa huu. Hapa ndipo alipopaita nyumbani ilipomkataa. Makesi kilikuwa kiziwa cha uhuru. Kuishi kwake huku kulimpa nafasi ya kuwa yeye. Hapa ndipo alipoamua kufanyizia kazi ujuzi aliopewa na bibi yake. Alijiona kama aliyeiita nafsi yake kutoka ilikojificha moyoni mwake ije imuhidumie. Akazalika upya! Makesi imekuwa shule bila karo. Amejua ukabila ni mpango wa Mungu tu wa kusawiri tajriba yake ya uumbaji kujitafutia sifa miongoni mwa binadamu. Mwanadamu lakini ameutumia kuwa msingi wa kubagulia. Tena ukabila haumo miongoni mwa maskini ila mwa matajiri na viongozi wa kisiasa. Ukabila ni mbinu ya wanasiasa na matajiri kuhujumu umoja na mshikamano wa jamii kwa manufaa yao binafsi. Hawa wamehitimu katika taaluma ya uongo na propaganda zinazokoroga akili za maskini. Makesi kulikuwa na watu wa makabila mengi na hungesikia wanazozana isipokuwa wakati mwanasiasa alipopita pale na kuwafukizia ukabila. Hebu wewe fikiria ulimwengu wa kabila moja na tamaduni moja. Ungekuwa unasinya kama kinyaa.

Mungu alituumbia uhitaji ili tuthaminiane. Mwanamume akanyimwa alichopewa mwanamke ili daima amhitaji kuimbe huyu. Mwanamke vilevile aishi kumhitaji mwanamume kwa kile alichonacho. Wakaumbwa warefu wavifikie vilivyo juu na wafupi wavichukue vya mvunguni. Wakaumbwa walemavu ili walio kamili wawe na shukrani kwa Mungu kwa uzima wao. Si kwamba walemavu wana kasoro, la, wamekamilika kwa njia spesheli aliyoipenda na kuikusudia Mungu. Mmoja akapewa kiti na mwengine kumbi. Mwengine tajiri, jirani yake maskini. Si kwamba maskini hana juhudi ni majaliwa. Tuko tulivyo si kwa ufaafu ama kutofaa kwetu, hiyo ndiyo nafasi tuliyoratibiwa. Tuishi kwa shukrani.

Meimes alikuwa amesoma kuchelewesha hukumu. Uchungu mwingi tunaoishi nao ni kwa sababu ya kuhukumiwa pasipo haki. Hukumu ikikalia kiti cha upendo, matokeo yake ni uhasama. Hajuti kabisa kuishi hapa Makesi. Amepata kito asichoweza kukibadili kwa fedha. Sasa hana budi kuhama pale. Lisilo budi hubidi. Ukijukumiwa nawe jukumika. Alikuwa na jukumu nyumbani.

***

Kama maji yanavyofuata mkondo wake, ndivyo maisha pia husonga. Changamoto, sintontofahamu na sintokujua huwa vituo vya maisha tu si vikomo. Maisha husonga tu. Mwenda ana miaka minne alipoifungua ofisi yake pale Tunu. Amejulikana sasa kwa uchoraji wa plani za nyumba Pemba nzima. Dharura amefaidi ujuzi wa kijana huyu na kumpendekeza kwa mkuu wa Pemba. Lakini hata baada ya kuwa na kazi nzuri na kipato cha haja mama yake bado hakuridhika. ‘‘Ana nini huyu mtoto, hatuletei mgeni hata tukamkataa? Ama mawazo yake yako kwa Doreen. Mmh. Ona mwandani wake hivi karibu anafunga ndoa na binti ya Dharura.’’ Jane mama yake alilalamika. ‘‘Tumwachie nafasi, labda hajapata wa kumpendeza. Tena wakati huu si kama wetu wa kuposewa. Mwenda ni mwanaume mwenye kipato. Tukimharakisha huenda akaangukia mitego ya wanaotaka kumpuja hela zake bila mapenzi.’’ Mwenge alisema haya huku mawazo yakimsafirisha enzi hizo alipomwoa mkewe. Akakumbuka hakumpenda. Alilazimishwa na wazazi wake waliopania kutia muhuri urafiki wao na familia ya akina Jane. Kilichomshangaza ni vile alivyokuja kumpenda kiumbe huyu baada ya ndoa. ‘‘Sawa daktari wa mapenzi, tunajua ulivyokuwa unanipenda. Kama si kujiweka na chakula changu kitamu ungekuwa ulinitaliki kitambo.’’ Jane alimtania mwenzake aliyekuwa katika fikra zizo hizo.

Kilichokuwa muhimu kwa Mwenda wakati ule ni kazi yake tu. Wakati mwingine alikuwa ofisini au nyanjani. Alikuwa amemwajiri katibu aliyemsaidia shughuli nyingine pale ofisini. Kusema kweli, mapito ya muda hayakumfikirisha sana kijana huyu. Alipoliwazia swala la ndoa ni wakati mheshimiwa Karani alipompitia pale ofisini kumpa mwaliko wa harusi. Aliona wasiwasi kuwa hajapata kuhisi chochote kwa msichana yeyote isipokuwa Doreen tu. Uhusiano wao ulikuwa umewafanya wenyeji wa jehanamu kwa siku nyingi. Siku baada ya mazishi ya Dan walipatana wakasalimiana, wakabaki kuangaliana tu. Macho yakaachiwa nafasi ya mdomo. Hisia sampuli ya umeme hafifu zilipitia mwilini wa kila mmoja japo kila mtu alifanikiwa kujidhibiti. Walipigana pambaja na kuachana kila mmoja akihisi kama aliyezungumza na mwenzake yote kwa mapana na marefu. Habari za Doreen kurudi bara zilimpa amani fulani. Hakupenda kufikiria kutoka hapo. Aliivamia kazi na mawazo yakampa nafasi.

Kuna huu mradi haumpi usingizi. Amepewa kazi ya kuchora plani ya hospitali ya kisasa na serikali ya kaunti. Hii ni baada ya kushida zabuni iliyokuwa na ushindani mkali. Hospitali yenyewe ilikuwa iwe na: sadaruki ya vitanda mia tatu, vyumba vinne vya uyoka wadi mbili kubwa za karatini, makafani ya kisasa ya kuhifadhi miili mia tatu hamsini hivi sehemu ya kushughulikia wagonjwa wa saratani vyumba kumi na vitatu vya kushughulikia wangonjwa wa kawaida na wanaokuja kliniki mbalimbali. Aidha, kulikuwa kuwe na ofisi kama saba hivi. Mwenda alihitajika kutumia nafasi aliyopewa vizuri ili kuacha nafasi ya kutosha ya maegesho na kupita kwa urahisi kutoka kitengo kimoja hadi kingine. Hajapata kazi kubwa hivyo tena tangu aanze taaluma yake hii. Alichora akafuta, akachora tena akafuta. Katika harakati hizi akamkumbuka rafiki yake wa chuoni. Akamtafuta amsaindie kwa mkataba ya kumpa asilimia kumi na tano ya pato baada ya kazi. Baada ya siku kadhaa alikuwa ashamaliza kazi. Alingojea siku tu ya uwasilishaji. Baada ya saa tatu za uwasilishaji, Mwenda aliwaridhisha washikadau. Alikuwa amejiahidi gari jipya baada ya kazi hii na kabla ya harusi ya Karani.

***

Dharura alifikiria kuhusu harusi ya mwanawe Nafuu. Kinyozi kwa kawaida hajinyoi. Alihitaji kasisi wa kufungisha ndoa hii. Yuko katika harakati za kurudiana na Mbalu ila amekataa juhudi za Nafuu za kutaka warudiane kabla ya harusi. ‘‘Huna mamlaka ya kutuharakisha sisi wazazi wako ama utatuvunjia heshima mtoto. Tuache. Cha muhimu ni wewe na Karani muanze maisha yenu.’’ Alimkemea mwanawe siku moja alipoona amezidi.

Mbaara na Dharura walihitaji muda. Kutengana kwa miaka hiyo yote si jambo dogo la kupaparikiwa. Mbaara haonekani tena malevini. Ni safi pia kuliko awali. Kule kuwa bavyaa wa mheshimiwa kumemtuma kubadilika pamoja na kule kurejea kwa Dharura maishani mwake. Alianza kuwajibikia tabia na mienendo yake. Nafasi hii ya kuyafinyanga tena maisha yake na kuyaunda upya hakuwa tayari imponyoke.

Ameduduiza hela kidogo anazopata kwa wanawe mpaka akaikarabati nyumba yake. Sasa ina viti vinne vya plastiki na meza moja. Bidhaa nadra katika nyumba hii. Ana mbuzi na kuku kadhaa wanaomtia shughulini kila uchao. Alionekana siku hizi shambani akilima, akisesa, kupogoa au akitengeneza ua. Katika mwanga huu uliomngaa aliona

alivyomkosea Dharura na mwanawe wa kipekee. Alivyojinyima hata nafasi ya kupata mtoto mwengine. Kweli hutambui umuhimu wa ulichonacho mpaka kinapokuponyoka. Pindi tu mkewe alipomtoroka maisha yalimwia magumu. Upweke nao ukawa mwandani wake. Akaishia kuongeza vipimo vya ile misokoto na vileo vingine na bila kujua akawa mfano mwema kwa walevi. Watu waliomjua walimsimanga, ‘‘Aliyekuroga kama bado yu hai mtafute. Yumkini mwanamume mwenye akili zake angemfukuzaje mwanamke mrembo na mwenye bidii kama Dharura?’’

Hakuhitaji kuambiwa hayo kwani aliyajua. Sasa alihisi kama asiye na haki ya kuitwa baba ya Nafuu. Hajakuwa wa mchango mwingine kwake isipokuwa wa kumzaa. Haidhuru. Muradi amepata nafasi atajikosoa. Mui huwa mwema ati!

Dharura aghalabu alipita kwa Mbaara akielekea nyumbani akamjulia hali. Walikuwa na mengi ya kuongea na kupanga. Harusi ya mwanawe ilikuwa chini ya mwezi mmoja. Kama ilivyokuwa tamaduni, wazazi wa Karani wangekuja kwa akina Nafuu kurasmisha posa. Wangeleta ‘kondoo wa shemeji’. Pale wazazi na msichana pamwe na wamwe na wazee wa mlango huo wangetaja kiwango cha mahari. Hii ni sherehe muhimu; siku ya mashemeji. Palihitajika mipango mahususi yenye makusudi ili kutodharaulika. Karani alishaleta ‘*Nchoolo’* -fungu la matawi ya mmea maalumu wa kitamaduni yaliyotafunwa na wazee wa jamii ya sehemu hii-kwa wazazi wa Nafuu na ikakubaliwa.

Siku hiyo Mbaara aliwaita wazee wa mlango ili kupanga mikakati ya jinsi sherehe itakavyoendeshwa. Dharura pia alikuwa katika kikao hiki muhimu.

Ilikuwa katika mkutano huu habari za kushtusha zilipofika. Ulimwengu mzima ulikuwa katika mshtuko huu. Ugonjwa sugu ulikuwa umezuka kule Uchina. Ugonjwa usiojulikana na uliosambaa kwa kasi ya ajabu. Dalili za ugonjwa huu zilikuwa pamoja na kuumwa na kichwa, kuenda chafya, kukohoa, joto jingi na kushindwa kupumua. Cha kushangaza zaidi ni uwezo wake wa kuua upesi. Ilishukiwa kwamba ugonjwa huu ulisambazwa kwa mate unapokoa ama kwenda chafya. Virusi katika mate vilingilia katika sehemu laini za mwili kama pua au macho. Kufuatia hili serikali za dunia ziliagiza raia wake kuvaa barakoa kufunika mdomo na pua. Aidha virusi hivi vilikuwa na uwezo wa kukaa

sakafuni, kwenye viti, komeo za milango na kadhalika kwa muda, hivyo mtu alipogusa sehemu hizi alibeba virusi kwa mikono yake. Watu walihimizwa kunawa mikono kila wakati kwa maji yatiririkayo na sabuni. Vilevile walihimizwa watumia vieuzi kueua mikono yao pasipo na maji ya kunawia.

‘‘Ulimwengu umekwisha!’’ Mzee Kenga alivunja kimya kilichokuwa kimetandanda pale kikaoni ili kusikiliza redio. Kenga hangeacha redio yake hii popote alipokwenda. Kutokana na hili, aliweza kuwa wa kwanza kupata matukio mengi ya ndani na nje ya nchi kuwapiku wazee wengine wa rika lake. Wakati huu alikuwa makini kufuatilia siasa za Marekani na ushindani kati ya rais Donald Trumph na mpinzani wake wa karibu Joe Biden. Akiwa njiani kuja hapa vilevile amepata habari ya vile mto Nile ulivyovunja kingo zake na kuathiri Sudan kusini pakubwa. Jambo hili, kulinga na taarifa lilikuwa limetendeka tena miaka mia moja iliyopita! “Uchina iko bara Asia, ugonjwa huu utatufikiaje Afrika. Acheni jakamoyo za bure.” Mzee mmoja alidakia. ‘‘Tena mbona kipindupindu na ebola na magonjwa mengine hayawafikii wachina kutoka Afrika?’’ Alizidi kupuuza. ‘‘Historia, mwenzangu historia! Dunia imewahi kukumbwa na mikurupuko mingi ya tandavu. Kwa mfano, mwaka wa mia moja sitini na tano kabla ya Kristu, kulizuka ugonjwa wa ndui uliowangamiza zaidi ya watu milioni tano kote ulimwenguni. Mnamo mwaka wa elfu moja mia tatu na arobaini kukazuka ugonjwa uliotokana na viroboto wa wanyama wagugunao, ukaitwa *Black Death* kule Ulaya.Takriban nusu ya watu barani humo walitangulia mbele za haki. Ugonjwa huu huu ulizuka tena kati ya mwaka wa elfu moja mia sita sitini na sita na kuua halaiki. Hii ni mifano tu ya mikurupuko ya tandavu iliyowahi kuikumba dunia. Sikukutajia uwele wa polio unaozidi kutukejeli tangu miaka ya elfu moja kenda mia kumi na sita hapo. Ama homa ya nguruwe ya juzijuzi tu mwaka wa kati ya elfu mbili na tisa na elfu mbili na kumi. Juzi tu mmesikia kuhusu zika. Ungojwa ulioangamiza mimba nyingi kule marekani na kwingineko.’’ Kenga aliwanywesha wazee wenzake kikombe baada ya kingine cha historia. Wepesi wake wa kumbukumbu uliwashangaza wengi wa rika lake ambao hata hawakumbuki walipozaliwa acha majina ya watoto wao wote. Miongoni mwa hawa ni Nguku, mganga maarufu na daktari mstaafu wa kienyeji aliyekuwa na wanawake thelathini na sita na watoto yamkini mia mbili na kumi. Aliwajengea wake zake nyumba zilizofanana katika shamba lake la ekari

themanini. Watoto walijengewa majumba kama mabweni. Kilichoshangaza ni jinsi umati huu ulivyoishi kwa amani. Hungejua ni mtoto yupi alikuwa wa mama yupi. Pale hakukuwa na kitu cha mtu binafsi. Ulikuwa mfumo kamili wa ujamaa. Kutokana na taaluma yake hii aliwavisha, akawalisha na kuwasomesha watoto hawa wote. Ungeona malori ya vyakula yakimwaga vyakula pale kwake ungedhani ni oda ya duka kuu.

Shule walikosomea watoto wake ilibadilishwa jina ikaitwa Nguku Academy. Kuwatambulisha watoto hawa waliokuwa asilimia themanini ya shule nzima, kila mtoto alisajiliwa kwa jina lake moja, jina la baba 'Nguku' alafu nambari ya mama yake alivyoolewa. Kwa mfano, kama mtoto ni wa mke wa kwanza angeitwa kama Mary Nguku 01. Nambari ingeenda mpaka Nguku 36 idadi kamili ya wake zake bwana huyu.

Sasa Nguku ana umri mpevu, anaweza tu kukumbuka wake zake wa kwanza watatu na watoto wao angalau wawiliwawili. Aliyemrithisha kazi yake yani Kalu Nguku 01 kufungua mimba wa mkewe wa kwanza.

Uwepo wake katika mkutano ule ulioitwa na Mbaara ulikuwa kwa sababu za kiheshima, kipesa na kiitifaki tu; si mchango wa maarifa. Wakati wote huu Kenga alikuwa anaongea, Nguku alikuwa ashajiweka barabara kwenye kiti chake cha plastiki na kulala. Alitoa ute. Kiti nacho hakikuwa tayari tena kuhimili uzito wa huyu bwana wa kilo mia ishirini. Mara tendeguu la nyuma likavunjika na kumpeperusha Nguku juu na kuanguka kwa kishindo, Wazee wenzake wakaruka kudhibiti hali. Walifurahia kuamka kwake hata hivyo ikizingatiwa hewa iliyoharibika kila baada ya dakika chache.

Kwenye mkutano huu aliouita Mbaara, machache tu yaliweza kuafikiwa. Huu ungekuwa labda mkutano wa mwisho kabla ya marufuku ya mikutano yote kutangazwa ili kudhibiti msambao wa tandavu ya Kachina kama wengi walivyoanza kuuita ugonjwa huo.

***

Kutokana na hali hii, harusi ya Karani na Nafuu ilisalia akilini. Sharti ulimwengu ungepigana kwanza na mgeni huyu asiyealikwa. Dharura alifunga makanisa yake matatu na kuwaagiza waumini wake kusalia nyumbani. Karani vilevile alionekana mara nyingi nyumbani. Hii

ni kwa sababu shughuli za bunge zilikuwa zimesitishwa kama zile za masomo.

# Sura ya Tisa

Dharura alikuwa na kibarua kigumu. Alipokea simu nyingi kila kulipokucha zikitaka msaada. Wazazi walipiga wakimtaka awazungumzie watoto wao wasiotulia nyumbani msimu huo wa Kachina. Wanaume nao walimtaka aongee na wake zao wasio na subira na wenye kelele nyingi wakati huo mgumu. Dharura alikuwa hatoi simu sikioni wakati mwingi. Angefanya huduma nje ya madhabahu.

Juzi Dharura alijumuishwa katika kamati ya kushughulikia janga la Kachina gatuzini. Amelitoa kanisa lake moja kutumika kama mahali pa kuwatengea na kuwatibia wagonjwa wa kachina. Kamati aghalabu ilikutana na gavana wa kaunti kila baada ya wiki mbili kutathmini mafanikio ya mikakati iliyowekwa na kuratibu mingine. Katika baadhi ya mikutano hii wamepata kuwa na mazungumzo ya kando na huyu kiongozi wa Pemba. Kilichomshtua kuliko kilivyomshangaza ni jinsi gavana huyu alivyomjua na kuyajua maswala yake ya ndani. Hata anajua kwamba Mwema alijaribu kumbaka!

Dharura hakupenda kusifiwa lakini kama ilivyokuwa kawaida, ukiwa karibu na wanasiasa sharti uzoee. Siku moja alipokuwa katika mojawapo ya mikutano hii, gavana alimvuta kando. Alimsaili msimamo wake juu ya mambo mengi ya kisiasa, kijamii na hata kidini. Wakati mmoja katika mazungumo haya Dharura alimwambia “Mheshimiwa, leo hii uko katika nafasi ya ugavana kuwawajibikia wanapemba. Nakusihi uwe muungwana na mkweli. Jitume bila kuangalia kando. Kuu zaidi ujue hili, siku moja utawajibikia matendo yako yote; mema na mawi.’’ Gavana alishusha pumzi na kusema, ‘‘Maneno yako ni mazito sana, yana ukweli wenye ncha kali. Hasa kwetu wanasiasa, ukweli haupendwi, siasa za ukweli haziwezi kukupeleka mbali. Siasa ni uongo kiasi. Kila neno lako lanihukumu. ‘‘Aah, la, mheshimiwa, si fungu langu kutoa hukumu ila nakataana nawe kuwa siasa lazima iwe ya kilaghai. Usisahau kwamba hata kama mimi ni mhubiri, pia nimepiga siasa. Siasa safi. Karani ni ushuhuda wa siasa za uungwana.’’ Walizungumza mengi. Muda sasa haukuwa nao. Gavana alitaka sana Dharura awe mshauri wake jambo ambalo alilipinga sana. Waliagana na Dharura akagurumisha gari lake akaondoka. Hakutarajia gavana awe anajua juhudi zake nyingi kama alivyojua. Gavana kwa upande wake alimwona Dharura kama mtu mzuri na mbaya kwa vipimo sawa. Alimwogopa kwa sababu asiyoijua.

Jioni ile aliwapata Karani na Nafuu kwake. Karani jikoni akikatakata kuku naye Nafuu akipika chapati. ‘‘Kuna nini hapa? Mbona Nafuu unamtumia Karani vibaya?’’ Alisema kwa utani wake wa kawaida. “Wewe nawe mama unaanza na uzushi tu bila hata salamu?” Nafuu alimwuliza mama yake aliyejibweteka kochini sasa. Chakula sasa kikaandikwa mezani wakala. Karani akawaaga akitaka kutoka. Dharura alipinga sana ikizingatiwa hakuwa na ulinzi siku hiyo.

Mama na mwanawe walipoachwa walisongeana wakafanya kikao. ‘‘Mwanangu wajua aliyelala haanguki. Aliyepaa juu zaidi ndiye mwenye kishindo kikubwa endapo ataanguka. Mjihadhari sana msije mkanisiriba tope.’’ Dharura alimwambia mwanawe akimkagua kwa macho. ‘‘Usihofu mama, tumeyazungumza kwa kina mambo yetu na hii leo tuna ombi moja kwenu wazazi wetu. Mturidhie tuwe na harusi ya watu wachache kama inavyofanyika kwingineko duniani. Hakuna haja ya kusubiri zaidi madhali hatujui hali hii itaendelea kwa muda gani. Isitoshe, cha muhimu ni nadhiri kati yangu na mwenzangu. Maisha nayo hayasimami mama. Hatuwezi kupanga jambo moja mwaka mzima hali pana mengine ya kushughulikia.’’ Nafuu alimweleza mama yote waliyoafikiana na mchumba wake naye mama akayasikiliza yote akikagua kila neno kwa uzito wake. Hakuwahi fikiria kuwa shughuli nzima ya harusi ya mwanawe ingechukua mkondo huu. Kimya chake kirefu kilimtia Nafuu kiherehere. ‘‘Mmh, nitazungumza na wazazi wengine jambo hili tupate mwafaka.’’ Alisema Dharura. Hakutaka kutoa kauli yake kabla ya kusikia kutoka kwa wazazi wa Karani kwani wao ndio waliokuwa na usemi mkubwa kimila. Yeye alikuwa tayari kwa chochote ambacho kingewafaa wana hawa wawili. Wamechumbiana kwa muda sasa na ujuavyo, sana ikizidi sana huwa si nzuri sana. Keshoye aliamua kumpitia Mbaara kuhusu swala lile.

***

Kalatu mkwewe Dharura alikuwa na matawi manne ya hoteli yake gatuzini Pemba. Alipanuka kimapato na kiumaarufu. Hoteli iliyoko Kalawa makao makuu ya Pemba ilipendwa sana na watu mashuhuri kutokana na huduma zake za hali ya juu. Alijenga hoteli katika ploti aliyonunuliwa na mwanawe pindi tu alipokuwa mbunge. Hoteli hiyo ilikuwa na vyumba vya malazi na kumbi za mikutano. Kalatu kwa misingi ya jamii alikuwa mkwasi. Alilia kivulini hasa. Walioheshimu

hadhi sasa walimhusudu. Mkewe pia ni vivyo hivyo kwa kina mama wanzake. Kila kikundi kilitaka awe mwenyekiti.

Moyoni mwa Kalatu hana cha kujivunia bila kumshukuru Rabuka kwa Dharura.

Uwele wa kachina ulimtembelea. Hali ilizidi kuwa si hali, labda kutokana na umri na ugonjwa wa kisukari alioishi nao kwa mwongo mmoja sasa. Juhudi za madaktari kudhibiti hali ziliambulia patupu. Baada ya wiki moja ya kupigana na ziraili alisalimu amri. Kulifurika majonzi katika familia ya Karani na eneombunge nzima la Tunu. Kilichotia hofu zaidi ni kuwa Tendi na kitindamimba wake Joy walikuwa pia na Kachina. Karani aliona ulimwengu ukimwamulia adhabu kwa kosa asilolijua.

Sasa Karani amemzika babake. Hangemwona tena ila hakika hangesahaulika; hangesahau vito vya maisha alivyomwachia yeye na wanuna wake. Alitiwa moyo na maendeleo ya mama na ndugu yake kule hospitalini. Wangeruhusiwa kwenda nyumbani wakati wowote. Nafuu muda huu wote hakutoka karibu na Karani;

***

Shida na umaskini si ngozi ya mwili. Huisha kwa wakati wake panapo kudura. Umaskini mkubwa ni wa akili. Kutoweza kujiamulia na badala yake kuishi sababu hujafa. Kujiamulia huanza kwa kujitambua wewe binafsi alkadhalika uwezo na udhaifu wako. Kila mja ameumbwa na upekee wake. Upekee huu unapoatambuliwa huwa talanta na vipawa vya kugugumiwa mate.

Kibanda cha Jimmy kilizaa duka anamokaa mama yake Kanini. Pale kibandani aliwaajiri wafanya kazi wawili. Uwezo wa kijana huyu katika ujasiriamali ni zaidi ya mtu aliyeusomea kama taaluma. Faida yake kwa mwezi sasa ni kubwa. Akaunti yake ilifura kila uchao.

Pale alipomtambua baba yake alifurahi sana. Angalau alikuwa na mzazi. Hata hivyo alishaamua kuishi maisha kama yeye. Bila kumtazamia yeyote, hata baba yake tajiri. Ahadi za baba yake kila walipozungumza hakuzipa nafasi kumwingia akilini. Kufikia sasa, amesafiri mara kadhaa kuwaona wazazi wake wapya na pia dada yake. Kila alipofika pale nyumbani shughuli zote nyingine zote zilisimama na sizizosimama

ziligeuzwa makaribisho yake. Kila mmoja pale aling'ang'ania fursa ya kumpa nafasi ya kifalme Jimmy. Baba mtu angemchukua akamzungusha kumwonyesha mali zake mengi pale Pemba na mashamba makubwa ajabu. Katika ziara kama hii walipata nafasi ya baba na mtoto. Kilichomshangaza Mbalu ni kwamba kijana huyu hakuonyesha msisimko hata alipopata mwao na alichomiliki. Alihofu kwamba hakuwa amemsamehe bado.

"Jimmy hii mali ni ya kwako, wewe na Doreen. Unafaa ufikirie vile utakavyoisimamia.'' Mbalu alimwambia Jimmy siku moja. ''La, baba inatosha wewe ni baba yangu. Nashukuru kupata mzazi japo ukubwani ila hilo la mali ni swala nzito. Sina haja na hata ubele wa kwako. Sitaki nionekane mtu wa pangu pakavu patilie mchuzi. Tena sitaki nionekane kufurahia kifo cha ndugu yangu nisiyewahi hata kumwona. Naridhia umpe Doreen fungu langu juu ya lake. Huna deni nami baba. Nimezoea kijisakia. Tayari nina duka na kibanda vinavyonipa faida nzuri. Karibuni nafungua duka nyingine." Jimmy alimweleza baba yake. Maneno ya mtoto huyu yalimwuma sana Mbalu. Alikumbuka barua aliyoiacha Dan. Kwa mara ya kwanza akadharau mali. Hebu fikiria, umemenyeka na kazi na bidii kuu kukusanya mali; uliua, ukalemaza na kundanganya, alafu ukimpa uliyemtafutia anakataa. Alihisi kama mpishi hodari aliyempikia mpenziwe chakula kitamu akakimwaga makusudi. Ama huyu kijana amezoea shida hata mali hataki?

"Mimi ndimi mzazi hapa na watoto wangu wanahaki ya mali yangu. Naheshimu msimamo wako japo haunipi haki ya kuwajibika na nafasi ya kukusoa kasoro za kijadi. Au unataka kuniua kwa majuto? Kabla sijasahau shika funguo hizi. Ni za nyumba niliyomwahidi mama yako Kanini. Mpelekee. Najua biashara yako iko Makesi na kutoka hapo kwenda Vonza ilipo nyumba hii ni mbali. Nakupa mojawapo ya magari yangu manane kufupisha mwendo huu." Mbalu hakuwa na fursa ya kuharibu katika kupiga maisha yake kiraka. Alijitahidi kutumia mali yake kuijenga familia yake na uhusiano na jamii kwa jumla.

Hakosi siku hizi katika shughuli za jamii kama vile harambee, mazishi au harusi. Aidha, aliwafadhili watoto maskini kadhaa kielimu. Malango yake yaliyokuwa yamefungwa na kuwekewa ulinzi yalikuwa wazi kwa majirani.

Kanini na familia yake walihamia Vonza kwa jumba la kifahari. Nje ya jumba hili paliegeshwa *Landcruiser prado* gari alilopewa Jimmy na baba yake. Kwa mwonekano walikuwa matajiri kwa majirani wasiokuwa na habari na maisha yao ya nyuma. Sussy na Jossy sasa walikuwa wanafunzi wa chuo kikuu na walisoma bila shida.

Pesa hubembeleza mwili na roho. Mwone Kanini alivyorembeka siku hizi. Uso wake ulimeremeta kuzidisha ulimbwende wa mavazi aliyohakikisha yamechukuana na mapambo yake. Alipokaa pamoja na mabinti zake alionekana mchanga kama dada yao mkubwa. Hangedhani hata katika ndoto kwamba siku moja angelala na kuamkia ghorofani. Alimwona Jimmy kama mlango wa heri. Majaliwa nayo yana nguvu aise!

***

Mvua iligoma kunyesha Pemba na vuinga vyake kwa miaka mitatu. Njaa na kiu vilinag'ata kama nge. Mto kalawa ulikuwa sasa mkojo wa mtoto mdogo. Misafara ya wateka maji ilionekana ikielekea katika visima vichache vilivyomo gatuzini. Hapo kama hukuwa na subira ungepatwa na shinikizo za damu. Watu walisubiri kwa saa kadhaa kuchota mtungi mmoja. Mara vita vingezuka visimani pale mmoja wa wateka maji alijaribu masihara ya kuruka wengine katika foleni ile ndefu ajabu. Sasa kila kisima kilikuwa na askari wa kuzuia migogoro ya aina hii. Waliotaka kuepuka msongamano waliamka saa kumi alfajiri. Hawa ni wale wenye magari yao ya kuteka maji. Wangewauzia watu waliokosa kuvumilia foleni kwa shilingi hamsini kwa mtungi wa lita ishirini. Wenye pikipiki zao pia walipata upenyu wa kibiashara na kuutumia sawasawa.

Kimeshuhudiwa watu wakifa kwa njaa na kiu jimboni. Vifo vya aina hii havijawahi kuripotiwa katika historia ya janibu hizi. Serikali ya kaunti ya Pemba ilijaribu kuongeza idadi ya visima kuokoa hali iliyoelekea kuwa ngumu. Vikichimbwa vitano vilikauka vitatu. Janga lilikuwa limewakondolea watu macho mekundu na kuwategea meno tayari kuwafanya mlo.

Siku moja gavana alipoona hali si hali aliita mkutano wa viongozi mbalimbali kuchanga mawazo na maarifa ya kukabili hali ile tata. Mkutano huu ulijumuisha wataalamu wa hali ya anga na wale wa kilimo, wanamazingira, viongozi wa kidini na baraza lake la mawaziri.

Aliwatambua kwa itifaki zao na kuufungua mkutano akiwarai kutoa maoni yao kwa uwazi na bila woga. Kwa kifupi alitaja machache ya mabadiliko ya hali ya anga yaliyoshuhudiwa na madhara yake katika kauli funguzi. "Kwanza natoa shukrani zangu za dhati kwa kutii mwaliko wangu. Tuko katika wakati mgumu eneo hili la mashariki mwa nchi. Si kitambo sana tulikuwa ghala la taifa letu na hata Afrika mashariki na kati. Tulishiba na kushaza. Kiwanda chetu cha Ng'ombe *Dairies* kimekuwa kikiuza maelfu ya lita za maziwa kwa mwezi tukapata fedha nyingi za kufanyia miradi mingi. Kutokana na ukame na kiangazi, ng'ombe wetu wamefariki. Kiwango cha maziwa leo hakiwezi kukidhi nakisi iliyopo. Vilevile Mto Kalawa na mto Heri imejikaukia. Mito ambayo ilitegemewa na kila kiumbe. Kupata maji siku hizi ni kibarua. Wananchi ambao wangekuwa wanafanya biashara na shughuli nyingine za kuzalisha mali wanakimbiza maji. Utendakazi wao aidha umeadhirika pakubwa kutokana na njaa na lishe duni ya bora uhai. Hivi karibuni shule zetu zitafungwa kwa kukosa maji.'' Mkuu huyu aligusia mambo tu ili kuwapa watu mshawasha na mkondo wa mjadala ambao ulinuiwa kungelenga suluhu.

Mmoja baada ya mwengine alisimama na kutoa mchango wake wa kilichofaa kufanywa. Mengi yalikubaliwa mengi yakapingwa. Kuna huyu mwanamazingira alisimama kutoa mchango wake wa kitaaluma. ''Serikali mpaka iwekeze katika njia mbadala za kisasa za kilimo na za kuhifadhi nafaka na vyakula vingine kwa siku za mwambo kama hizi. Kwa mifumo bora ya uhifadhi wa vyakula kaunti yetu ina uwezo wa kulisha raia wake kwa zaidi ya miaka mitano ya ukame. Jingine sharti tuwe na mabwawa kadhaa katika mto Kalawa na mto Heri ya kuhifadhi maji kunaponyesha badala ya maji haya kwenda bahari Hindi. Ikumbukwe pia Mito hii iliyokauka ni ile ile iliyotufukuza viamboni kwa maji na mamba wake. Kutoka mahali nilipo nawaambia kwamba tunaumizwa na athari za tabianchi. Hali ya kubadilika kwa anga ipo kudumu hivyo hatuna budi kubadilika pia.'' Jamaa huyu mwenye tumbo kubwa lililokuwa karibu magotini alipigiwa makofi akaketi. Tumbo hili lake lilikuwa ghala tosha kuhifadhi nafaka ya karibu eneobunge nzima!

Mwengine alisima. ''Kuongezea alilosema mtangulizi wangu, ili kujitosheleza kichakula mpaka tutafute mbegu za nafaka zilizo na uwezo wa kustahimili hari ya jua na mvua haba. Serikali yetu pia itufundishe njia mbadala za kilimo. Kwa mfano ukulima wa uyoga, konokono,

panyabuku na hata nyoka kwa minanjili ya chakula. Hatuhitaji mvua kulima konokono au uyoga. Pia raia wetu wanafaa waambiwe kwamba punda, mbwa na paka pia ni mlo. Mbona ufe njaa hali una mbwa wako sita, punda kumi na paka kadhaa?  Nilipokuwa kule Uchina tulikula hawa wanyama. Mwisho kabisa bwana gavana ningetaka gatuzi letu lisajiliwe miongoni mwa maeneo kame nchiniASALili kupata msaada wa chakula na bidhaa nyingine.'' Mchango wa huyu waziri wa zaraa wa kaunti ulizua mgogoro mkali. Wengi waliapa kufa njaa kuliko kula alivyotaja bwana huyu. Utawezaje kumla nyoka ambaye akikuuma unafariki baada ya saa chache?

Aliyekerwa zaidi nusura awafunike midomo wanenaji hawa kwa viganja vyake ni Dharura. Alisimama na kupewa nafasi. Alichemka ndani kwa ndani; akaapa kusema ukweli.

''Mheshimiwa gavana wetu, acha nikushukuru kwa mwaliko wako katika kikao hiki muhimu. Tena nishukuru kwa utangulizi wako pale mwanzo iliotupa shabaha yetu kuwa hapa. Ila naona kidogo kulingana na watangulizi wangu ni kama tulipotoka kabisa. Naomba wanisamehe kusema hivyo. Uwepo wa gavana na mawaziri wake hapa ni uwepo wa serikali kama sikosei. Ina maana kwamba kufikia tulipokongomanishwa hapa serikali haikuwa na la ziada na ilitaka msaada wetu. Kurai serikali ifanye hili au lile. Ni kama kule kwa mtoto kumwomba mama maziwa naye mama anamgeukia mtoto na kumwomba mkate! Maoni yangu ni haya tusiangalie janga tulilonalo kwanza. Tuangalie kilichosababisha janga lenyewe. Mgonjwa afikapo hospitalini hana budi kupatiana historia fupi kumhusu ili kumsaidia daktari kumganga.

Mimi nimekulia chini ya vilima vya Lemba vilivyofunikwa na msitu wa Hidaya. Msitu huu ulikuwa mkubwa. Ng'ombe Dairies ilikuwa mpakani mwa msitu huu. Mbavuni mwa Lemba mlibubujika mito ya maji na vijito. Eneo lote la Tunu na Kalawa kwa upana na urefu wake lilikuwa Kanani. Kulinyesha kila wakati. Migongo ya wakulima ililalamika kujipinda kwa mipini mashambani sikwambii kubeba mazao ya kila nui. Si kahawa si mahindi si mikungu mikubwamikuwa ya ndizi. Almuradi hawakutoka mashamabani kutoka Junuari mpaka Disemba. Watu fulani waliingia msituni - maabadi ya mababu zetu- kwa mashine na matrekta. Mpaka sasa msitu umekatwa takriban kilomita kumi kuingia ndani na bado tunapoongea hivi sasa mnasikia mashine zikilia humo. Hayo mashamba ya michai na mimbuni si mwajua ni ya nani? Nawauliza, si

mnajua? Je, ninaposema nanyi hivi si mwajua wanaokata miti ni kina nani? Haihalisi kukaa hapa kuambiana uongo. Sumu yenye sukari bado ni sumu si asali. Haihalisi kucheza na akili za wanatunu kama tiara au gololi. Kumsifu simba aliyewala wanao si hakikisho atakuhurumia aisee. Mwite mfalme, mwite mwenye nguvu; bado atakula pia. Haitoshi kujenga maghala, haitoshi kujenga mabwawa au kufuga sijui konokono. Ajali kuu kuwahi kutokea miongoni mwetu ni kukubali kwamba hakuna kitu tunachoweza kufanyia mazingira yetu.

Tuliyaharibu mazingira, nayo sasa ndio yameanza kutupiga dondi. Hatujaona bado hasira zake Huu ndio mwanzo. Na kama mjuavyo mwanzo wa ngoma ni lele. Ngoma bado kuanza na tayari tushaanza kutapatapa kama vifaranga waliobughudhiwa na mwewe. Ndio sasa mkoko unaanza kualika maua. Tusipoanza kuyauguza mazingira naona maafa mengi. Kwani hamwoni tunapochimba visima vya awali vinakauka? Utafika wakati hata visima vyote vikauke. Hapo maji safi ya kupoza taya zetu yatauzwa kama mihadarati. Jameni tunapoomba misaada tutafuteni suluhu la kudumu. Tupande miti. Watu watoke msituni. Sheria kali ziwepo kulinda raslimali hii muhimu. Huenda ikachukua miaka kurekebisha hali hii lakini tutarithisha watoto wetu mazingira safi, maji na mavuno tele kama ilivyokuwa hapo awali. Ukupigao ndio ukufunzao. Natusome kwa janga hili. Viongozi wetu muwe mstari wa mbele kuregesha hadhi ya msitu wa Hidaya. Msiwe kama lile zimwi la simulizi za kimapokeo lililokuwa na nyuso mbili. Uso wa mbele wenye sura nzuri na tabasamu sumaku. Uso wa nyuma mbaya ajabu na wenye kuwala watu waliovutwa na tabasamu ya ule wa mbele. Ninachoomba nikuona mto Kalawa na mto Heri na maji yake maenge, samaki, swara, simba, mbogo na ndovu urithi wetu adimu ukiwa salama. Naamini pia mwaomba hivyo. Asanteni.'' Dharura alimalizia mchango wake alioutoa kwa amri na mamlaka. Watu walijiinamia. Gavana naye aliandikwa aibu usoni. Ni miongoni mwa adui wa msitu wa Hidaya. Alifanya biashara ya kuuza mbao Ulaya. Aidha, aliyepewa kandarasi ya ujenzi uliohitaji mbao jimboni sharti angemnunulia mbao ambazo angeuza kwa bei mara ndufu. Walinzi wa msitu huu walishafungwa macho wakamwachia kuutawala. Gavana huyu alipata mali yake mle msituni.

Kampeni za kitaifa za kulinda misitu na raslimali nyingine ziliposhika kasi kitumbua chake kikatishia kuingia mchanga. Hakuwa

tayari kuachilia mnofu uliokuwa midomoni umponyoke hivihivi. Mpaka angetakasa biashara yake. Njia yake ilikuwa moja; kukaa meza ya mabwana. Aliamini kuwa ukitaka kumvizia adui yako mkaribie ndipo umshtukie kwa karibu bila yake kujipanga. Akajitoma siasani kwa mwili na roho kwa tikiti ya chama tawala. Kwa misuli yake ya kifedha alinyakua kile kiti. Watu walisema kuwa alikuwa akimwaga pesa kama hazikuwa na dhamana kwake.

Kama gavana wa kaunti alikuwa na ushawishi katika taasisi zote za serikali. Waliofika kutetea mazingira gatuzini walipewa makaribisho ya Kipemba wakarudi wakihofia maisha yao.

Siku hii amevuliwa nguo kandamnasi ya wangwana. Hakuzoea ukweli wa aina hii kutoka kwa akina hakuna kama Dharura. Akajuta kumwalika mtu huyu.

Baada ya kuufungua moyo wake Dharura alishika njia akajiondokea. Alisindikizwa kwa macho na karibu kila mtu kuhakikisha kwamba aliyemgusa punda tako alikuwa na akili timamu. Walimwona majinuni kabisa. Kufikia hapo, walizungumza machache. Waliafikiana kuunda kamati ya kulinda msitu wa Hidaya. Waliokuwepo hawangepata mwenyekiti mwafaka isipokuwa Dharura. Japo gavana hakufurahia hangepinga kauli ya wengi. Kamati hii ingefadhiliwa na hazina ya kaunti. Wanakamati wangepewa mafunzo mudhubuti kuongeza maarifa na utendakazi. Kamati hii ingehudumu kwa miaka mitano pale wanakamati wapya wangeteuliwa.

Usiku wa manane siku hiyo Dharura alipigiwa simu iliyomwonya dhidi ya kuropokwa na kupayapaya maneno shelabela. Adhabu ya kukiuka mipaka aliyopewa ingevutia kifo chake. Sauti iliyopiga ilikuwa dhabiti na ya kutisha ajabu? Liwalo na liwe! Aliapa kusimama na ukweli hata ungawa shubiri.

Kazi ya kupigana na mifumo na wenye mifumo ni ngumu. Kabla hata kuanza mchakato wa kupanda miti tena katika msitu huu, sharti kwanza mpaka wake halisi ungebainika kwani mashine za mkuu zilifuatwa na majembe. Ukifika maeneo mengine utaona ekari za michai, mimbuni na maranchi makubwamakubwa ya ng'ombe wa maziwa na wa nyama. Sharti hawa mabwanyenye waliogushi mpaka hatimiliki za

mashamba haya wangetoka. Ingechukua mkono wa serikali kuu kuwaondosha jambo amabalo pia lingechukua muda.

Dharura aliona ugumu huu akahisi kama aliyebeba tani nzima mabegani mwake. Alijua fika pia alikuwa kwenye njia telezi iliyohitaji tahadhari. Alikumbuka simu ya usiku ule akahofu zaidi. Aliishi kusikia siasa zina uzaha, sasa ndio amedhihirikiwa na ukweli. Kilichomhofisha ni kuwa kama angepokea vitisho kama vile kwa kutoa maoni tu itakuwaje kwa matendo hasa kutimuliwa kwa wale walowezi haramu?

Ni katika mkururo huu wa mawazo ndio Dharura alipochukuliwa na usingizi. Mchana wote alishindia vita vya nafsi, akatae au akubali wadhifa ule wa kuongoza kamati ya uokoaji wa msitu wa Hidaya. Alijipata baharini yeye na wanakamati wengine wakiongelea kwa shwari ila mara bahari ikachafuka. Dhoruba kali na mawimbi yalitisha kuwasomba. Mmoja kati ya wale wanakamati alizama na kuibuka hana uhai alielea tu majini kama gogo la mkakasi. Dharura na wengine walishtuka karibu wakate tamaa ya kutoka pale hai. Kwa mbali Dharura alisikia sauti dhabiti na nzito. ‘‘Wewe u zaidi ya kimbunga, kimbunga kipitapo na vyote vilivyo katika njia yake pasi na kutetereka. Ita nguvu kutoka kila kuingo cha mwili wako zikuhudumie. Wewe u simba, guruma, na kila kiumbe atasinyaa. Wanaokutisha watajitisha wenyewe. Msitu wa Hidaya u mikononi mwako. Kilio cha watu, wanyama na ndege hakitakupa amani mpaka maji yatakaporudi mto Kalawa na mto Heri!’’

‘‘Dharura!’’ Sauti kuu ya kutisha ilimwita naye akaitikia kwa hofu ‘‘Naam!’’Akazinduka amelowa jasho na kutweta kama mwanariadha katika mbio za masafa marefu. Tangu hapo akaogopa hata kufunga macho tena.

Miezi kadhaa imepita tangu kamati ya kuuokoa msitu wa Hidaya iundwe. Safari za kwenda kwa mwekahazina wa kaunti hazina hesabu. Bado waliambiwa ruhusa ya kuipa kamati ile pesa haukuwa umetolewa. Nao wanakamati wakaelewa lugha ya mkuu wao.

Waliamua kusaka wafadhili. Lakini kabla ya kufanya hivyo, wangeanza kwa kukuza miche ambayo wangepanda katika sehemu zilizokatwa miti na bado hazikuwa zimetwaliwa. Mhalaka wa kamati na maafisa wa msitu huu uliwasaidia palipotokea haja. Maafisa hawa walikuwa wamechoshwa pia na vitisho vya gavana. Shirika lisilo la kiserikali la umoja wa mataifa

UNEP lilifika katika msitu wa Hidaya. Lilipopata kamati kama ile ya akina Dharura lilikuwa na kazi rahisi ya kutunza mazingira.

Basil, mkubwa wa shirika hilo alitamaushwa na ukweli kwamba msitu ule uliharibiwa na watu waliofaa kuulinda. Vilevile aliwahurumia wanakamati wale waliofanya kazi katika hali ile ngumu. Basil pamoja na wanakamati wale walianzisha mchakato wa kuhamazisha umma kuhusu umuhimu wa kutunza na kuhifadhi misitu.

Alisaidia pia kufikia serikali kuu na mashirika mengine yenye nia sawa. Baada ya kipindi si kirefu. Wote waliokuwa katika maeno yaliyokuwa msitu walipewa ilani ya miezi sita ya kuhama. Kukata miti msitu pia kulikuwa marufuku.

Uharibifu wa msitu huu ulimlikwa na vyombo vya habari vya nje na ndani ya nchi jambo lililomtia gavana kubuhuti. Kuna hili gazeti la SAUTI YETU ambalo lilimfanya kukosa usingizi. Kichwa cha gazeti hili siku moja kilisoma ZIMWI LA MSITU WA HIDAYA. Pale likaeleza kwa mapana na marefu jinsi biashara hii haramu ya kuuza mbao kutoka msitu huu iliendeshwa. Watu mashuhuri wakatajwa pale yeye akiwemo. Vilevile, maafisa wakuu wa idara ya misitu walitajwa katika ufichuzi ule.

***

Alipoketi pale ofisini mkuu huyu alikosa starehe. Kiti kikamea miiba, akasimama na kuanza kutangatanga pale kama mtetea anayetafuta pahali safi pa kutagia. Mara alijikuna kichwa mara kidevu chake kilichojaa mvi.

Akajichukia kwa ujinga wake. Ni vipi nge anaweza kujing’ta? Huu ni ule mwiba wa kujichoma. Laiti angalijua ule mkutano ungalimzalia kisirani asingaliufanya. Mbaya zaidi kualika mdomo uliochongoka kama Dharura. Hangefikiria hata kwa ndoto kwamba mambo yangemwendea mvange kama yalivyo sasa. Alikoka moto ukamchoma.

Alimchukia mwanamke huyu na kumwogopa kwa vipimo sawa. Mbona kiumbe huyu atambe kama moto wa nyikani? Mbona kila mahali yuko ni lazima aonekane? Mbona asikilizwe mtu hata kisomo cha haja hana?

Mustakabali wake wa kisiasa uliingia hatihati. Sharti angefanya jambo, jambo lenye hakulijua tangu hapo.

Waliosikia kauli mbiu ya kutoka msituni walifanya hivyo kwa hiari. Waliobaki walibembelezwa kwa mkono wa serikali. Gavana alipotezaaekari za majanichai pamoja na hoteli kubwa ya kifahari katika oparesheni hii.

Mfumo una nguvu mwenzangu. Kama wewe ni wa kuupinga mfumo wowote basi fikiria tena baada ya tena. Ni karibu na kujaribu kubiringisha mlima. Mfumo hasa wa uongozi tena ule wa kisiasa uogope sana. Kuna madubu na madubwana, papa na nyangumi walioneemeshwa na utimbakwiri. Unahitaji nguvu za ziada kupigana na kiongozi aliye mamlakani. Viongozi hawa wana nyenzo za kufanyia chochote kile kingawa kibaya na kuishurutisha sheria iwalinde na kuwakinga. Sheria huwaongopa wakubwa hawa nao wanasheria huwaabudu. Katiba si ya mlalia mate. Katiba ni chombo cha kiistiimari kilichoasisiwa kumdhiti na kumtiisha maskini miguuni pa mwenye uwezo na nguvu. Kifupi sheria ni wao na wao ndio sheria! Kuthubutu watu kama hawa ni kushindana na ndovu kunya.

Kulizuka kilio pale Kalawa na Pemba nzima siku ile kifo cha Dharura kilipotangazwa. Kifo hiki kulingana na wadaku kilitokana na ajali ya barabarani ambapo gari lake lilikosa mwelekeo na kugongana ana kwa ana na lori lililotoka upande ule mwingine. Kwingineko ilisemekana kuwa lori hilo ndilo lililoingia safu si yake makusudi na kuligonga lile la Dharura. Lori hili la taka la mji wa Kalawa lilikuwa limekwama barabarani pale tangu jana. Kulikuwa na wanaume wanne waliokuwa wakiingia mle na kutoka. Cha kushangaza hawa watu hawakuwa wafanyakazi wa barasa la mji, vilevile hawakuwa mafundi kwa sababu hakukuwa na shughuli zozote za kulirekebisha lile gari. Dharura hakuwepo tena. Jumbe za rambirambi zilifunika anga ya Nafuu na familia yake. Rambirambi za kwanza zilitoka kwa gavana wa kaunti akimtaja mwanamke huyu kama ngangari na aliyewapiku wengi katika utendakazi wa chochote alichofanya, Alimtaja kama mfano mwema wa makasisi waliongoza waumini katika njia yao nyoofu ya paradiso. Aliahidi kugharimia gharama zote za mazishi ya mwendazake.

Pale kwenye mochari ya hospitali kuu ya Kalawa kulijaa watu waliofika kuhakikisha kweli mwanamke huyu alikuwa amefariki. Vilio pale vilisawiri vile vya vyura wakati wa masika. Muradi kila mtu alikuwa na lake alilolililia. Kuna wale waliomboleza kufiwa na kasisi wao, wengine aliyewavua wanao mikononi mwa ugaidi, wengine mwanaharakati na baadhi mwanamazingira.

Utiriri wa payo vilianza pale. Udaku ni kikohozi. Hauzuiliki. Mengi yalisemwa ila hakuna aliyediriki kuyasema paruwanja. Wandani wa binti huyu wa mrina asali walijua tangu hapo haikuwa ajali ya kawaida ila hawangedhibitisha. Waliyaachia majaliwa kunena. Polisi walikuwa na kazi ya ziada kukitegua kitendawili kile. Walilizungushia eneo hilo la ajali utepe na kuanza kuangalia hiki na kupima kile. Baada ya muda, gari la Dharura likavutwa hadi kutuo cha polisi.

Nafuu na mumewe walionekana wakitoka chumba kile cha kuhifadhia maiti. Walitumia mbinu zote kukwepa wanahabari waliokuwa wakisaka habari kwa hali na ghamu. Walijitoma garini na kuelekea kusikojulikana. ‘‘Mwenzangu nina hofu,” Nafuu alianza hali ameudhibiti usukani. “Gari lililohusika ni la mama ila maiti tuliyemwona pale ana shaka. Mama akitoka asubuhi alikuwa anaenda kumwona Basil yule mwanamazingira-Pemba mjini si Kalawa kwa shughuli rasmi. Tena mama hakuwa amesukwa hivyo kama unakumbuka kwa sababu tulikuwa naye jana mpaka jioni. Daima mama hajawahi kuvaa suruali ndefu, yule maiti amevaa. Isitoshe, hapendi lipustiki na marashi kama ya yule. Ila cha ajabu ni kuwa sura, kimo na mwili mzima ni wa mama!”

Karani alikuwa pale kiwiliwili tu, mawazo yake yalikuwa mbali hata pale mkewe alipomzindua. “Naongea na jiwe?’’ “Mmh, shaka yako inalandana na yangu na imeniathiri pakubwa. Tena kama ni ajali ya kawaida mbona ana tundu la risasi kidarini. Inadaiwa pia kumeokotwa marisawa katika eneo la ajali. Mpaka tufike kwa D.C.I. Lakini naomba jambo moja, kwamba hii shaka ibaki baina yetu wawili. Mipango ya mazishi ianze kama kawaida. Kuna uwezekano ikawa ni yeye tu.

***

Nyumbani kwa Karani kulifurika watu wa kila aina wote hawa wakileta rambirambi. Siku ya mazishi hasa kwa Karani nayo iliwandia haraka. Yapata wiki tatu tangu Dharura afariki. Yangefanyika siku tatu kutoka leo. Maafisa wa D.C.I hawakulala. Wamekuwa wakiingia na kutoka mochari kila baada ya siku moja au mbili tangu ajali ile ilipofanyika.

Simu waliyopata kwa mabaki ya gari lile kuongezea kizungumkuti haikuwa yake Dharura bali ya mwanamke raia wa Tanzania kwa jina Huduma Ngozi. Stakabadhi zilizokuwa pamoja na simu zilimwashiria

mwanamke huyu. Nafuu wakaitwa na makachero wale. Walishangaa upeo wa kushangaa. Hawakumjua wala kuwahi kumsikia mtu aliyetajwa. Sasa kama ni hivyo mama mwenyewe yu wapi? Maswali sugu yalizidi kuunda jedwali ngumu kwa mtu na mumewe. Kufikia hapo makachero wale waliomba msaada wa wenzao wa Tanzania ili kulifumbua fumbo lile.

Saa zilienda upesi. Mazishi yangefanyika chini ya saa ishirini na nne. Walihitaji habari muhimu ambazo hawakuwa wamezipata kufikia wakati ule. Wangechelewa kidogo kungezikwa mtu tofauti ama mazishi yangehahirishwa bila sababu maalum. Lakini hata hivyo mambo yalilainika kiasi walipopata isharamawimbi za simu ya Dharura mjini Takuja mtaani Vonza. Usiku wa manane mtaa huu ulipokea wageni. Wageni walifika kwa dharura kusaka Dharura! Dharura alifika pale yapata wiki nne zilizopita. Mtu na dada yake walijawa na furaha isiyo na kifani. Siku hizi zimewakumbusha utoto wao na maisha ya dhiki kuu. Kifo hicho cha Huduma kulifichua siri angavu. Dharura na Huduma walikuwa Pacha. Mamake alimtoroshea kule Tanzania baada ya mila na desturi kukinai. Pacha sharti wangeuawa.

Kwa muda wa mwaka mmoja Dharura alikuwa akiwasiliana na Huduma tangu wapatane katika mtandao wa *Facebook*. Huduma sasa alikuwa humu nchini kukutana na pacha wake. Siku iliyozaa mauti yake walikuwa wakutane katika hoteli ya Kalatu kule Kalawa. Hawangezuia machozi ya furaha walipopatana pale Kalawa. Waliongea mengi ndugu hawa waliotenganishwa na majaliwa mara walipozaliwa. Roho zao zikavutana kama walioishi tangu utotoni. Ama hayo yalikuwa yale ya damu na maji? Baada ya kula na kunywa ulifika wakati wa gari la Huduma kupata huduma. Kweli ilikuwa safari ndefu kutoka Mwanza mpaka pale Kalawa. Dharura alikuwa amtambulishe kwa Nafuu na mumewe jioni ile. Dada wale waliamua kubadilishana magari ili kila mtu alionje la mwenzake. Dharura akaongoza mwenyeji wake njia. Walipopiga kuruba moja ili waingie gereji aliyeizoea Dharura palitokea kionja. Lori lililokuwa limebeba watu wane pale mbele lilikuwa linajikokota barabarani likitoka upande ule mwingine. Dharura alilipita mbio ila akapunguza mwendo akawa analiangalia kupitia kamera ya nyuma. Hakuamini macho yake pale lori lile lilipomwingilia Huduma na kumrusha mtaroni kando ya barabara. Wawili kati ya wale wakatoka

mbio na kuchungulia kama alikuwa hai wakasikika wakisema 'kazi safi!' Hapo wakaliacha lori lile pale na kupanda bodaboda na wakatoroka.

Dharura alikumbuka simu ile ya usiku wa manane. Maskini dada yake amekufa kifo chake hata hawajapata kujuana vyema. Akajuta kumtia dada yake safarini. Safari ya mauti. Kila pahali sasa palinuka kifo. Sharti angeingia mafichoni. Hivyo ndivyo alivyojipata kwa dada yake mkubwa Kanini ambaye si miaka mingi tangu warudiane. Kanini alilaghaiwa na yule daktari wa Kalawa kwamba angemwoa akamwacha Dharura na bibi yake mkongwe bila ya kupigwa na mshipa. Wawili hawa waliachwa wahitaji mmoja mzee sana naye mwengine mchanga sana. Dharura alimchukia Kanini kwa moyo wote kwa shida aliyopata kumlisha na kumwuguza bibi yake mpaka pale alipoaga. Huyu daktari angempeleka Takuja na baada ya kumpa watoto wawili akawa umande.

Sasa Jimmy walikuwa wanatazamana uso kwa uso na wageni waliojitoma ndani ya nyumba bila mwaliko bastola mkononi. Watu hawa hawakuwa na ugumu wa kumtambua Dharura. Walijitambulisha kifupi baadaye wakamwita chemba na kumhoji kwa kina. Aidha walimweleza kwamba walishagudua njama iliyokuwepo ya kumwangamiza lakini kulikuwa kwema mpaka pale.

Watu wale walipoondoka, Dharura alichemkwa na hari kutenda lililo nadra. Kuhudhuria mazishi yake! Makechero wale walikuwa wamemwambia hilo halingekuwa na shida. Tena ingekuwa njia mwafaka kusitisha mazishi yale na kumfichua muuaji ambaye angepewa nafasi nzuri pale mazishini.

Shughuli za mazishi zilikuwa bambam. Watu wa kila aina walikuwa wamejaa pale uwanja wa shule ya msingi ya Ibra. Jukwaa la aina yake lilikuwa limeezekwa kwa hafla hii muhimu. Viongozi mashuhuri kote Pemba wangekuja. Wa kidini na wa kisiasa. Dharura hakuwa mtu sampuli ya akina mimi na wewe ambao tukifa leo mazishi yatajaa walevi na wendawazimu wenye njaa. Sikwambii idadi kubwa ya majibwa ya kijijini yatakayokuwa makitaimu kungojea matapishi ya vyakula duni watakavyobugia hawa akina hakuna baada ya konyagi.

Aghalabu katika mazishi ya akina Dharura mpaka uwe makini na itifaki ama uhukumiwe kumkosea kiongozi fulani heshima. Hapa watu hutambuliwa pindi walipowasili kwa mikongo yao. Mazishi haya ni

sherehe kuu kushinda hiyo harusi yako uliyohifadhi katika kanda za video duni kwa mbali. Katika mazishi ya kina Dharura hakukosi siasa.

Waandalizi waliokuwa na sare rasmi kwa siku hii walionekana wakikimbia hapa na pale kufanya hili au lile. Waliweka mshipi wa bendera ya nchi upande wa juu wa jukwaa ukazunguka jukwaa nzima. *"One two ...one two*…mic testing…one two!" Mafundi wa mitambo walijaribia vipazasauti.

Kufikia mnamo saa tatu hivi wachinjaji walikuwa wamemaliza kuwachinja ng'ombe kadhaa waliotolewa na gavana. Wapishi nao walikuwa katika juhudi kuu za kuhakikisha chakula kii tayari kwa wakati mzuri. Ibada ya mazishi ingeanza saa nne unusu. Kufikia wakati huo umati mkuu ulikuwa umejikusanya hata usipate pa kutema mate. Watu mashuhuri walianza kuingia kwa magari ya kifahari yaliyoashiria hadhi na vyeo. Wengine walifika kwa magari yenye ving'ora, watu wakabumburushwa huku na kule kutoa nafasi ya kupita na kuegesha. Viongozi kama hawa walikuwa na walinzi wenye suti jeusi mashati meupe tai nyekundu na miwani mieusi. Waone walivyowazunguka wakubwa hawa, mtu alishangaa walikuwa katika hatari gani tusiyoiona sisi. Kazi ya walinzi wale ilionekana ngumu lakini hivyo ndivyo walivyokidhi familia zao maskini.

Jeneza lililokuwa pale mbele ya jukwaa lilikuwa la kima kikubwa cha pesa. Ibada ilianza kwa mbolezi. Nyimbo hizi ndizo hufanya watu walie zaidi ya msiba wenyewe. Baada ya ibada zilifuata hotuba za watu mbalimbali kuanzia na shehe Musa aliyekuwa rafiki mkubwa wa Dharura na aliyekuwa na mitazamo sawia ya kidini. Hakika watu hawa wawili walifaana sana kutoka enzi zile walipokuwa wanapigana na watu waliokuwa wanasajili vijana kujiunga na kundi lile la kigaidi la Sinautu mpaka wakati wa kuhamasisha watu dhidi ya Kachina.

Gavana alimmwagia mwendazake sifa baada ya sifa kwa msamiati teule. Hakukosa kusema vile mama huyu alikuwa rafiki yake wa karibu. Akataja mchango wake mkubwa katika jamii na mapenzi yake kwa msitu wa Hidaya. Bila shaka alijitia sononeko.

Ulikuwa wakati wa familia. Kabla ya Mbalu kuwahi pale pa kipaza sauti. Dharura alikuwa pale amejitoa ule mtandio na miwani. Watu walioshtuka walikanyagana wakikimbilia wasikokujua. Mpaka watu

mashuhuri kama gavana walikuwa mbioni isipokuwa Karani na mkewe. “Msiuane mkinikimbia. Sijafa ni hai. Msiumizane nikajilaumu kwa majeraha yenu.’’ Dharura alijitahidi kuwatuliza watu waliokuwa wanapiga duru kama waliopagawa.

Jinsi kiumbe huyu mwanadamu alivyo wa ajabu. Walilia kifo chake kwa wiki nne. Sasa badala ya kufurahia kwamba yuko hai wanamtoroka kwa hofu! ‘‘Tulieni niwapashe mnachotaka kusikia.” Umati ulianza kuregesha utulivu wake. Waliokuwa wametoroka walirejea ila kwa tahadhari kuu.” Aliendelea “Nashukuru Mungu kuwa bado niko hai japo niliponea kwa tundu la sindano. Waliyemwua na aliye jenezani hapa ni Pacha wangu Huduma Ngozi.” “Pacha!’’ Kila mtu alishangaa. “Naam, pacha wangu.” Dharura aliuambia umati. “Miaka ya awali kama tunavyojua jamii yetu iliwaona pacha kama laana. Hivyo mama alipotuzaa alimwomba mkunga wake mtanzania amwokolee mmoja wetu ndipo akamchukua Huduma aliyenitangulia kuzaliwa na kutorokea naye kwao. Alimlea mpaka akawa mtu. Kufikia kifo chake dada amekuwa mwanamke mwanabiashara tajika Mwanza. Juhudi zangu kidogo za kupigania msitu wa Hidaya zimesambaa kote Afrika mashariki na Afrika nzima. Hapo ndipo zilipomfikia dada yangu ambaye tangu hapo alikuwa mwanamazingira kule kwao. Akawasiliana nami akitaka ushirikiano wa pamoja katika kazi hii adhimu ya utunzi wa mazingira. Tulivyozidi kuwasiliana kupitia mitandao ya kijamii ndivyo tulivyozidi kushangaa jinsi tulivyolandana kwa kila kitu. Hapo ndipo nilipomdokolea siri niliyokuwa nimeiweka moyoni siku zote. Kumbe kabla ya yule mkunga kuiaga dunia alimweleza kila kitu kuhusu usuli wake pia. Tukapanga kukutana.” Watu wote walimakinika kama watahiniwa waliosuburi mtihani muhumu. “Laiti ningalijua Judas wangu alishapewa pesa na akala! Nikisema hivyo si mwajua mhusika? Uchunguzi umefanyika na watu wawili sasa wamo mbaroni wakiwasaidia polisi kwa uchunguzi zaidi. Hasidi wangu amekuwa hapa akiniomboleza. Aliyetoa pesa nipokwe uhai ameyagharimikia mazishi yangu pia.’’ Miguno ya ghadhabu ilisikika hapa na na pale.

“Ninachoomba ni msamaha kwa wote walioniomboleza. Nimekuwa na nafasi nadra kuzipokea rambirambi zangu mwenyewe binafsi. Kuona machozi ya dhati kama ya ndugu Musa, iliuma sana kinyume na mengine ya Mamba ya mwafulani hapa. Niwaambie ndugu zangu mlio hapa, hakuna aliye na uwezo na hatamu ya maisha yako. Tena

niwaambie hakuna aliye na kitenzambali cha kudhibiti akili na mkondo wa wako wa mawazo. Maamuzi yako hayafai kusahihishwa kwa yale ya mwenzako. Aisee!

Alimalizia pale akawasalimu wengi ila akasema machache. Akaiendea jamaa yake na kuketi kando ya Mbalu. Alijua wana mengi ya kujua ila haingekuwa pale uwanjani. Upande wa kushoto wa jukwaa aliketi mtu mwenye mawazo chungu nzima. Hakuwa na starehe mahali pale gavana yule. Aibu ilijichora usoni. Kitumbua kishaingia mchanga. Mara baada ya sala zala mwisho gavana alitoka. Alihitaji kuwa mbali sana na mahali pale. Alihitaji majibu fulani kutoka kwa mtu fulani. Hakuwahi garini mwake kabla ya kutambua kuwa maafisa wa D.C. I walikuwa na ruhusa ya kumtia mbaroni kwa mashtaka ya mauaji. Hakuwa na nguvu ya kubisha.

# Sura ya kumi Moja

Basil alikuwa ofisini mwake jijini Takuja ambamo ni makao makuu ya UNEP. Alipekuapekua faili fulani na kutikisa kichwa ishara ya kuridhika. Hii ni baadhi ya ripoti anazopokea kuhusiana na uokoaji wa msitu wa Hidaya. Pamwe na ripoti hii zimo picha kadhaa za ushuhuda na idhibati. Sasa asilimia sitini ya eneo lililoharibiwa limepandwa miti inayoendelea vyema. Ufadhili zaidi ulikuwa umetolewa pale ambapo habari za mahangaiko ya watu na wanyama yalipoangaziwa na kufikia masikio yenye huruma.

Naibu wa gavana wa Pemba alipochukua hatamu mambo yalikuwa nafuu kwa kiasi kikubwa. Alijitolea kushirikiana na ile kamati teule na UNEP katika kila lililohitajika.

Siku hii ya Jumatatu mwendo wa saa nane Dharura alipokea simu ya Basil iliyomwarifu kwamba kulikuwa na kinyanganyiro cha tuzo la *Champions of the Earth Award kategoria* ya *Inspiration and Action* na alikuwa amechaguliwa kushiriki na gatuzi lake. Kwa upande wake Dharura aliona kwamba hakuwa amefanya ya kutosha katika kutunza mazingira kutosha kuwania nafasi kama ile. Alikubali shingo upande.

Hakuutilia maanani ujumbe ule. Alijituma kuhakikisha miti iliyopandwa haikauki. Walikuwa sasa wameingia katika mpango wa kuuza kaboni na kampuni fulani ya ulaya kwa msaada wa Basil. Wanatarajia kutumia fedha watakazopata kukuza miche zaidi na pia kuchimba visima vitakavyosambaza maji ya kunyunyizia miti ile. Zaidi UNEP iliajiri watu kadhaa wa kuitunza miche na miti wakati wote ili kuhakikisha haiharibiwi na wanyamapori au magonjwa.

Siku moja akiwa katika shughuli zake za kuwasimamia watu pale Dharura akapokea simu ya Basil ikimweleza kuwa alikuwa ameshida tuzo ile. Hakuamini masikio yake. Alipata naima tele kwa habari ile. Alimpigia Nafuu akamwelezea. Wote walifurahi. Haukupita muda kabla yake kuanza kusakwa na wanahabari waliotaka awaeleze alivyofanya yote waliyoyasikia. Angewaleta pale msituni na kuwahadithia shida na hatari iliyokuwepo kuwang'atua watu pale pamoja na shughuli nzima ya kupanda miti kwa kile kiangazi. Habari zake zilisambaa ulimwenguni na wapenzi wa mazingira walimtumia jumbe za pongezi.

Japo tuzo hii haikuja na pesa kama zilivyo tuzo nyingine lilimfungulia milango mingi. UNEP ilimfanya balozi wa mazingira wa heri njema. Ilikuwa furaha mara dufu kwani Jumamosi iliyofuata ilikuwa kuu kwa kwake na Mbaara. Siku ambayo viumbe hawa wangerudiana tena baada ya miaka mingi. Hakika Nafuu hakumjua baba mpaka umri wa miaka mitano au sita hapo. Wazazi wake waliachana akiwa mdogo wa kujua kilichoendelea. Wote wawili walikuwa wamechangamkia jambo hili kama maharusi waliofunga ndoa. Wote wamefuzu kutoka chuo kikuu cha maisha shahada nazo zimo mioyoni. Mbaara alijiapia kufidia hasara ya mapenzi aliyomsababishia mkewe kwa ugumu wa moyo na ulevi. Dhamani yake kwa mkewe haikuwa na mfano. Alijiona mwenye bahati ya mtende kuiachilia bahati na ikamrudia tena. Siku hii Mheshimiwa Karani na mkewe walikuwa na yote ya kushukuru kwa tendo hili wazazi wao. Angalau wangeondoleana upweke badala ya kuishi kila mtu kivyake. Furaha kubwa ni kuwa wangempokea mjukuu wao aliyekuwa karibu kushika ardhi Pamoja.

Dharura aliyashika majukumu yake kama awali. Sasa ni mtu mashuhuri si Pemba tu bali nchini na dunia nzima. Mali alikuwa nayo: mashamba, ploti na hata biashara. Haya lakini hayakumpa kiburi mbele ya mumewe aliyekuwa karibu tu na alivyomwacha miaka ile. Aliapa kumwanzishia biashara ya duka kuu wakati lile jumba lake la ghorofa mbili kule Kalawa litakapokamilika. Aidha, alimwachia kusimamia mali yote kama mwanamume wa nyumba kazi aliyoifanya vyema.

Si kitambo sana tangu Karani na mkewe walipofunga nikahi katika sherehe iliyokuwa ya wachache kwa sababu ya janga la kachina. Ugonjwa huu ulikuwa umetishia utangamano wa kijamii hasa wetu wafrika. Sheria zote zilizowekwa zilikuwa za kutenganisha jamii. Jimmy naye na Jamila wakafanya yao vilevile baada ya kuchumbiana kwa muda.

***

Ndoa yake Jimmy na Jamila haikuwa sawa. Kanini aliondokea kumchukia mkazamwanawe ajabu. Hakuwa na sababu maalum. Hii ilianza tu pindi alipowaona wazazi wake. Jimmy alimwendea Hassan bamkwewe kwa neno.

Katika maongezi yao Jimmy alimjuza Hassan jinsi alivyojipata mkononi mwa Kanini. Pale ndipo alipojua alichohitaji kujua muda wote huo. Kama Hassan alivyomwambia ni kwamba amewahi kufanya kazi hospitani ya Kalawa kama daktari. Hapa ndipo alipoanza taaluma yake. Tena ndipo alipopata kujuana na Kanini wakawa wapenzi.

Alipopewa uhamisho mpaka Makesi walihama pamoja wakimwacha nyuma dada yake mdogo na bibiye. Hakupata kuwajua wazazi wa Kanini. Kule Makesi maisha yalikuwa mazuri lakini mabaya kwa wazee wake waliomtaka Kanini abadili jina. Aliposusia kufanya hivi wazazi walitishia kumkataa na kumlaani asipoachana naye.  Kwa jinsi alivyompenda hakusikia maneno yao na hivyo waliendelea kuishi mpaka wakamzaa Jossy. Kanini alimkosea alipogundua alikuwa na uhusiano wa kando na afisa mkuu wa kituo cha polisi cha Makesi na kupelekea kupata mimba naye. Sussy akazaliwa. Alikuwa tayari kumsamehe aliposhtukia Kanini pia alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa zinaa usiopona. Alitafuta uhamisho na kubeba kilichokuwa chake na kwenda kuanza maisha upya. Hapo ndipo alipomwoa mama yake Jamila aliyekuwa muuguzi hospitalini alikohamishiwa. Hawakupata kuongea na Kanini tena mpaka pale Uhusiano wake na Jamila ulipowakutanisha.

Ukweli huu ulimwadhiri sana Jimmy. Hajawahi kujua kwamba Jossy na Sussy si wa baba mmoja. Pia hakujua kwa mama yake mlezi ameishi na virusi vya ukimwi. Hassan alipoona hivyo alizidi kumwelezea “Sijakupa ukweli huu uende kumwumbua mama yako. Kusudi kuu la kukuambia ni uelewe kwamba shida ya Kanini si nyinyi ni mimi. Anampima Jamila kwa mizani yangu. Anahofu pia tofauti zenu za kidini huenda zikavuruga maisha yenu. Uamuzi ni wenu wawili. Ndio maana sisi hatukupinga Jamila alipotuambia anakupenda. Mungu ni yule mmoja njia za ibada ndizo tofauti. Tena mungu mwenyewe hana dini.’’ Alimrai amwendee mama yake kwa upole na amhakikishie kwamba yote ni salama. Jimmy aliporudi Takuja alimwendea mama yake wakaongea roho yake nayo ikatulia.

Jimmy alipomweleza shangazi yake –Dharura- kuhusiana na mgogoro kati yake na mama yake aliingilia kati na kumsuta dadaye kwa kuchukiza watoto. Alimweleza bayana kwamba mwana akinyea kiwiko hakikatwi

Jossy alipohitimu shahada yake ya uuguzi, aliajiriwa kwenye hospitali kuu ya Takuja. Kutokana na gharama ya kila siku ya kuja nyumbani aliamua kupanga nyumba karibu na kazini kwake. Ni mwenye biidi sana katika taaluma hii aliyoipenda. Alihisi aliyeumbwa kuifanya. Kila anayepitia mikononi mwake huishi kushukuru kinyume na wauguzi wengine ambao huwa na roho kavu kihisia. Hawa ni wale walioshtumiwa kwa kuangalia kina mama wajazito wakijifia kwa machungu ya uzazi.

Kwa sadfa siku hii alikuwa nyumbani Jimmy alipokuja. Ilikuwa furaha ilioje ndugu kukutana baada ya muda mrefu? Lakini dada ya mtu alitaka kujua mbona walitoka nyumbani kwenda kuishi mjini kati. Jambo hili alililikwepakwepa likasahaulika. Jossy naye alimtangazia kuwa alikuwa amepata mchumba aliyenuia kumleta nyumbani karibuni ila bado alikuwa hajamwambia mama. Aliendelea kumwambia kuwa mchumba wake mzungu kutoka Kiuba. Alikuwa daktari pale alikofanya kazi na angemchukua waende kwao ng'ambo kadarasi yake itakapoisha miaka mitatu ijayayo. Ni kutokana na hili aliogopa sana mtazamo wa mama, aliohofia haungekuwa chanya. Jossy akamwomba amtembelee siku moja amwone huyu rafiki yake.

Jimmy alipokutana na Mike alishtuka kidogo. Alikuwa mzee wa takriban miaka hamsini hivi. Hata mvi zilikuwa zimemtoka kichwani. Mike alifurahia kutambulishwa kwa Jimmy kama mchumba. Aliwapeleka hoteli moja ya kifahari walipokula kunywa kuogelea na kufurahia. Lakini Jimmy akamwona kando dada yake na kumweleza jinsi uhusiano wa aina hii ungeweza kuathiri maisha ya ndoa. Alimweleza kwamba mahitaji yake kama kijana yatakuwa tofauti na yake kama mzee. Pia Uwezekano wa maisha marefu naye pia ni finyu kotokana na sababu za kibaolojia ambapo magonjwa mengi huazia uzeeni. Huenda wasipate kuwalea wanao kufikia ukubwani. Kadhalika, huenda mzee kama yule asimtosheleze kihisia na hili huenda likawa ufa utakaobomoa familia.

Mwisho akamtaka achunguze uwezekano wa familia nyingine huko kwao au kwingineko. Jossy hakuwahi kutazama mambo kwa mkondo huu. Alimshukuru sana kaka yake na kumwahidi kuwa angetilia maanani maaso yake. Kwa kweli alikuja kupata kwamba bwana huyu alikuwa na mke na wototo wakubwa. Kitinda mimba wa mzee huyu alikuwa mkubwa wake kwa umri. Cha kushangaza, watu hawa wote hawakuwa na shida na ndoa yake na Mike. Kwa Jossy ulikuwa mgogoro mkubwa sana kulingana na mila na tamanduni za zao. Hakuwa tayari

kujipalia makaa ya kumchoma. Hawakuwahi kumtajia yeyote kuhusiana na haya ila walipokuwa wawili Jimmy angemtajia kwa utani, “Ulisema tunaenda Kiuba lini? Wote walicheka mtu asijue walichokichekea.

# Sura ya kumi na Mbili

Gerezani Kimwilu Mwema na aliyekuwa gavana Dkt. King'ori wamekuwa marafiki wa toka nitoke. Mwema ndiye aliyempokea pale na kumkinga na makaribisho ya jela. Yanayofanyika humo jela hayazungumzwi kwa sauti. Gereza hili ni miongoni mwa magereza makuu nchini. Yana wahalifu wa kila namna wakitumikia vifungo mbalimbali. Baadhi ya miaka michache na baadhi vya maisha. Katika jela kila kitu isipokuwa kupumua ni starehe na anasa ghali. Bidhaa vya msingi kama dawa ya meno, shashi na vinginevyo kupata ni ngumu.

Kupata mahitaji kama chakula cha haja kwa yule mfungwa hana pesa ni kibarua kigumu. Ingekulazimu uwahonge wajumbe. Wengi wa hawa huingizwa katika umende ili wapendelewe. Tabia hii imekidhiri kupindukia katika magereza yote popote. Waliopinga kushiriki hulazimishwa na hata kubakwa na wenye nguvu na ushawishi kule. Pia, wangepatiwa kazi ngumungumu kupigwa na hata kubaguliwa. Dhuluma hii ilichangiwa pakubwa sana na tofauti za kiumri baina ya wafungwa.

Kijana wa miaka ishirini atawezaje kujikinga dhidi ya dhuluma ya mwanaume mkubwa wa miaka arobaini? Kutokana na maisha kama haya, wafungwa wengi huugua magonjwa ya kiakili wanaposhindwa kukabili migogoro ya kisaikolojia inayochangiwa na baadhi na dhuluma hizi pamwe na kule kunyimwa uhuru, faragha na kuwapeza wapendwa wao. Cha kutamausha ni kuwa idara ya magereza haina huduma madhubuti za kukabiliana na msongo wa mawazo na shida nyinginezo za kisaikolojia.

Tangu Mwema ampokee gavana anakula mazuri ya ulimwengu. Kila kitu anapata kwa vipimo vikubwa. Gavana naye angalau hakuwa na upweke mkubwa alivyodhani kwa sababu ya uwepo wa huyo kondoo wa bwana. Mwema alimsimulia mengi yenye hofu aliyoyashuhudia na kuyasikia. Alimhadithia kisa cha jamaa mmoja aliyejiua pale alipofungwa pasipo haki.

Baba yake marehemu alipofariki kwa njia isiyoeleweka haukupita muda mrefu kabla ya ami yao kuanza kuwafurusha kutoka mahali walipopaita nyumbani. Kisa na maana mama yao alikataa kurithiwa naye. Kesi ilipofika kwa polisi haikwenda mbali iliishia pale kituoni. Mambo

yaliharibika pale ami alipoanza kumpiga mama yake baada ya kuchukua ng’ombe wao watatu na kuwauza. Alimkabili ami yake na kumpiga mkono ukavunjika. Mama alikuwa ashang’olewa meno mawili ya mbele na yule jamaa. Kijana alishtakiwa na kesi ikageuzwa kwamba yeye ndiye aliyekuwa akimpiga mama yake na ami alipokuja kumwokoa mama mikononi mwake akapigwa pia. Kijana huyu alijipata pale jela akihudumia kifungo kwa kosa la jinai. Kilichomtuma mautini ni kusikia kuwa ami alikuwa amemshurutisha mama yake kuwa mke wake wa nne. Tetesi pia zilisema alikuwa anamyemelea mkewe.

Kijana aliumia kwa kuwa haki haikuzingatiwa katika kesi yake kwa kuwa hakuwa na pesa kuununua ukweli ulioonekana mpaka na kipofu. Alishindwa angerudi wapi baada ya kifungo kwani hakuwa na chochote, si shamba si nyumba si mama si mke. Alijiamulia kifo kuliko kutoka jela na kurudi tena huko kwani hakuona akimwacha ami yake bila alama.

Akamsimulia King’ori jinsi biashara ya dawa za kulevya ilivyoendeshwa pale jela. Mahabusu waraibu wa dawa hizi walishirikiana na wahoroso wengine katika biashara ile haramu. Wangeletewa na kuwauzia wengine pale. Pale kuna wafungwa waliokuwa na simu walizozitumia kulaghai raia kule nje kupata pesa. Simu hizi zililetwa na wawa hawa askari. Gavana alishangaa sasa kwa nini jela iliitwa mahali pa kurekebishia tabia badala ya mahali pa kuharibia tabia zilizoharibika tayari!

Jela ni Chuo Kikuu cha Uanasheria. Kule kuna watalaamu wa ‘kuruka’ kesi wengi. Wengi wemeingia pale na kuongozwa kutafuta rufaa na wakafanikiwa kutoka. Kuna wale walioonywa dhidi ya rufaa kulingana na kesi iliyowakabili. Masila ni mmoja wa watalaamu hawa. Kila aliyeingia jela hili mpaka angempa huduma yake hii adimu. Mzee huyu wa miaka themanini na saba alihukumiwa kifo yapata miongo mitatu iliyopita baada ya kumuua mkewe na mwanamume aliyekuwa mpenzi wake wa siri. Hukumu hii ilikuja kubadilishwa ikawa ya maisha baada ya serikali kuondoa hukumu ya kifo. Masila ndiye mahabusu mkongwe zaidi mle. Aliitwa na wengine Babu.

Amekuwa wa msaada pale katika kutatua migogoro baina ya wenzake. Kutokana na umri wake mpevu hakupewa kazi ngumu. Kazi yake ilikuwa ni kuchambua nafaka na kulisha nguruwe. Hakuwa na tamaa

ya kutoka pale. Kwake hakuona haja ya kwenda kujitambulisha kwa watu wa jamii wasiomjua.

***

Kesi ya Mbalu imeisha baada ya kukosa mashahidi wa kutosha dhidi yake. Karani kwa heshima ya marehemu Dan alikuwa amekataa kuwa shahidi kwa ile kesi. Waliojitokeza kama mashahidi hawakuwa na ushahidi wa kumhusisha moja kwa moja na uhalifu kwani Nduli mshukiwa mkuu alipatikana hana akili timamu kusimama kizimbani ama kutoa habari zozote za kuaminika.

Furaha ya kuondolewa mashtaka dhidi yake iliyeyuka mara alipopata habari za kuugua kwa Mwenda mkazamwana wake. Kwa muda mrefu sasa amekuwa akihisi maumivu madogomadogo viungoni aliyopuuza kama machovu ya kazi. Alikosa hamu ya chakula na kumwaga damu kwa pua bila jeraha. Mara alijihisi dhaifu kabisa asiweze kufanya kazi. Angepumzika kwa siku chache na kuendelea tena na shughuli zake. Amewahi kwenda hospitali kuu ya Kalawa na kuambiwa kuwa ndamu yake ilikuwa imepungua. Akapewa dawa na orodha ya vyakula ambavyo angetumia kuongeza viwango vya damu mwilini. Baada ya muda alirudi tena kliniki kama alivyoagizwa. Damu yake ilikuwa imepungua kuliko awali.

Daktari angemtuma kufanyiwa vipimo vya magonjwa mbalimbali ambavyo vilikuwa hasi. Mwisho daktari alimshauri kufanya kipimo cha saratani ya damu. Siku hii Mbalu aliyotoka kusikiliza kesi yake mara ya mwisho ndiyo Mwenda alibainika kuwa na saratani ya damu daraja la tatu. Habari ile ilipokelewa kwa mshtuko mkubwa. Saratani kama inavyojulikana ni ugonjwa wa mauti. Mtu apatwapo na saratani ya aina yoyote huingia katika safari ya machweo. Mtu huishia kufyonzwa mali yake kukidhi matibabu na safari sizizo na hesabu za hospitali. Mwishowe hufa na kuwaacha waliompenda katika kinamasi cha uhawinde.

Mwenda alianzisha matibabu yake upesi katika hospitali ya Sifa. Hapa angepewa dawa za tiba-kemikali kuua seli za saratani na kupunguza uharibifu wake kwa uboho. Pia aliongezwa damu kila baada ya siku chache pamoja na kupewa dawa kadhaa. Mwenda alipata mshauri nasaha

aliyemsaidia kukabiliana na hofu na mawazo mengi. Siku zilivyokwenda ndivyo hali yake ilivyoimarika. Aliweza kuendelea na kazi yake ya kawaida japo si kama pale awali. Mkewe Doreen alijipa moyo mkuu. Alimfaa mumewe kwa kila lililohitajika. Alikuwa ameratibu kazi yake kwendana na majukumu mapya kwa Mwenda. Angefika ofisini kwake saa nne baada ya kuhakikisha mumewe yuko katika hali nzuri siku hiyo. Ilipobidi alikosekana kazini na kukaa na naye. Mwanao Majaliwa alikuwa darasa la tano. Alikuwa ameanza kugundua hali ya baba yake inabadilika pale alipomwona nyakati nyingine anakimbizwa hospitali na kulazwa kwa siku kadhaa. Doreen alichukua muda na mwanawe kumweleza kifupi ili kumwondolea hofu iliyokuwa bayana usoni.

Kwa upande wake Mwenda, japo alikuwa na maumivu alijikaza kutowakata moyo jamaa zake waliomzunguka. Alikuwa ameapa kupigana kiume bila kujihurumia. Akiwa katika hali ile alikuwa sana na hamu ya kujua walivyoendelea wagonjwa wengine wa saratani hii ya damu. Kwa msaada wa madaktari wake aliweza kuunda kikundi cha kimtandao cha *Myliod Leukamia Survivors* kulichowaunganisha wagonjwa wengi wa humu nchini na hata nchi za nje. Watu hawa walitiana shime na kubandilishana mawazo yaliyowasaidia kujielewa zaidi. Kundi hili lilifanya kila juhudi kuhamazisha umma juu ya saratani hii. Liliandaa warsha mbalimbali na kualika watalamu. Wavutini kikundi hiki kilitafiti na kusambaza matini muhimu katika nyanja hii.

Kutokana na kampeni zake hizi Mwenda ametambuliwa kama shujaa katika vita dhidi ya saratani na unyanyapaa unaoizunguka. Alipata mialiko si haba kutoka kwa hospitali na masharika mengi yaliyojihusisha na ugojwa huu kuwahutubia na kuwamotisha wagonjwa na waadhiriwa. Japo kazi hii ilikuwa ya ujima aliifurahia kwani alihisi msukumo asiouelewa wa kutoa nasaha ile. Alikuwa yule mtu wa ukipigwa mawe yachukue ujijengee kasri, ukipewa ndimu itumie kutengeneza sharubati. Kuishi kwendana na majaliwa. Si kunugunika kila leo juu ya hili au lile. Kwake maisha mema yalikuwa ya kushirikiana na kushirikishana.

Mwenge baba yake Mwenda hata hivyo alikuwa mashakani. Alikumbuka kemekali waliyoitumia kuhifadhi nyama pamoja na kivyere yake Mbalu. Alihofu sana. Ilikuwa na uwezo wa kusababisha saratani mbalimbali lakini kwa msukumo wa pesa na wadhifa ambao hakuupata hakujali wa kufa wala wa kupona. Sasa mwanawe wa kipekee alikuwa na saratani. Alipoketi pale sebuleni akakumbuka maongezi yake na Mbalu

miaka mingi iliyopita hotelini mzalendo pale alipomwambia, "…chagua unachotaka kama ni watu au pesa.'' Maneno haya yamekuja kubeba maana kwake baada ya miaka. Kila alipofikiria hali mwanawe maneno hayo yalikuja akilini kama mwangwi. Kweli mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu. Mkuki ulikuwa barabara mwilini mwa huyu afisaa mstaafu wa afya. Alidharau kina mimi na wewe hata akatukosea maana ya kuishi. Akacheka kilema bila mwao kuwa kingemfika. Mazidadi yake yote katika taaluma ile yalimpita akilini kama filamu. Vile familia ya Malele ilivyotaabika alipopiga mhuhuri kuharamishwa kwa leseni yake ya kazi. Wototo wake walivyoacha shule kwa kukosa karo na mkewe kujifia nyumbani kwa kukosa matibabu.

Mwenge alipokuwa katika usono kochini hali amefunga macho, akamwona mkewe Malele darini akiwa na majonzi belele. Machozi aliyolia yalimwangukia na kumchoma kama asidi. Alifungua macho upesi na kupitisha mikono usoni kama anayenawa. Mkewe amezoea kushtuka kwake kila mara usiku siku za hivi majuzi. "Si mimi! Si mimi niliyekuua ni yeye!'' Mara baada ya kulala kidogo alikurupuka na kuanza mbio kuelekea nje usiku. Tabia hii ilimshtua sana Jane mkewe. Alipomshauri waende hospitali alidai kuwa yeye hakuwa mgonjwa. Pia alishangaa ni nani huyu mumewe amewahi kuua na ambaye roho yake ilikuwa inamtaabisha. Hangedhubutu kumwuliza hilo kwani matokeo yake yangekuwa hasira tu.

Mwenge anakumbuka kama jana alivyopata kazi yake. Mbalu alipokuwa mbunge alikuwa kama mungu wa eneo bunge lake. Aliheshimika na kuogopwa na kila mtu. Alichotaka kilifanyika. Hata maafisa wa usalama walimwogopa na kumnyenyekea. Alilohusika hawangetia lao au wangejipata wamehamishiwa sehemu kame na hatari za nchi. Kushirikiana naye pia kungekuinua kwa viwango vya juu. Mwenge kwa kujua hili alimwendea mheshimiwa huyu. Ilikuwa nyakati za kampeni. Mbalu alimwahidi kazi ila kwanza angemfanyia kazi fulani ndogo. Kazi yenyewe hakuijua.

***

Dharura alikuwa amezidiwa na majukumu. Nyadhifa nyingi alizokuwa nazo kwa mtu wa kawaida ingekuwa vigumu kuzitekeleza ipasavyo. Alipofanya uteuzi wa moyoni aliwaendea wale wazee wa kanisa. Wakakaa kitako na kuzungumza. Ulikuwa wakati wa Dharura

kupokeza uongozi wa kanisa kwao. Wazee wale walikuwa na wingi wa shukrani. Walimwombea baraka chekwachekwa katika majukumu yake mapya ya utunzi wa misitu na rasilimali za kijadi.

Ili pia kupunguza mzigo wa kazi alijiuzulu kama mwanakamati wa hazina ya eneo bunge na vilevile kama kiongozi wa kile kikundi cha muugano wa wahubiri cha Tunu walichoanzisha na shehe Musa.

Ofisi yake ya *Balozi wa Mazingira wa Heri Njema* ilikuwa katika makao makuu ya UNEP jijini Takuja. Ratiba ya kazi yake ilibana kwelikweli. Alihitajika kusafirisafiri sana kote nchini akipigia upatu upanzi wa miti, uhifadhi wa misitu na matumizi aula ya rasilimani za kijadi. Alishirikiana na waimbaji na waigizaji mbalimbali tajika kutoa matini na jumbe alizoweka katika wavuti.

Kutokana na kazi yake ngumu angepatikana wikendi tu au wakati wa likizo. Mbaara kwa wakati mwingine ndiye angeenda kumtembelea kule Takuja alikokaa katika jumba la Karani.

Vyama mbalimbali vya kisiasa vilimtafuta kugombea kiti kwa tikiti yavyo kwani walijua alikuwa na ushawishi mkubwa na rekodi safi ya utendakazi. Kilichokuwa muhimu kwake wakati ule ni huduma katika nafasi aliyokuwa kwa wakati ule. Jibu hili halikuwakaa vyema walioswali ila hawakuwa nalo wangefanya kwani ule ulikuwa msimamo Dharura. Angalau kwa wakati ule.

Basil aliridhishwa sana na kazi ya mwanamke huyu hata akamshauri arudi shuleni apate elimu ya kutosha kwani kama ambavyo angemwambia, angesoma angekuwa kiongozi mashuhuri zaidi. Mara ya kwanza alichukulia kama utani ushauri ule ila mzungu huyu alimaanisha alichokisema. Hatimaye Dharura alijiunga na shule ya anuai kusomea maendeleo ya umma. Elimu ilikuwa kizingiti kikubwa kwake kuwania kiti hiki cha ugavana. Hata hivyo aliusiwa agombee kile cha mwakilishi wa kina mama.

Msitu wa Hidaya ulichukua sura mpya baada juhudi za miaka michache zilizokuwa na pandashuka si kiduchu. Mkono wa UNEP chini ya uongozi wa Basil ulikuwa dhahiri. Watu walioishi mizunguko ya msitu huu walikuwa na kila sababu ya kushukuru. Hewa ilianza kubandilika.

Ndege waliokuwa wametoroka sasa walianza kuonekana mmoja mmoja. Dharura aliyatazama haya kwa tabasamu ya moyoni.

***

Ukweli ni kama tiba chungu ya kipekee kwa ugonjwa unaolemaza mifumo ya kijamii. Familia nyingi zimevunjika kwa kukosa dawa hii. Vikundi vingi vya kijamii vimekufa kwa kukosa ukweli. Taasisi muhumu za kitaifa zimeyumbishwa kwa upungufu wa ukweli. Nikwambie mwenzangu, hakuna badili ya ukweli na kujaribu kuufunikia na kuuficha ni kama kule kutia kaa la moto mfukoni mwa nguo iliyo mwilini. Ukweli ni ukweli, huwe shubiri au halua, uwe nanga au ubele. Mwingine huwasha kama upupu na kung'ata hisia. Lakini bado ni ukweli. Ukweli ni ukweli tu. Mwanadamu naye ameibukia kuogopa ukweli kama mauti na kuishia kuhasirika ajabu. Wengi wameangamia. Nawe usijiamini. Fahamu kuwa mnyama mla kuku akipata kifaranga atamla pia. Zaidi ujue, maji pia humuua kiboko licha ya uzoefu wake wa kuogelea. Ni wazi kama meno ya ngiri pia adui wa swara ndiye yule wa mbogo. Ukiona mwenzako amechomwa kidole na mto nawe usitie chako pale kama wewe si juha. Huchukua hekima kutambua hekima.

Mwenge pale kituoni mwa kurekebishia akili aliendelea vizuri ila msukumo wa nadra na hatari ulimjaa kifuani. Alichotamani ni kumpuzika moyoni haijalishi kwa gharama gani. Alikuwa tayari kuyabusu madhara ya ukweli alioficha kwa miongo hata kama ulikuwa pilipili. Aliyaangalia maisha yake akaona yalivyojaa siri nyingi. Kama katika siri hapakuwa na amani aliona ajaribu ukweli. Alimwangalia mwanawe akaona adhabu ya majaliwa. Kuwa na mtoto mmoja hakukuwa kupanga uzazi, amejaribu kupata mwengine bila tija. Aliona nguvu kuu iliyopambana kufanya malipizi kwa uhaini wa mazidadi yake.

Miungu wa jua na mwezi walikuwa mashahidi dhidi yake katika kesi ya kitaswira. Mpaka aungame. Mashahidi hawa watokeapo kutoa ushaidi huwa ni ushahidi usiopingika. Ushahidi wao usipokubaliwa hao hao hugeuka mahakimu na kukuhukumu wenyewe. Hukumu hii huishi kusomwa vitabuni na kupitishwa kwa vizazi na vizazi kama simulizi. Unafaa ujue humuhumu duniani huishi nguvu ya nguvu. Nguvu zawazishi inayotoa kilichowekwa pasipostahili na kukirudisha mahali pake asili. Nguvu inayowapakulia waovu maovu na wema mema. Nguvu hii haijui mfalme au mtumwa, tajiri au maskini, msomi na asiye na kisomo.

Hufuata tu mawimbi ya haki sawia na yale ya redio ila yake hufika popote. Hii ni nguvu ya majaliwa.

Doreen alikuwa na ujio wa bamkwe nyumbani. Mkewe Mwenge hakuwa na kilichomtamanisha au kumfurahisha siku hizi. Hata alipopata habari kuwa mumewe alikuwa katika hali nzuri ya kurejea nyumbani hakusisimka. Dunia ilikuwa ishampa adha ya kutosha kujali la uhai wala la mauti. Isitoshe alikuwa na hofu kuhusu mwaliko wa mkewe Tufani na bwana Malele kumpokea mumewe. Watu hawa hawajawahi kutangamana wala kutagusana nao kwa karibu hapo awali. Ama afya yake Mwenge haijarudi kikamilifu? Hawa wawili ndio tu alioruhusu kumlaki pale nyumbani. Hata msiri wake Mbalu hakuwa na habari ya ujio wa rafiki yake mpaka siku iliyofuata.

Kwa upande wao, mkewe Tufani na Malele pia walikuwa na mengi ya kuuliza. Mkewe Tufani anavyokumbuka alitangamana na huyu Mwenge alipokuja kukagua mkahawa wake enzi hizo mumewe alikuwa katika siasa. Malele naye anakumbuka tu alivyomharamishia leseni yake ya kazi. Wote walivuta kumbukumbu hizi kutoka mbali. Waliongea machache kwani kila mtu alikuwa katika ulimwengu wake wa mawazo.

Mwenge alifika nyumbani mtu tufauti kabisa na aliyetoka pale kama miezi mingi iliyopita. Aliwaita wageni wake wakala na kuzungumza mengi mpaka pale aliwaomba waende faraghani.

Mwenda hakupata nafasi ya kumlaki baba yake kwani alikuwa ng’ambo kwa matibabu ila walikuwa wanawasiliana kwa simu. Kule aliendelea kupata nafuu na siku zilivyosonga ndivyo alivyojihisi kibonge. Alitazamia kurejelea kazi yake kama kawaida. Alikumbuka hakuwa amekamilisha kazi ya Jimmy na kumpigia kuomba radhi. Mwenda alimdata sana mkewe na Majaliwa mwanawe. Watu hawa walimtia nguvu na kuongoza dira ya alivyofaa kuishi.

Mkewe Mwenge kinyume na alivyotarajia, mumewe alikuwa amebadilika kabisa. Alikuwa mwingi wa shukrani kwa bwana Chumo aliyewavua katika shida ile kwa kumpeleka hospitali. Alionekana mchangamfu na mwepesi wa tabasamu. Kweli uzima wa mtu si mali bali amani ya moyoni.

Mbalu alipata fununu ya mkutano wa Mwenge mkewe Tufani na bwana Malele akafadhaika. Alimtembelea siku iliyofuata na kumpata Mwenge tofauti na aliyemjua kwa miongo sasa. Alimwambia mgeni wake kuwa hakuwa tayari kuhukumiwa na nadhiri zake. Vilevile akamnasihi afuate mkondo ule kama alitaka amani ya kudumu siku zile za uzee wake. “Ajihukumuye hahukumiwi,’’ alimwambia Mbalu.

Mbalu alikuwa ameanza kuzidiwa na uzee. Mwili sasa ulianza kulegea, macho nayo hayangeona mbali. Hangekosa bakora mkononi. Siku hii hakutaka kuendeshwa na dereva wake kwani hakutaka mtu wa kundoea maongezi yake na Mwenge. Kinyume na ilivyokuwa ada yao kuketi sebuleni, wazee hawa walifanyia mazungumzo yao garini mwa Mbalu nje ya lango la boma.

“Mwenzangu una nguvu. Mimi siwezi kuwatazama kwa macho niliowadhulumu kuwaomba msamaha ila katika wasia wangu nimewapa fidia ya kiasi fulani cha pesa. Hilo ndilo limeniweka nisipatwe na yaliyokupata. Kwa kweli mali, vyeo na jina kubwa hubadilisha mtu akajiona kiumbe mwenye nguvu kuliko wengine. Bila utu hivyo vyote ni ubatili. Ebu nione leo, ninatembelea mkongonjo ambao Malele anatembelea, nikilia mguu analia mgongo.  Tumeyaona kwa macho yetu, tuwarithishe wana wetu yaliyo mema.’’

Kwa hayo marafiki hawa waliagana bila kujua ilikuwa buriani. Mbalu alipotoka pale kwa Mwenge giza lilikuwa limeingia, rai za mwanawe Doreen kumpeleka nyumbani hazikufua dafu*. “Once a driver always a driver!’’* Mbalu alisema huku akiliwasha gari lake na kuwatifulia vumbi wenyeji wake walioachwa wakicheka. Alipokaribia daraja kuu la Mto Kalawa alipatana na pikipiki iliyotoka ule upande mwingine na mwangaza wa taa yake ukayapofusha macho ya Mbalu dhaifu. Kufumba na kufumbua kishindo kilisikika mtoni ambao ulikuwa umefurika furifuri kwa mvua iliyokuwa imenyesha usiku wa kuamkia hio siku. Mvua hii ilipokelewa kwa shangwe na matumaini ya mavuno baada ya kipindi kirefu cha kiangazi. Watu walipokea habari za kifo cha Mbalu kwa mshtuko mkubwa. Mahali papo hapo ndipo Mwenge alipomtumbukiza Tufani miaka mingi iliyopita kwa amri yake Mbalu.

Lilikuwa ni wingu jingine la huzuni katika familia ya aliyekuwa mheshimiwa. Jamaa zake waliposoma wasia wa mwendazake walizidi kushangaa. Ni vipi watu wasiokuwa wa familia wangerithishwa milioni

moja kila mtu? Katika shangaashangaa hizi ndipo Mwenge alipowaambia kuwa rafiki yake aliridhia hivyo kufidia makosa fulani aliyowatendea watu hao. Kando na hayo, Katika wasia wake Mbalu alirai kusiwepo na kupiga siasa katika mazishi yake. Aidha, katika risala za rambirambi, alipenda kusiwe na mtu wa kumsifu au kusifu maisha yake. Aliagiza yasomwe au yatajwe aliyofanya mabaya tu.

# Sura ya kumi na Tatu

Penzi kuu hugeuka chuki kuu kama usaliti utajikita kati. Mara nyingi hili huleta beluwa ikawapiku watatuzi. Paka wako akikunyang'anya mnofu mkononi jua huyo si paka tena ila pakashume, mchukulie hatua. Tia akilini pia mgeni akistarehe sana kwako, kwake kumepungukiwa kitu. Jossy ni muda sasa hawaonani uso kwa macho na dada yake. Sussy alipoolewa na mhasibu mwenzake aliyekuwa akifanya kazi na benki kuu ya nchi ilimbidi aombe uhamisho ili kumkaribia mumewe. Kwa sadfa ikawa wamekaribiana na alipoishi dada yake Jossy. Ilikuwa nafuu sana kwao kwani ilifupisha masafa waliyopiga kutembeleana dada hawa waliopendana sana.

Baada ya uchumba wa Mike kugonga mwamba, Jossy amejaribu mahusiano na wanaume kadhaa yakifeli. Mara huyu alikuwa wa mapato ya chini kuliko yake. Mara huyo alikuwa mnene kama trekta. Mara yule cheusi mpingo. Aliwachagua na kuwachuja vijana wengi waliomjia kwa urafiki. Almuradi kila barobaro alikuwa na kasoro isiyovumilika. Kidogokidogo waliomjia wakapungua na mwishowe akawa hata salamu hapati. Alizinunua.

Alizidisha mapambo na kubadilisha mitindo yake ya nywele kila mara. Mavazi yake aali yangechukuana vyema na mapambo yale. Akanywa tembe fulani zilizofanya ngozi yake iwe kama ya mzungu. Bado hali ikawa ileile. Miaka nayo ilikuwa inasonga upesi bila huruma na kuimbe huyu. Alipojaribu kuwafuatilia aliowachuja kwa kutokuwa na hiki au kile akagundua walikuwa miongoni mwa matajiri ibuka mjini na bara. Wengine wamepata jiko na walikuwa na watoto wakubwa. Bila shaka kiherehere kilianza kumnyemelea na kumnyatianyatia jinsi chui afanyiavyo windo lake. Majuto nayo si wajua ni mjukuu?

Mmoja wa aliowadharau ni Ojwang. Ojwang kulingana na mizani yake alikuwa na kila alichokichukia. Kwanza, Ojwang wakati huo alikuwa hana kazi. Siku moja alimwambia, "Mara ngapi nimekuambia sina haja na kitu kifupi kinene cheusi na mviringo kama gurudumu la lori? Tafuta wa tabaka lako ndugu. *Am not a low life like you.*" Ojwang alihisi fundo kubwa na kavu kooni asiweze kusema lolote. Akainamisha kichwa akajiendia zake. Jambo hili halikumpendeza Sussy. Alimkaripia.

Sussy katika shughuli zake kazini siku moja Ojwang alikuja akisaka kazi pale kwao. Akatumia fursa ile kuomba msamaha kwa niaba ya mwenzake. Hapo wakajenga mhalaka wa kudumu. Alipopata kazi katika benki kuu Ojwang alimwarifu na wote walifurahia. Kwa utendakazi wake mwema kijana huyu alipanda daraja haraka akawa mmoja wa mameneja pale. Uhusiano wao na Sussy ulizaa penzi na wakawa mume na mke.

Hapo ndipo Sussy alipohamia karibu naye na karibu pia na dada yake. Kufikia wakati huu Jossy hakuwa na mwenza. Upweke ulianza kumparamia pale wenzake wa rika lake walipata nyumba na kuanza shughuli za ulezi. Majuto ni mjukuu huja baadaye. Aliumia kuona jinsi maisha ya Ojwang na nduguye yalivyotebwereka. Angefanyaje na hayazoleki yamwagikapo?

Hangekaa sana bila kupita pale kwa Sussy. Wakati mwingine angepitisha wikendi yote pale. Ojwang alikuwa mwanamume mcheshi na kila alipokuwa watu waliumia mbavu kwa vicheko. Tabia hii ilimleta Jossy karibu sana shauri alipenda matani yake.

Siku moja hii asubuhi, Sussy alimpeleka mwanawe wa tatu hospitalini baada ya kulala kulia usiku kucha. Kwa kuwa ilikuwa wikendi Ojwang hakuenda kazini mapema, Jossy naye alikuwa likizo ndogo, akawa alikuwa pale kwa dada yake. Hawa wawili waliachwa nyumbani. Kumbe Jossy ameishi kutafuta fursa kama hii kumchanganya Ojwang. Alipotengeneza chai alitia dawa fulani katika kikombe cha bwana wa nyumba na muda si muda Ojwang akapandwa na jazba za kiume. Yakawa ya kuwa. Baada muda Ojwang alianza kuhisi kuzungunzungu na mara akaanguka. Jossy kwa mshtuko hakukumbuka kumwarifu dada yake ila alimkimbiza hospitalini. Hospitali aliyompeleka ni ileile Sussy aliyompeleka mtoto. Wakabanana pale kila mtu ameshtuka. Baada ya uchunguzi ilibainika kuwa Ojwang alikuwa amepewa dawa ya kusisimua hisia. Alikuja kuyaeleza mwenyewe alipoziduka.

Kufikia hapo Jossy na Sussy wakawa kuku na mwewe. Hakuna aliyekivuka kisingiti cha mlango wake akienda kwa mwenzake. Cha kuumiza zaidi ni kule kwa Jossy kupata mtoto kutokana na tendo lile. Mtoto huyu aliishi kuwa kumbukumbu la kudumu na saruji iliyounga uhasama kati yao. Mama yao amejaribu kuwaleta pamoja bila mafanikio.

Ilifika wakati akasema kwamba dawa madhubuti ya tukio lolote ni mapito ya muda.

Mtafaruku huu ulimpelekea Kanini kukumbuka Hasani na maasi aliyomtendea wakiwa na yule mkuu wa polisi. Alijiona mjinga aliyeongozwa na ashiki za ujana. Kwa kiasi alilaumu kifo cha wazazi wake katika umri wake mdogo. Labda wangalikuwepo wangalimpa makuzi yaliyofaa na angaliepukana na ufito wa mama ulimwengu uliompa sasa wana wasibaba na ugonjwa wa kuuguza.

Nchi ilikuwa bado inapitia kipindi kigumu cha kiuchumi na jambo hili lilisababisha ukosefu wa huduma muhimu kwa raia wake. Mojawapo wa huduma hii ilikuwa ile ya matibabu na dawa bila malipo kwa waathiriwa wa ukimwi. Hospitali nyingi zilikosa dawa hii muhimu, wagonjwa nao wakawa mashakani. Ilimbidi Kanini kwenda kutafuta dawa hizi muhimu kule alikofanya kazi mwanawe Jossy. Mwana akamwona mamaye akingia na kutoka sehemu ya V.C.T. Kwa sababu ya zogo lao na dada yake mama bado alikuwa na hasira na mwana huyu na hakutaka mengi naye. Baada ya salamu fupi nusu rasmi alishika njia akarudi nyumbani. Jossy hakutaka kumwuliza alichojia pale japo alikuwa na shauku ya kujua. Akamwendea yule mhudumu wa pale aliyekuwa pia rafikiye na kabla hata hajapata kuuliza lolote alijibiwa na faili ya mama mtu iliyokuwa pale mezani.

***

Jimmy alikuwa na watoto watatu na maisha yao yalikuwa na wingi wa furaha japo bado aliuhuzunikia kifo cha ghafla cha baba yake baada ya miaka michache ya kumjua. Hata hivyo alikuwa na kila la kushukuru kwa muda walioishi. Mercy alikuwa kama mama halisi. Alimpenda na kumthamini.

Alikumbuka siku Jamila alipojifungua mtoto wao wa pili msichana alivyopokea habari ile kwa furaha na kusema alikuwa ‘amezaliwa tena.’ Hii ni kwa sababu mtoto huyu angeitwa jina lake kulingana ni mila. Mercy alifunga safari mpaka Takuja kumpa jina. Aliwabebea kila alichokiona kizuri bara. Licha ya umri mpevu alionekana mwenye nguvu na mchangafu labda kutoka na kazi yake katika shule aliyofungua kuhudumia watoto walemavu. Shule hii ilikuwa kama

kumbukizi ya mwanawe Dan. Kazi ya shule hii yake ilikuwa imemchukua mwili na roho.

***

Mbaara ni jina kubwa Pemba. Biashara ilimkubali. Kila alichokianzisha kilifana. Kilichovuma zaidi ni duka lake la vifaa vya ujenzi. Ndiye aliyeuza kwa bei nafuu kuliko maduka mengine ya aina hii. Kutokana na hilo, wateja walitumana oda kutoka mbali na naye angewapelekea kwa gharama yake. Sasa alikuwa na malori kadhaa ya usafirishaji wa aina hii. Dharura aliporudiana na Mbaara hakuamini kiumbe huyu anagebadilika kiasi hiki. Kila aliporudi kutoka kwa safari zake nyingi alipata mabadiliko. Mwanaume huyu anaheshimika sana siku hizi kinyume na hapo awali alipokuwa mpenzi wa chupa jeusi. Bayana, huku ni kule kuwa tai mfuata simba; hakosi mlo. Mbaara wa leo ni tunda la kushirikiana na watu wafaao.

Dharura alizidi kupiga msasa kampeni zake za kuwaniana kiti cha mwakilishi wa kina mama. Kulingana na takwimu, hana ushindani kwani mshindani wake hakuwa na wasifu mzuri kutokana na ushirikiano wake na yule gavana wa awali. Tena hamna la haja alilowafanyia watu alipokuwa kitini isipokuwa kule kujipondoapondoa na kubadilishabadilisha magari kama nguo. Alionekana nadra na kwa kipindi kifupi. Watu wake walimwona runingani na kusoma mitandaoni akisema kuhusu jambo hili au lile. Juzi alinukuliwa akisema vile mshahara wa wawakilishi wa wanawake ulikuwa mdogo na ulistahili kuongezwa. Aidha, hakuwa mfano bora kwa vijana wa kike kwani alitumia vijiko vingi kulia chakula kimoja sahanini. Baada ya kura Dharura aliibuka mshindi.

Dharura alimwahidi bosi wake Basil aliyekuwa mshauri wake pia kwamba hangelegeza kamba kutetea maliasili. Pia alimwahidi kuwasilisha miswada bungeni inayolenga nyanja hii. Basil alimpongeza sana kwa ushidi wake. Dharura hakuhitajika kujiusulu kutoka kwa wadhifa wake kama balozi wa heri njema kwani kuchaguliwa kwake kama mwakilishi wa kina mama kuliongeza umaarufu wake uliohitajika kuvutia watu wengi zaidi nchini.

Kwa upande wake, Nafuu alijivunia mama yake. Alimwona kama dira ya kufuata. Ukimpambaja aliyepaka marashi hunukia marashi pia.

Nafuu alikuwa akisimamia vikundi vyote vya wanafunzi wanamazingira katika Tunu. Kila siku ya kuadhimisha mazingira kila mwaka vikundi vyote vilikusanyika katika shule moja na kupanda miti. Shule nyingi sasa zilipata sura mpya. Vile vile yeye na walimu wengine wasimamizi wa kila shule huandaa semina kuwahamazisha wanafunzi kando na kuandaa mashidano ya insha juu ya mazingira. Mwandishi bora angetuzwa kwa zawadi kemkem kando na kupewa miche anuai kwenda kupanda kwao nyumbani. Kupitia mama yake ameweza kumwalika Basil na wananamazingira wengi mashuhuri kuongoza semina hizi. Amewahi pia kumwalika mama mwenyewe. Mama alitumia maarifa ya mwanawe kuwafikia wanafunzi shuleni na vyuoni kupitia walimu. Katika mashindano ya muziki na maigizo pia amekuwa akifadhili ubunifu katika daraja lolote uliolenga utunzaji wa mazingira.

***

Mwema na gavana pale jela walikuwa kati ya walioheshimika miongoni mwa wafungwa wa Kimwilu. Wawili hawa waliishi kufaana pale kama ndugu. Siku ile gavana alipatwa na shida ya kupumua Mwema alihofu sana. Alikimbia kumwarifu askari aliyekuwa zamu kwenye lango la bweni usiku ule. Gavana King’ori alikimbizwa hospitali na kutibiwa. Mchana uliotangulia usiku ule yeye na wengine walishida shambani kulima. Vumbi ndiyo iliyompa gavana mzio kinyume na habari zilizosambaa kwamba wafungwa wengi wa Kimwilu walikuwa na kachina.

Marafiki hawa wawili walikuwa na siku chache wawe huru huria. Hili jambo liliwachangamsha sana. Walitamani wangeharakisha muda. Lakini hata hivyo Mwema kwa kiasi alikuwa na shaka. Angerudi wapi? Watu watamwamini tena kama kasisi wao. Wasipomkubali angefanya nini ikikumbukwa kwamba kanisa na boma yake viko katika kiwanja kimoja. Jakamoyo hili alimmwagia gavana aliyemsikiliza kwa huruma. Mwema hakuwa na familia. Familia yake ilivunjika mara ilipoumbika. Mwema, Kama alivyomsimulia mwandani wake alikuwa na mke mrembo sana kule kwao magharibi mwa nchi. Alikuwa ameoa tu pindi alivyomaliza kidato cha nne. Hili lilitokana na shinikizo la baba mzazi aliyekuwa na shauku ya kuona mjukuu wa mwanawe wa kipekee wa kiume miongoni mwa wasichana watatu, kabla ya mauko yake aliyoyaona

usoni kila uchao kutokana na ugonjwa wa kisukari uliomsumbua. Mama yake mzazi alikuwa mwalimu wa sekondari katika shule moja pale jimboni. Mwema hakujua amani katika familia ni nini. Mama yake alikuwa simba katika ile boma jambo lililomnyima baba yake nafasi kabisa. Vituko vya mama vilianza tu baada ya baba yake kuachishwa kazi katika shirika la reli. Nchi ilipolemewa na misukosuko ya kuichumi kutokana na ule ugonjwa wa kachina, iliamua kupunguza wafanyakazi katika mashirika mbalimbali ili kumudu gharama ya mishahara. Baba yake Barasa kama lilivyokuwa jina lake Mwema halisi, alikuwa miongoni mwa wengi waliotemwa nje.

Maisha ya mzee huyu yakachukua mkondo mwingine alipokosa kazi. Mawazo mengi nayo yakamshika mkono na kumwelekeza kwa chupa jeusi; akawa mlevi mwenye jina lake. Ulevi huu kulingana na wototo wake ulichangiwa na kelele cha mama kisichokoma. Alimzomea na kumkaripia mbele yao akimwambia vile yeye alivyoshindwa na majukumu yake kama mwanaume katika familia. Kukafika wakati akaanza kumtembezea mzee mkono alipokuja mlevi na kumnyima chakula. Mzee huyu ilipofika hapo akawa na rafiki mmoja tu; pombe.

Watoto wake walipojaribu kumtetea walitishiwa kutolipiwa karo na kufukuzwa nyumbani wakajikunja. Barasa alipokuwa kidato cha tatu mama yake akapata mtoto mvulana, baba mtu alipotaka kujua mengi alipigwa na mkewe ajabu. Mzee hakuwa na wa kuambia kwa kuhofia unyanyapaa uliohusishwa na mwanamume kupigwa na mkewe. Alilia machozi yakienda tumboni jambo linalokisiwa kumletea shinizo la damu.

Siku moja baba yake Mwema akamwita faraghani. Akamweleza jinsi alivyohisi hana tena tamaa ya kuishi. Ugonjwa nao ulimlemea mno. Alimrai apate jiko haraka iwezekanavyo ili ampe mjukuu kabla ya kengele ya ziraili kukirizwa. Barasa alipofanya mtihani wake wa kidato cha nne alienda nyumbani kusubiri matokeo mara mbili. Alishampa mwanafunzi mwenzake ujauzito. Alimchukua akampeleka nyumbani. Hivyo ndivyo Mwema alivyopata familia. Mama akamguezia mwanawe na mkazamwana ukali, nyumbani pakawa hapakaliki. Mkewe Mwema angepewa kazi za sulubu pale bila kuzingatia hali yake. Hakuweza kufikia miezi tisa. Alijifungua njiti ila kwa kudura zake mungu kivulana hiki kikaishi. Baba yake Mwema hakuishi sana baada ya kumwona huyu mjukuu. Mama aliendealea kuharibu boma lake kwa viganja vyake mpaka

pale watoto wake walipoamua kumtoroka mmoja baada ya mwengine akabaki na yule mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa.

Mwema na mkewe walitorokea Takuja mtaa wa Makesi. Alifanya vibarua vya kila aina ili aweze kuikidhi familia yake changa. Alitoka siku moja kama kawaida kusaka riziki. Kurudi jioni akapata kijibarua mezani

*Kwa mpenzi Barasa*

*Laiti ningekuwa na subira zaidi ningekaa ila kwa sasa sina hata chembe. Nimeona unavyojikaza na kumenyeka kutushughulikia kimahitaji hapa mjini. Umejikaza kama baba na bwana. Siwezi kuendelea kukuumiza zaidi mpenzi. Moyo wangu huwezi kuweka tena siri. Mtoto huyu si wako. Ni wa aliyekuwa mwalimu wetu wa Hisabati. Hata hivyo sikumpenda. Nilikupenda wewe ila sasa nimegundua kuwa penzi si pato. Naumia kufanya uamuzi huu ila naona nikupunguzie mzingo wa kulea mwana si wako.*

*Mkeo mpenzi.*

Mwema alihisi mwiba mkali ukimchoma moyoni bila simile. Alihisi usaliti kila pande. Alichukia mwanamke huyu na wote kama mama yake. Kweli nyoka ni nyoka na kila nyoka na sumuye. Alichukia usuli wake. Akajichukia mwenyewe kwa kufanyika mjinga. Akaamua kujimaliza. Hakuwa na lolote la kutazamia. Masomoni hakufua dafu, nyumbani kuliwaka moto, mkewe naye huyu amemfyonza nguvu ya ujana wake na kupuruka kama kipungu. Kwa ule ujira aliopata siku ile aliingia kwenye baa na kupiga mtindi kwelikweli. Ni pale ambapo wazo la kuanzisha kanisa lilipotoka na kusahau lile la kujiua. Aliketi nyuma ila karibu na wanaume wawili waliokuwa wakizungumza kwa sauti za chinichini lakini ya kutosha kusikika na aliyekuwa karibu. Alipofutilia mazungumzo hayo aligundua kuwa walikuwa na nia ya kufungua kanisa kama biashara. Aliwasikia wakiorodhesha mbinu za kuwavuta waumini na zile za kuwafanya watoe sadaka nono. Watu hawa walionekana kutojali lolote. Barasa alijilinganisha nao na kuona msabaha mkubwa. Yeye pale alipokuwa alikuwa na sumu mfukoni aliyopanga kunywa baada ya kulewa kabisa. Mtu asiyehofia kifo anawezaje kuhofia laana ya waumini isiyo na uwezo wa kuua. Laana gani tena na hawa waumini ndio kina mama yake na mkewe waliofanya maasi kupiku viwango vya msamaha. Hawa waumini ndio waliowanyanganya mayatima mali na

kuwafukuza wajane ili kutwaa mali waliyorithi kutoka kwa mabwana zao. Mmh, watu hawa ndio wenye roho chafu na jeusi sizizokombolewa kwa maombi ya siku moja. Labda ndio maana hawakosi kanisani.

Barasa aliamua kwenda mbali asikojulikana na kujaribia maisha tena. Jina nalo akabadilisha lisimkumbushe mama aliyempa wala usuli. Akajiita Mwema. Alijipata Tunu. Baada ya kufanya vibarua hapa na pale alipata mtaji wa kukondi vyombo vya mziki na kumlipa mwenye kuvipiga kila Jumapili. Chumba cha kulala alichokondi ndicho angekibadilisha kanisa Jumapili. Angetoa vyombo vyote nje na kupanga viti, jioni angevirudisha tena. Kwa miezi michache baadaye aliweza kukondi kiwanja na kuweka hema na kulikahamishia kanisa pale. Urafiki wake na mwenye kiwanja hiki ambaye pia alikuwa mshiriki wake kulipelekea kumwuuzia ardhi ile.

Baada ya gavana kusikiliza kadhia zote za mwenzake, alimtuliza na kumwahidi mkono wake. Aidha alimjuvya kwamba alikuwa na haki ya ardhi yake yalipokuwa makanisa yote matatu kwa kuwa alikuwa na hati miliki. Mwema hakutaka kuzua hisia kali miongoni mwa waumini. Alikuwa radhi awaachie vyote kama hiyo ingekuwa fidia tosha kwa maasi aliyowatenda miaka ile. Alihofu zaidi kwa sababu Dharura alikuwa sasa mwanasiasa mwenye ushawishi mkubwa. Watu hawa wawili wangejitania kwa kusema kuwa wote wawili walikuwa wakiuguza machungu ya kiboko cha Dharura.

Wiki mbili kabla ya siku yao ya kutoka, kulikuja mfungwa mmoja kijana wa takriban miaka ishirini na miwili hivi. Mrefu kwa kimo na mweusi. Kwa kumwangalia alikuwa mtu mwenye woga mwingi. Kwa siku tatu sasa alikuwa hajala wala kunywa kitu. Alizidi kuwa dhaifu ila hakuonekana kujihurumia. Mtu ambaye angewezana na mtu kama huyu ni marehemu Masila. Sasa mwili wake ulikuwa unaburudisha mchwa futi sita chini ya ardhi na roho yake kama wavyotania wenzake gerezani, ilikuwa imehamishiwa jela la mbinguni.

Gavana akamwendea yule kijana yule na kuzungumza naye. Baada ya muda kijana akafungua moyo na kuwasimulia yaliyomleta pale. Nyongesa kama lilivyokuwa jina lake alikuwa amemwuua mama yake mzazi baada ya mzozo wa muda.

Ilitokea kwamba Nyongesa hajapata kumwona baba ama ndugu yake tangu azaliwe ila aliishi kuambiwa kwamba alikuwa na kaka mmoja na dada wawili. Wadaku wa habari walimjuvya kwamba mama yake ndiye aliyewafukuza nyumbani kwa kisirani chake. Juhudi za kutaka kujua kutoka kwa mama mzazi zilipatana na ukali wa ajabu. Alikuwa mpweke na asiyeruhusiwa kutangamana na watu isipokuwa tu shuleni. Nyongesa katika kung'ang'ana kujitambua na kusaka uhuru wake alipatana na vijana watoro waliomfunza matumizi ya vileo mbalimbali. Aidha, walimwingiza katika uchopozi na wizi wa vitu vidogovidogo kama kuku. Bila kutambua alijipata katika genge sugu lililoiba mpaka kwa maduka makuu na mabenki kutumia bunduki pindi tu alipomaliza kidato cha nne. Kijana huyu aliondokea kuwa mwenye shabaha kuu. Hangelenga akose hivyo akawa kiungo muhimu kwa genge lile. Alipanda daraja mpaka akawa komanda pale komanda wao alipopatwa na shaba ya polisi. Aliamini katika kuubusu mkono asioweza kuukata. Alijenga mhalaka na baadhi ya askari kurahisisha oparesheni za kundi lake. Kila baada ya oparesheni angewapelekea wale askari wakora kifumba macho. Aliposhikwa mmoja wa vijana wake alipiga simu tu na kuachiliwa. Alianza biashara pia ya kuuza bunduki alizoletewa na haohao maafisa kutoka Sudan kusini. Magenge yenye silaha hatari yakajaa mtaani. Watu walihangaishwa, mabasi yalitekwa na abiria kuporwa. Maduka yalivunjwa, magari yaliibwa mchana peupe maegeshoni. Lalama za raia kwa maafisa wa polisi ziliambulia patu.

Mama mtu alipojua kuwa kijana wake ndiye kiongozi wa genge hili sugu akamfukuza nyumbani. Machungu ya tabia ya mtoto huyu aliyekuwa chanzo cha kupotea kwa wanawe wengine nyumbani kulimzidi mama huyu. Kweli Nyongesa alikuwa sura kamili ya mwanaharamu kwa matendo yake haramu. Anakumbuka alivyompenda zaidi ya wale wengine. Alimchukia sasa na kuwona kama bundi. Siku moja, Nyongesa alikuja amekimbizwa na polisi wa *Fyling Squad* akaingia nyumbani. Maafisa wale walizingira boma la mwalimu yule na msako ukaanza. Mama mtu alishtukia kupatikana kwa bunduki kadhaa zimechimbiwa katika nyumba ya kijana huyu. Nyongesa pia alikuwa analala kwa nyumba yake ile kila siku alipokuwa karibu. Alikuwa amechimba shimo kutoka mahali shambani karibu na uzio mpaka kwa nyumba yake. Hivyo ndivyo alivyoweza kuhifadhi bunduki zake mle. Alipokamatwa mama alifurahia na kuwaomba wale askari wahakikishe amefungwa miaka mingi iwezekanavyo.

Jambo hili lilimwuuma mwanawe na akaapa kumpa funzo akifanikiwa kutoka hata kwa bondi. Kweli mwenye pesa ndiye mwenye nyenzo. Nyongesa alitumia wale askari wenye zile silaha kuongea vizuri na wale wenzao na punde aliachiliwa hata kabla ya kufikishwa kortini.

Mama alishtukia jioni moja siku mbili baadaye taa ya nyumba ya kijana wake imewaka. Kwenda kuangalia alimpata Nyongesa pale ametulia. Mauti ikamsukuma mama. Akaanza kumkaripia akimwambia vile amempaka tope pande zote. Vile alihujumu heshima yake kama mwalimu mkuu wa shule ya kitaifa. Vile alijutia kumzaa kisirani kama yeye aliyechangia kutorokwa na wanawe. Kwa hili Nyongesa hangestahimili tena. Alikuwa amevuta vya kuvutwa akanywa vya kunywewa na kijidunga vya kudungwa. Alikuwa amezoea kuitwa kisirani. Alishangaa mama alivyokubali kuzaa kisirani. Na kama yeye alikuwa kisirani basi yeye kama mzazi alikuwa zaidi kwani mdimu huzaa ndimu. Vilevile hakuona alivyowafukuza ndugu zake ambao hajawahi hata kuwaona. Akafikia bastola yake na bila kupigwa na moyo akamlenga mama.

Muda huu wote Mwema alikuwa ameyatunga macho ukutani pasi na neno mpaka pale aliposikia Nyogesa akisema alikuwa amemuua mama yake. Akashtuka kama aliyekuwa usingizini.

“Eti ulisema unaitwa Nyongesa kutoka Magharibi mwa nchi?’’ alimwuliza yule kijana. “Naam.’’ Akajibu. “Mama yako alikuwa mwalimu na alikuwa amewafukuza ndugu zako ambao hukuwajua?’’ “Naam. Kwa nini umeshtuka bwana mkubwa?’’ “Dunia zungu zunguka! Gavana huyu ni ndugu yangu haki ya Mungu!’’

Ndugu wawili wakaunganishwa na uhalifu jela la Kimwilu. Wakasimuliana mengi. Mwema alihuzunika kwamba mama yake hakuwepo tena. Alikuwa ameapa kuwasaka mama na dada zake atakapotoka pale. Aidhuru japo yadhuru.

La kushangaza kwa gavana na Mwema ni ile ziara ya Dharura kimwilu siku tatu kabla ya kutoka kwao. Walishtukia kuambiwa kwamba walikuwa na mgeni mashuhuri. Alipowaona alisimama na kuwakimbilia kwa mikono wazi. Mwema alikaramka kwa hili ila gavana. Alihofu ni mbinu moja tu ya kujiuza kisiasa ila walipoongea kwa mapana na marefu akausoma moyo wa mwanamke yule. Aliwaeleza kuwa alikuwa

ameandaa karamu kubwa ya makaribisho yao na kwamba wangekujiwa pale kwa msafara wa magari ya wanatunu na waumini wa Mwema. Alimweleza Mwema kwamba waumini wake walikuwa bado wanampenda. Alikuwa na jukumu kubwa la kujiaminisha upya.

## Sura ya kumi na Nne

Shule ya upili Tusomeni ni shule kubwa mashiriki mwa nchi. Shule hii ya mseto ina wanafunzi yamkini elfu mbili na mia tano. Kando na idadi hii kubwa Tusomeni nzuri ni kimasomo. Daima haikukosekana miongoni mwa shule kumi bora kitaifa. Nidhamu yake pia ilikuwa kiwango cha juu. Alipokuwa shuleni hata yale majibwa makubwa ya shule hii hayangebweka bila ruhusa wake. Walimu walionekana mbioni kila walipotoka darasa hili kwenda jingine. Kengele ilipoguswa tu shughuli zilibadilika mara moja kuendana na ratiba. Uzembe pale lilikuwa neno geni. Mabawabu walionekana ange kama wanajeshi vitani. Hungeingia shuleni bila sababu maalumu. Mkuu huyu alikuwa na kamera zake kila mahali isipokuwa msalani tu. Alipoketi pale ofisini mwake aliona kila sehemu ya shule. Amewahi siku moja kumpigia simu mpishi aliyemwona akificha nyama za kuwapikia wanafunzi kwenye koti lake na kumwamuru azitoe akiwa palepale ofisini. Mbunge wa eneo hili pia amewahi kupata shida ya kuingia shuleni alipofika bila mwaliko wala taarifa. Ilibidi akaguliwe kama raia wa kawaida na kusubiri mpaka Moto aliyekuwa mwalimu wa Hisabati kumaliza vipindi vyake viwili vya kidato cha tatu.

Kutokana na sifa za shule na za mwalimu huyu, shule hii ilikuwa tamanio la wazazi wengi kwa wanao. Wanafunzi walitoka kila pembe ya nchi kuja kusomea Tusomeni. Mabweni ya shule hii yalikuwa mengi na ya ghorofa. Mabweni nadhifu ya kisasa.

Michezoni, Tusomeni haikuzipa shule nyingine nafasi pia. Moto aliwatafuta wakufunzi wa kila mchezo kuwafunza wanafunzi. Kwa kawaida kinolewacho hupata. Mchezo wa raga uliokuwa uraibu wake, ulikuwa wa kiwango cha kimataifa. Kwa sasa shule hii ilikuwa na kikombe cha timu bora cha Afrika mashariki na kati.

Warsame mtoto wa Amina Said alikuwa kidato cha tatu katika shule hii adhamu. Amina alikuwa mama mwenye chake. Alihamia kaskazini mashariki mwa nchi angali msichana mdogo kusaka riziki. Alikuwa ametoroka ukali wa siku zote wa aliyeita mama. Alipofika

maeneo yale akawa yaya katika familia ya bwana Omar, tajiri mkubwa eneo lile. Utendakazi wa msichana huyu ulimridhisha kupita kiwango hata alimpendekeza kwa Said kifungua mimba wake katika ndoa. Said naye hakufanya ajizi, akamwoa yule msichana. Alivua jina Risper Apondi akawa Amina Said. Kifunguamimba wake Amina ni huyu Warsame. Kijana mwerevu ajabu na mwenye kijituma kwa kila alilolitia mkononi. Zaidi, mwana huyu aliumbika; mtanashati ajabu kando na kimo na tambo lake la wastani.

Nasieko Wafula alikuwa darasa moja na kijana huyu wa Kisomali. Walikuwa na mengi yaliyowatagusanisha. Kando na kuwa walikuwa na wamemiliki nambari za kwanza mbili darasani mwao, walikuwa vijiranja. Tena, walikuwa katika kundi moja la Hisabati. Kwa njia isiyoeleweka roho za vijana hawa wawili zilivutana. Siku moja Nasieko alipogonjeka ghafla na kukimbizwa hospitali iliyokuwa karibu, Warsame hakula chakula hata alipopata ruhusa wa kutembelea. Japo walimu walitambua hilo hawakuliona la mno kwa sababu walijua ulikuwa urafiki wenye vipimo kubalika pale.

Warsame hakuona ugumu wa kumtambulisha rafiki yake kwa wazazi wake walipomtembelea. Lakini kulikuwa na mtu mmoja aliyeumwa na urafiki huu. Momanyi, mtoto wa mwalimu mkuu aliyekuwa kidato hicho cha tatu ila darasa tofauti.

Alimpenda Nasieko kama rafiki ila aliona ni kana kwamba alimpuuza kwa sababu ya ukaribu wake na Warsame. Alitafuta nafasi yake kwa msichana huyu akapata ile ya kimasomo tu kinyume na matarajio yake. Momanyi akaamua kutumia marafiki zake Nasieko wa karibu Rose na Kanene. Hawa wawili nao wapeleka ujumbe uliomfikia Warsame. Kijana huyu akajitwika jukumu la kumwona Momanyi kwa neno moja au mawili. Momanyi naye alijihisi bosi kwa sababu za kawaida. Alikuwa mtoto wa mwalimkuu. Mazungumzo haya yaliyonuiwa kuwa mema yakawa vita vya ngumi na maneno jambo geni pale kwa Moto.

Jambo hili lilimzuzua mwalimumkuu. Mwanawe aliamua kumvua nguo hadharani. Tangu aingie pale hakujawahi kisikika wanaotusiana acha kipigana. Akawachukua pale ofisini kwake na mara ofisi ikawa kliniki ya watoto wadogo. Wanafunzi wengine walisikiliza vilio hivyo kutoka

madarasani mwao. Haukupita muda kabla ya Nasieko, Rose na Kanene kuitwa.

Kesi kama hii ya utovu wa nidhamu ilistahili watoto kutumwa nyumbani kwa wiki mbili. Hivyo wazazi wa wanafunzi hawa walipigiwa simu kuja kuwachukua watoto wao saa sita kamili siku iliyofuata. Momanyi pale angemleta mama yake.

Kasisi Mwema alipopata ile simu ya mwalimu wa Rose hakuwa na budi kuwajibika. Akafunga safari. Safarini alikuwa na kila la kijilaumu kwa kukosekana kwake katika malezi ya mwana huyu aliyemkubali tu alipotoka jela akiwa na darasa la nane. Mama ya alikuwa muumini wake enzi zile alikuwa kasisi wa sarakasi. Alipogundua alikuwa na ujauzito wa Mwema, alimwendea na kumjuvya. Mwema naye kama kawaida akamkana na kumshurutisha aitoe ile mimba jambo ambalo yule msichana alipinga. Basi akaamua kutomtaja mahali yule kasisi wa kuzimu. Akapata mtoto msichana na kumlea. Pale Mwema alipotoka jela alimwendea mama Rose kwa msamaha na kumwahidi kuwajibika tangu pale.

Safari ilikuwa ndefu, naye akamua kusafiri mara mbili; kimwili na kiakili. Mawazo ya dada zake yakaanza kumpiga akilini ni kana kwamba waliachana jana. Alishanga ni vipi hata na utandawazi wote huu hukuweza kupata fununu ya waliko dada hawa. Alikumbuka walivyopendana utotoni, akaikumbuka michezo waliyocheza, akakumbuka walivyolia marehemu baba yao alipopigwa na mama bila huruma hali alikuwa mgonjwa wa shinikizo damu. Jinsi walivyompa chakula chao aliponyimwa na mama. Aliyakumbuka maneno ya baba. “Mwanangu pata nguvu. Nguvu ya mwanaume wa siku hizi imo akilini si katika misuli. Ninayopitia ni juu yenu wanangu, vingine ningetoroka nikaishi mbali na mama yenu. Lakini sitaki mkose mama na baba mkose. Heri nifie hapa mkiniona. Najua mtapata shida baada ya kifo changu. Ila kumbuka jua na mwezi ni macho ya Mungu yanayoona kila kitu na kwa wakati wake yatawapakulia wahitaji haki zao.’’

Akajaribu kuvuta sura za dada zake kutoka kwa kumbukumbu zake. Mpaka wawe wamebadilika sana. “Ama walikufa?’’ Hili wazo lilimshtua akamlaani shetani na kuliwingia mbali.

Amina naye aliushika usukani na kuvuta masafa kwa kasi. Aliondokea kuwa derava stadi. Mara nyingi Said hupendelea amwendeshe walipokuwa katika safari ndefu kama hii. Said alikuwa pale kando ya mkewe anasinzia. Walirauka asubuhi na mapema msimu ule wa Ramadhani na mara baada ya udhur wakang'oa nanga. Amina pale alikuwa na mawazo sawia na ya kaka yake. Wakati mwingi alipokumbuka ndugu zake Barasa na Nancy na maisha machungu ya utotoni alilia sana hadi ikamchukua mumewe kumfariji. Said alikuwa amegundua hili na kuwaonya ndugu zake dhidi kumkosea kwa namna iliyomfanya akumbuke aila yake. Amina aliomba Mungu kwamba siku moja awakutanishe na ndugu zake. Haijalishi hata kama ni katika umri mkuu bora awatie machoni aondoe lile fundo chungu moyoni na upweke wa miaka mingi. Aliishi katika uwalii.

Nancy kufunga mimba wao alikuwa na machache ya kukumbuka. Anachokumbuka tu ni kwamba alikuwa na kaka na dada ambao walitoroka wakamwacha na mama mkali. Anakumbuka akitoka kwenda kuwatafuta baada ya mama kukaa siku mbili hajarudi nyumbani na yule ndugu yake mdogo. Baba yake na alikuwa dhaifu na mhitaji asiweze kusukuma kitimaguru chake alichotumia kutoka baada ya ajali ile kule kazini enzi zile alipofanya na shirika la reli kama makanika. Nancy hakuwahi kumwona baba yake kwa miguu miwili.

Alikumbuka akiabiri basi la Takuja. Makanga alishtukia baada ya kuzusha abiria wote bado kulikuwa na mtoto kwa gari. Mtoto huyu hangeweza kueleza alikotoka wala alikokwenda. Alichosema tu ni kuwa aliwatafuta ndugu zake Barasa na Apondi waende nyumbani kwa sababu baba yao alitaka chakula na dawa. Akiuliziwa mama alilia na kusema hakutaka mama. Nancy alipelekwa katika kituo cha polisi na baadaye kwa mama Hani mtawa aliyewahifadhi watoto yatima na waliotupwa au kupotea kama yeye. Sasa Nancy ni mwalimu wa Kemia na Hasabati kama alivyokuwa mama yake.

Saa tano kamili Mwema aliligusa lango la shule na kuonyeshwa pambajio. Dakika chache baadaye mwanamke mfupi na wa rangi ya maji ya kunde akajiunga naye pale pamabajioni. Moyo ulimwenda mbio Mwema. Akamwangalia tena yule mwanamke aliyeonekana kubabaishwa na jambo fulani akilini. Macho ya kakutana sasa. "Nancy!" Mwema akaita kwa kutoamini. "Naam mwenzangu, waonekana kunijua ila mimi kidogo huji akilini. Tumepatana wa wapi?'' Aliuliza bila hisia zozote.''

“Nakujua sana! Wewe ni dada yangu aliyepotea. Mimi ni kaka yako Barasa.’’ Kwa maneno haya wakavaa wazimawazima.’’ Ah, Mungu ni mkubwa ati,” alisema Nancy. Singeamini ningekupata tena kaka yangu, ni kitambo hata sura yako siikumbuki. Habari ya Apondi?’’ Aliuliza kwa pupa. “Sijapata kumwona tangu tulipokivuka kisingiti cha mlango wa kwetu.

Wakiwa katika mazungumzo hayo, watu wawili waliwakaribia, mwanamke aliyevaa buibui na kujitanda mtadio kichwani na mwanamume wa asili ya kikushiti. Walikuwa wanazungumza Kisomali.

Amina alishtuka akaupanua mdomo wazi. Mwema naye sawia. Kikapita kimya kama cha dakika. Kila mmoja akijaribu kuongea sauti ikapotea, miguu nayo ikawa nanga, vilivyoyumba tu vilikuwa vichwa vya hawa wawili.

Said akaona avunje kimya. “Kwani mnajuana au nini?’’ Hapo Amina akafanya hatua kumrukia Mwema. “Kaka yangu!” Akazimia kifuani mwake. Kadhia hizi ziliwatoa walimu waliokuwa majilisini kuja kujionea.

Alipoziduka alimtambua Nancy, akamshika akambusu wote wakalia kwa sauti kuu kutakasa moyo na hisia. Maisha waliyopitia yakapita akilini. Wakalia zaidi. Kabla hawajapata kusimuliana walivyofika pale katibu wa mwalimu mkuu aliwaita pale ofisini. Kuingia mle tu, Mwema alimtambua Moto mwalimu wake na kumsalimia kwa heshima. Mlango ulibishwa na Ashley akaingia. “Ashley!!!’’ Mwema na Amina walitamka kwa pamoja.

Moto alionekana kuchanganyikiwa. “Mwamjua mke wangu!’’Hapo Ashley akasema, “*Its a long story darling…for another day.”* Kumbe hakuwahi mwambia alikuwa ameolewa na Mwema kwa miaka miwili. Alivyojua Moto ni kwamba Ashley alikuwa ametorokea kwa nyanya yake alikojifungulia Momanyi. “Nanyi mnaonekana kujuana pia!’’ Moto alizidi kusaili. Mwema akasema, “Kweli alivyosema mkeo Ashley ni kisa kirefu sana. Kisa cha majaliwa. Kirefu kisichohitaji ofisi sababu tilivyo hapa sote tu familia moja na mambo ya familia na ofisi hayashikani mikono. Moto hakubisha. Yeye pia ana kisa kisichojulika na wengi. Alivyomtunga Ashley Mimba. Alikumbuka. Ndio, alikumbuka jinsi vipindi vya ziada mle ofisini mwa idara ya Hisabati vilivyogeuka na

kuwa vya kimapenzi. Ashley hakuwa mzuri katika somo la Hisabati. Kwa kuwa alikuwa kidato cha nne, alikuwa na kila sababu ya kutafuta usaidizi wa Moto. Jambo moja liligeuka jingine. Kila jioni Ashley aliyeyukia ofisini kwa Moto. Almuradi alikuwa na swali hili au lile kwa mwalimu wake. Naye mwalimu alimfunza kila kitu! Kitambo kidogo Ashley akaanza senesene, si kutapika si kuchukia harufu mbalimbali si uvivu wa kuamka. Akamwendea Moto aliyeshtuka ghaya. Moto alimhakikishia kuwa angemwoa baada ya kukamilisha masomo yake na kujifungua kwa kuwa hakuwa bado amepata jiko. Ila moyo wa Ashley haukuwa kwake bali kwa Mwema mwanafunzi mwenzake katika kidato cha nne. Alifuata moyo wake. Alipoukamilisha mtihani wake akamfuata Mwema. Riziki ilimpiga Mwema chenga kweli kweli. Alisikika akisema kwamba tangu pesa zianze kuchorwa sanamu za wanyama pori zilitorokea msituni. Ashley naye akaona hawezi kula mapenzi na mwanawe. Akamsaka Moto aliyekuwa anasuburi muda mwafaka ampose na kumuoa rasmi. Bila kupoteza wakati tena Moto alirasmisha kila kitu kulingana na mila na sheria. Ashley akawa mkewe. Ni kweli kabisa alivyosema Ashley. Ni kisa kirefu. Kisa cha kijamii. Kuwepo kwa hawa watu tena katika ofisi hii ya mwalimu mkuu, kuzungumza wanayoelekea kuzungumza, ni matumizi mabaya ya ofisi. Wote waliongozana nyumbani kwa mwalimu mkuu isipokuwa watoto.

***

Siku hiyo Dharura alikuwa akiandaa sherehe ya kuadhimisha mwongo mmoja unusu tangu awe balozi wa heri jema wa UNEP na mwongo mmoja kama mwakilishi wa kina mama wa Pemba bungeni. Miongoni mwa aliowalika ni gavana wa sasa, aliyekuwa wakati mmoja gavana King'ori na Mwema, Mheshimiwa Karani, Mercy mkewe Mbalu na wengineo. Basil naye alitumia sherehe ile kuwashukuru watu kwa kuunga mkono juhudi za kufufua msitu wa Hidaya ulioimarika pakubwa sasa. Kadhalika, Basil alimvulia Dharura kofia kwa mfumo wake wa uongozi uliobadilisha Pemba nzima. Alitazamia kustaafu karibuni na kurudi kwao ulaya.

Tunu chini ya uongozi wa Dharura imepiga hatua kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na kipindi cha mtangulizi wake. Sasa watu walimtaka awe gavana wao. Jambo hili halijamkaa vyema gavana wa sasa kwani aliona hatari ya kushindwa. Ni juzi tu alijaribu kumwekea tuhuma za ufisadi ambazo zilileta maandamano kote Pemba. Uchunguzi ulipofanywa

kuhusiana na tetesi hizi zilimpata mwanamke huyu mweupe zaidi ya pamba. Dharura alipokuwa alijua alikuwa na kibarua. Kibarua cha kujilinda na adui yake mpya.

Hata hivyo aliapa kuwania kiti kile kwa vyovyote. Alihisi aliyetumwa kutakasa siasa ya Pemba. Njia nayo aliijua; kuwahudumia watu wake kwa uadilifu. Pale katika sherehe ile alizidua kampeni yake ya ugavana wa Pemba. Asichokijua ni kwamba adui yake alikuwa ashamtenda ya kutendwa. Akiwa pale tu jukwaani alipokea taarifa ya kifo cha Mumewe aliyefumaniwa dukani kwake na watu wasiojulikana na kipigwa risasi.

Saa moja baadaye ingekuja tanzia nyingine. Ajali mbaya ya barabarani iliyohushisha gari la Mwanawe alipokuwa njiani kuhudhuria hafla hii. Dharura aliishiwa na nguvu za mwili na roho. Lakini alijizoazoa, akajikaza japo kwa nguvu nyingi mpaka pale sherehe zipokwisha. Akafululiza hadi hospitalini. Maishani mwake ameona mengi. Ukiwa, mauti, njaa na dhuluma vilimjua kwa jina, naye akavijua kwa ladha na mionjo.

Dharura alihitaji hakimu. Alimpata yule hakimu wa mahakimu. Hakimu huyu alikuwa tayari kusikiliza na kuhukumu kulingana na haki. Wakili wa mwanga naye -Majaliwa- alikuwa ameishi kutetea haki tangu mwanzo wa dahari. Wakili huyu ndiye wake. Hangehongeka. Hakuhitaji malipo ya pesa. Malipo yake yalikuwa ni ile furaha usoni mwa wateja wake. Yeye ni tabia yake kuwapa hata walio makaburini tabasamu. Wao ni jamaa na jamii ya walionyimwa stahiki yao pia. Walionyamazishwa milele wasiseme ukweli. Waliosusia mabaya ya wabaya wakafikwa na mabaya. Dharura hakuhitaji huruma. Alihitaji haki tu. Hakuwa tayari kumlamba yeyote kisigino.

Yeye wakati huo alikuwa risasi iliyofyatuliwa. Imo hewani. Sharti ilenge.

# MWISHO